# KANISA

## *KUELEKEA MAONO YA PAMOJA*

Baraza
la Makanisa Duniani

# KANISA
## *KUELEKEA MAONO YA PAMOJA*

Andiko Kuhusu Imani na Utaratibu wa Kanisa, Na. 214.

Tafsiri ya Toleo la Kiswahili na
Mchg. Dkt Faustin Mahali

Maandiko ya **Baraza la Makanisa Duniani**

KANISA

Kuelekea Maono ya Pamoja

Andiko Kuhusu Imani na Utaratibu wa Kanisa Na. 214

Hakimiliki © 2013 Machapisho ya Baraza la Makanisa Duniani (BMD). Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunukuu sehemu ya kitabu bila ruhusu ya mpiga chapa, isipokuwa kwa nukuu fupi au mapitio ya sehemu yake, omba kibali: publications@wcc-coe.org.

*Machapisho ya BMD ni mpango unaohusika na kuchapisha vitabu vya Baraza la Makanisa Duniani. Toka kuanzishwa kwake mwaka 1948, BMD linaendeleza umoja wa Kikristo katika Imani, ushuhuda na huduma kwa ajili ya kuijenga dunia inayoheshimu misingi ya haki na amani.Ikiwa ni ushirika wa dunia nzima, BMD linayaleta pamoja makanisa zaidi ya 349 ya Kiprotestanti, Kiorthodiksi, Kiangalikana na mengineyo yanayowakilisha zaidi ya Wakristo milioni 560 katika nchi 110 na linafanya kazi kwa karibu na Kanisa Katoliki.*

Mistari ya Biblia ni kutoka "New Revised Standard Version" © Hakimiliki 1989 ya Dawati la Elimu ya Kikristo la Baraza la Kitaifa ya Makanisa ya Kristo Marekani kwa kibali maalumu.

Mchoro wa Jalada na Usanifu wa Kitabu cha Kiswahili:
Mchg Dkt. Faustin Mahali

ISBN: 978-2-8254-1587-0

World Council of Churches
150 route de Ferney, P.O. Box 2100
1211 Geneva 2, Switzerland
http://publications.oikoumene.org

# Yaliyomo


***Dibaji*** **.......... v**

***Neno la Utangulizi*** **.......... vii**

**Utangulizi .......... 1**

**Sura ya I .......... 6**

**Misheni ya Mungu na Umoja wa Kanisa .......... 6**

A. Kanisa Limekusudiwa na Mungu .......... 6

B. Misheni ya Kanisa katika Historia .......... 9

C. Umuhimu wa Umoja .......... 11

**Sura ya II .......... 14**

**Kanisa la Utatu Mtakatifu .......... 14**

A. Kutambua Mapenzi ya Mungu kwa Kanisa .......... 14

B. Kanisa kama *Ushirika* wa Utatu wa Mungu .......... 15

*Uwezo wa Mungu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu .......... 15*

*Unabii, Utume na Ufuasi wa Watu wa Mungu .......... 18*

*Mwili wa Kristo na Hekalu la Roho Mtakatifu .......... 22*

*Kanisa Moja, Takatifu, la Kikatoliki na la Kimitume .......... 23*

*Jinsi muendelezo wa mapokeo na mabadiliko yanavyohusiana na mapenzi ya Mungu .......... 26*

C. Kanisa kama Ishara na Mhudumu wa Mpango wa Mungu kwa ajili ya Dunia .......... 26

*Usemi kuhusu "Kanisa kama Sakramenti" .......... 29*

D. Kanisa kama Ishara na Mhudumu wa Mpango wa Mungu kwa ajili ya Dunia .......... 29

*Uhalali na Hali ya Tofauti Iletayo Mgawanyiko .......... 32*

E. Ushirika wa Makanisa ya Kikanda .......... 32

*Uhusiano wa Kanisa la Eneo na la Kiulimwengu .......... 35*

**Sura ya III .......... 36**

**Kanisa: Kukua katika Ushirika .......... 36**

A. Tayari lakini Bado ........................................................... 36
B. Kukua Katika Mambo Muhimu ya Ushirika: Imani, Sakramenti, na Huduma ........................................................ 38
*Imani* ........................................................................................ 39
*Sakramenti* ................................................................................ 42
*Sakramenti na Taratibu za Ibada* ........................................ 46
*Huduma ndani ya Kanisa* .................................................... 47
**Sura ya IV ........................................................................ 62**
**Kanisa: Duniani na kwa ajili ya Dunia ............................. 62**
A. Mpango wa Mungu kwa ajili ya Uumbaji: Ufalme ........... 62
B. Changamoto ya Kimaadili ya Injili .................................. 65
C. Kanisa katika Jamii .......................................................... 67
**Hitimisho ........................................................................... 71**
**Mchakato Ulioleta Andiko la Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja ............................................................................... 73**

## *Dibaji*

Katika ziara zangu za kuzungukia makanisa duniani, nimeona changamoto nyingi juu ya umoja kati ya makanisa na makanisa na ndani ya makanisa yenyewe. Mazungumzo ya pamoja ya kiekumene kati ya makanisa na taasisi zake ni ukweli ulio wazi na yanachangia pia katika mahusiano kati yake hata nje ya mipaka yake. Katika hali hii, mahusiano mapya hujengwa. Hata hivyo kuna hali ya wazi na ya msingi miongoni mwake ya kukosa uvumilivu kwani yanahitaji kuona vuguvugu zaidi katika kufikia mazungumzo ya pamoja na maridhiano. Baadhi ya makanisa na taasisi zake yanaona kuwa kuna maswali mapya ambayo yanaweza kuleta mpasuko zaidi. Vuguvugu la kiekumene linaonekana kukosa nguvu katika baadhi ya makanisa hakuna wasemaji wenye utayari kulisemea kama vipindi vya nyuma. Kuna hali ya kuelekea kwenye mipasuko na kuangalia zaidi vitu vinavyounganisha watu wachache kuliko watu wengi. Bila shaka, wito wa kuungana hauishii tu kwa kuzaliwa kwa changamoto mpya, bali kinyume chake. Hata hivyo tunahitaji pia kuona mihimili mingine ya wito wa kuelekea umoja wenye nguvu na kujikumbusha wenyewe kuwa tunakumbatiwa na upendo na tunaitwa kupendana (1 Kor. 13).

Katika mukitadha huu, Kamisheni ya BMD juu ya Imani na Utaratibu wa Kanisa inaleta kwetu tuzo, ambayo ni tamko kuhusu Kanisa: ni tunda la miaka mingi la kazi kuhusu elimu ya kanisa. Kama chimbuko kutoka chapisho la *Ubatizo, Ekaristi na Huduma* (1982) na itikio la makanisa la chapisho hili, chapisho la *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* lilipokelewa kwenye Kamati Kuu ya 2012 na kisha kupelekwa kwenye makanisa ili kuendeleza mjadala zaidi kuhusu Kanisa na kuomba majibu yao kuhusu andiko hili. Utafiti huu na mchakato wa majibu yake utachangia kwa kiwango kikubwa kwa miaka ijayo kuamua juu ya hatua zaidi kuelekea umoja ulio wazi zaidi. Kazi ya utafiti wa kikanisa unahusu mambo yote

yahusuyo Kanisa na kazi zake za misheni ndani yake na kwa ajili ya ulimwengu wote. Hivyo, chapisho hili la *Kanisa* lina mizizi yake katika asili na misheni ya Kanisa. Linaakisi malengo ya kikatiba na utambulisho wa BMD kama ushirika wa makanisa ambao unayaita makanisa kufikia lengo la umoja unaoonekana.

Umoja ni kipawa cha maisha, na pia ni kipawa kitokanacho na upendo, na wala hautokani na misingi ya kufikia miafaka au makubaliano kati ya kanisa na kanisa. Kama ushirika uliojengwa na makanisa tunaitwa kuueleza umoja unaohusu maisha ambao tumepewa kwa njia ya Yesu Kristo aliyejitoa maisha yake pale msalabani na katika ufufuko wake ili tuweze kushinda dhidi ya ubaya wetu, dhambi zetu na maovu yetu. Kwa kuwa kama andiko hili la *Kanisa* linavyotangaza: "Ufalme wa Mungu ambao Yesu ameufunua kwa njia ya Neno la Mungu kwa mifano na kuusimika kwa njia ya matendo yake yenye nguvu, na hasa kwa njia ya fumbo la pasaka katika kifo na ufufuko wake, ndio hasa lengo la mwisho la ulimwengu wote kuufikia. Kanisa limekusudiwa na Mungu si kwa ajili yake lenyewe, lakini kwa ajili ya kutumikia mpango wa Mungu wa kuubadili ulimwengu" (§ 58).

*Olav Fykse Tveit*
Katibu Mkuu
Baraza la Makanisa Duniani

## *Neno la Utangulizi*

Muunganiko wa andiko hili la *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* ni sehemu ya malengo ya kibiblia juu ya umoja wa Wakristo: "Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja" (1 Kor 12:12-13).

Kusudi la msingi la Kamisheni juu ya Imani na Utaratibu wa Kanisa ni "kuyahudumia makanisa wakati yakiitana kwa ajili ya umoja ulio wazi kwa njia ya imani moja na kwa njia ya ushirika wa pamoja katika Ekaristi Takatifu, unaojieleza katika ibada na maisha ya pamoja katika Kristo; kwa njia ya ushuhuda na huduma kwa dunia nzima, na kuelekea katika utimilifu wa umoja huo ili ulimwengu uweze kuamini" (Kanuni 2012).

Lengo la huu wito wa pamoja kuelekea umoja wa wazi unaambatana na ulazima wa kutambuana kama makanisa, kama kielelezo cha kweli cha Ukiri wa Imani unaotuita kuwa kanisa "lililo moja, takatifu, la ulimwengu wote [katoliki], na la kimitume." Pamoja na Ukiri huu wa Imani bado katika hali isiyo ya kawaida ya mgawanyiko wa kikanisa, tafsiri za kanisa juu ya asili na misheni ya Kanisa vimeongeza mashaka kuwa mafundisho mbalimbali ya makanisa si tu yanatofautiana, bali pia hayapatani. Hivyo kufikia muafaka juu ya mafundisho ni jambo lililotambuliwa kwa muda mrefu kuwa ni lengo la msingi la kitheologia katika kutafuta umoja wa Kikristo. Kitabu hiki cha pili kinachounganisha *Imani na Utaratibu wa Kanisa* ni matokeo ya kitabu cha kwanza juu ya *Ubatizo, Ekaristi, na Huduma* (1982), na majibu rasmi juu yake, ambayo yaliyatambua maeneo ya msingi katika mafundisho ya kanisa

yaliyohitaji utafiti zaidi;[1] na pia kinatokana na maswali yaliyotokana na mafundisho ya kanisa yaliyojitokeza katika andiko la kitafiti kiitwacho *Ubatizo Mmoja: Kuelekea Kutambuana na Kuheshimiana* (2011).

Kwa miaka ishirini sasa, uwakilishi toka makanisa ya Kiothodoksi, Kiprotestanti, Kianglikana, Kiinjili, Kipentekoste na Kikatoliki, katika Kongamano la Dunia kuhusu Imani na Utaratibu wa Kanisa (1993), vikao vitatu vya ndani vya Kamisheni juu ya Imani na Utaratibu wa Kanisa (1996, 2004, 2009), na mikutano kumi na nane ya Kamisheni iliyosimikwa, na vikao vya kutengeneza rasimu mbalimbali vilitafuta kuyafunua maono ya asili, kusudi, na misheni ya Kanisa kiulimwengu, kimataifa, na kiekumene. Makanisa yametoa majibu ya kina na ya kujenga katika hatua mbili za mwanzo juu ya njia ya namna ya kuwa na tamko la pamoja. Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Kanisa inaitikia wito wa makanisa na andiko hili, *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja*, ni andiko la pamoja, linalokutanisha, na ni tamko juu ya mafundisho ya Kanisa. Muunganiko huu uliofikiwa katika andiko hili la *Kanisa* yanawakilisha matokeo yasiyo ya kawaida ya kiekumene.

Kuna malengo mawili tofauti, lakini yanayohusiana katika utume wa andiko la *Kanisa* kwa makanisa kwa ajili ya utafiti na itikio rasmi la makanisa hayo. Lengo la kwanza ni uamsho mpya. Andiko hili la *Kanisa*, ambalo ni la kimataifa na kiekumene, haliwezi kuhusishwa na utamaduni wa mafundisho fulani ya pekee. Tangu mwaka 1993 had 2012, maelezo ya kitheologia na uzoefu wa makanisa mbalimbali yamewekwa pamoja kiasi kwamba makanisa yanayosoma andiko hili yanaweza kujikuta yakipewa changamoto ya kuyaishi maisha ya

[1]Linganisha, *Baptism, Eucharist & Ministry, 1982-1990: Report on the Process and Responses*. Faith and Order Paper No. 149. WCC: Geneva, 1990, 147-151.

kikanisa kwa ukamilifu; mengine yataona baadhi ya mambo ambayo yamekuwa yakipuuzwa au kusahauliwa; na makanisa mengine yanaweza kuona yameimarishwa na kuthibitishwa. Kama Wakristo wanaoendelea kukua katika maisha ya imani yao katika Kristo, watajikuta wakisogeleana wenyewe kwa wenyewe kwa ukaribu zaidi, na pia kuishi katika mfano wa kibiblia wa mwili mmoja: "Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa katika Roho mmoja."

Lengo la pili ni la makubaliano ya kitheologia juu ya Kanisa. Kama ilivyo kwenye umuhimu wa mapatano yaliyofikiwa katika andiko la Imani na Utaratibu wa Kanisa kwenye *Ubatizo, Ekaristi na Huduma*, majibu rasmi ya makanisa katika mchakato huu yana nafasi yake pia. Machapisho sita ya itikio la makanisa yameonyesha maeneo mbalimbali ya muafaka kati yao kwenye masuala ya msingi ya ubatizo, ekaristi na huduma. Athari chanya ya mapatano ya makanisa yaliyojitokeza katika andiko la *Ubatizo, Ekaristi na Huduma* kuelekea umoja wa Kikristo, nyaraka zake zimetunzwa vizuri na mchakato wake ni endelevu. Itikio miongoni mwa makanisa kutokana na andiko la *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* halitatathimini tu mapatano ya yaliyofikiwa kwenye andiko la *Imani na Utaratibu wa Kanisa*, bali litatafakari pia kiwango cha makubaliano juu ya mafundisho ya Kanisa. Kama ilivyo katika mapatano kuhusu ubatizo, itikio la andiko la *Ubatizo, Ekaristi na Huduma* lilileta mwamko mpya kuhusu kutambuana kati ya makanisa, yakihimizana kuwa na umoja ulio wazi katika imani moja na ekaristi moja.

"Majibu ya kikanisa" yaliyotokana na Kamisheni ya *Imani na Utaratibu wa Kanisa* yalihusisha makanisa ambayo yalikuwa sehemu ya Kamisheni na jumuiya za makanisa ya Baraza la

Makanisa Dunia. Inatumainiwa kuwa hata makanisa mapya yaliyojumuika katika vuguvugu hili la kiekumene yataukubali mwaliko wa kutafiti na kutoa maoni juu ya andiko hili. Kamisheni pia inaalika mawazo toka katika taasisi za makanisa, kama vile mabaraza ya kitaifa na kikanda na Jumuiya za Kikristo Duniani, ambazo mazungumzo ndani ya vyombo vyake yamechangia sana katika kufikia mapatano ya tafsiri iliyopo kwenye andiko hili la *Kanisa.* Maswali ya kipekee yaliyoulizwa kwa makanisa kwenye andiko la *Imani na Utaratibu wa Kanisa* ili kuuongoza mchakato huu yanapatikana mwishoni mwa Utangulizi wa Andiko hili la *Kanisa*. Maswali kwa ajili ya utafiti ni ya kitheologia, kivitendo, na kichungaji. Kamisheni iliomba kuwa majibu rasmi yatumwe kwa sekretarieti iliyopo katika Baraza la Makanisa Duniani kufikia tarehe 31 Desemba 2015.

Kwa kuwa kuandaa andiko hili imechukua miongo miwili, tunapenda kutoa shukrani zetu kwa wale wote ambao wameubeba mchakakato huu kwa maombi na kwa njia ya vipawa vyao vya kitheologia: tunawashukuru Wanakamisheni wa Imani na Utaratibu wa Kanisa, makanisa na watheolojia waliotoa majibu ya utafiti wa andiko la *Asili na Kusudi la Kanisa* (1998) na *Asili na Misheni ya Kanisa* (2005), wajumbe wa sekretarieti ya Imani na Utaratibu wa Kanisa, na wenzetu waliotangulia kuongoza mchakato huu na kuuratibisha na wakuu wa idara za Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Kanisa.

*Canon John Gibaut*
Mkurugenzi wa Kamisheni juu Imani na Utaratibu wa Ibada

*Metropolitan Dr Vasilios wa Constantia Ammochostos*
Msimamizi wa Kamisheni juu ya Imani na Ibada

**Utangulizi**

"Mapenzi yako yatimizwe" ni maneno wanayoomba kila siku waumini wengi wasiohesabika kutoka makanisa ya Kikristo. Yesu mwenyewe aliomba maneno haya katika bustani ya Getsemane muda mfupi kabla hajakamatwa (ling. Mt 26:39-42; Marko 14:36; Luka 22:42). Katika injili ya Yohana, Yesu anayafunua mapenzi ya Baba kwa Kanisa pale alipoomba juu ya wanafunzi wake kuwa wamoja, ili ulimwengu upate kuamini (ling. Yohana 17:21). Kuomba ili mapenzi ya Bwana yatimizwe kunahitaji juhudi zitokazo moyoni ili kuyakubali mapenzi yake kwa ajili ya na kwa kipawa cha umoja. Andiko la sasa – *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja*–linajaribu kutatua moja ya matatizo yanayofikiriwa kuwa ni magumu yanayoyakabili makanisa katika kuondoa vikwazo vilivyobaki katika kukiishi kipawa cha ushirika kitokacho kwa Bwana: yaani uelewa wa asili wa Kanisa lenyewe. Umuhimu mkubwa wa kipawa na lengo hili unaangazia maana ya mambo ambayo yanatakiwa yashughulikiwe katika kurasa zinazofuata.

Lengo letu si kutoa andiko la muungano, maana yake, andiko ambalo, wakati likiwa halielezei makubaliano kamili juu ya masuala yote yaliyofikiriwa, ni zaidi ya chombo kwa ajili ya tu kuamsha utafiti zaidi. Bali, kurasa hizi zinaeleza ni kwa kiwango gani jumuiya za Kikristo zimefikia katika uelewa wa pamoja kuhusu Kanisa, kuonyesha hatua zilizofikiwa na pia kuonyesha kazi ambayo bado inahitajika kufanywa. Andiko la sasa limechambuliwa na Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Kanisa, ambayo kusudi lake, kama lilivyo kusudi la Baraza la Makanisa Duniani kwa ujumla, ni kuyahudumia makanisa "yanapoitana kwa ajili ya umoja ulio wazi katika imani moja na ushirika wa ekaristi moja, inayojieleza katika ibada na katika maisha ya pamoja katika Kristo, kwa njia ya ushuhuda na huduma kwa dunia nzima, na katika kusonga mbele kuelekea

umoja kamili ili dunia iweze kuamini."[1] Umoja huu ulio wazi unapata maelezo yenye ustadi wakati wa kushiriki ekaristi takatifu, ushiriki ambao unamtukuza Mungu wa Utatu na kuliwezesha Kanisa kushiriki katika Misheni ya Mungu kwa ajili ya kuleta mabadiliko na wokovu wa dunia nzima. Tamko la sasa limetumia majibu ya makanisa kwa kazi ya andiko la Imani na Utaratibu wa Kanisa juu ya mafundisho yake katika miaka ya karibuni na nyaraka za mwanzoni za makubaliano ya kiekumene ambazo zote zilitafuta makubaliano kwa njia ya kutafakari Neno la Mungu, kwa matumaini kuwa, kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu, kipawa cha Mungu cha umoja kinaweza kufikiwa. Kwa hiyo haya ni matokeo ya mazungumzo katika ngazi ya kimataifa, na hasa majibu ya makanisa yaliyotokana na utafiti juu ya *Asili na Misheni ya Kanisa*, michango ya mawazo iliyotolewa katika mkutano wa wazi wa kamisheni juu ya Imani na Utaratibu wa Kanisa uliofanyika Krete mwaka 2009 na michango mbalimbali toka kanisa la Orthodoksi katika kongamano liliyofanyika Cyprus mwaka 2011. Kwa kuongezea, andiko hili linajenga msingi wake kwenye mazungumzo mengi yaliyofanyika kati ya kanisa moja na jingine yaliyojikita kwenye hoja ya "Kanisa Moja" hasa katika miongo ya hivi karibuni.[2]

Ni matumaini yetu kuwa kitabu hiki cha *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* kitayasaidia makanisa kwa njia tatu: (1) kwa kutoa majumlisho ya matokeo ya mazungumzo ya kiekumene kuhusu mada mbalimbali za mafundisho ya kanisa katika miongo ya karibuni; (2) kualika mada ili kutathimini matokeo ya mazungumzo haya – kuyathibitisha matokeo

[1]L. N. Rivera-Pagán (mhariri.), *God in Your Grace: Official Report of the Ninth Assembly of the World Council of Churches*, Geneva, WCC, 2007, 448.

[2]Kwa ajili ya maelezo zaidi juu ya mchakato huu, angalia maelezo ya kihistoria yanayopatikana mwisho wa kila andiko.

mazuri, kuainisha mapungufu na au kuonyesha maeneo ambayo hayajaangaliwa kwa kina; na (3) kutoa fursa kwa makanisa kutafakari kuhusu uelewa wa makanisa yenyewe juu ya mapenzi ya Bwana ili kukua pamoja kuelekea umoja mpana zaidi (ling. Ef. 4:12-16). Nimatumaini kuwa kwa mchakato huu wa habari, majibu na ukuaji, kwa kukubali, kuboresha na kutoa changamoto kwa makanisa yote, andiko hili litaleta mchango mkubwa na hata kuwezesha kufikiwa kwa baadhi ya hatua za kimaamuzi kuelekea kufikia umoja ulio kamili.

Kitabu hiki kimepangwa kwa kufuata mada zinazojadiliwa kuhusu masuala ya kikanisa. Kitabu hiki cha *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* katika sura yake ya kwanza kinachunguza jinsi jumuiya ya Kikristo inavyoasilishwa na misheni ya Mungu katika kuleta mabadiliko ya kuiokoa dunia. Kimsingi Kanisa ni la kimishenari, na umoja wake unahusiana kwa karibu na misheni hii. Sura ya pili inaweka bayana vipengele muhimu katika kulielewa Kanisa kama Jumuiya, ikikusanya matokeo ya tafsiri zote jinsi maandiko ya Biblia na yahusuyo Kanisa yanavyolihusianisha Kanisa na Mungu na baadhi ya madhara ya mahusiano haya katika maisha na mifumo ya Kanisa. Sura ya tatu inaangalia kwa kina juu ya ukuaji wa Kanisa kama hija ambamo watu wanauendea ufalme wa Mungu, na hasa juu ya baadhi ya maswali magumu ya mafundisho ya kanisa ambayo yameleta mgawanyiko wa makanisa katika kipindi cha nyuma. Sura hii inasajili maendeleo kuelekea mapatano zaidi kuhusu baadhi ya mambo haya na kufafanua vipengele ambavyo makanisa yanaweza kuvihitaji ili kutafuta kukaribiana zaidi. Sura ya nne inaendeleza njia kadhaa muhimu zinazotumika na Kanisa ili kuhusiana na dunia kama alama na wakala wa upendo wa Mungu, kama vile kumtangaza Kristo ndani ya madhehebu na dini zingine, kushuhudia maadili ya msingi ya Injili na kutoa majibu ya mateso na mahitaji ya mwanadamu.

Majibu mengi kutoka makanisani kuhusu Imani na Utaratibu wa Kanisa yaliyotokana na utafiti wa *Ubatizo, Ekaristi na Huduma*, ya mwaka 1982, yalionyesha kuwa mchakato wa mapokezi uliofuata baada ya chapisho kuhusu mapatano ni muhimu kama vile mchakato ulioongoza uzalishaji wenyewe.[3] Ili kuufanya kuwa nyenzo kwa ajili ya mazungumzo ya kweli kuhusu mafundisho ya kanisa ambapo makanisa yote yanaweza kutoa mchango muhimu, makanisa yanatakiwa kwa haraka si tu kutoa mawazo yao ya kina kuhusu kitabu hiki cha *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja*, bali kuleta majibu rasmi kwa Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Kanisa, kwa kuzingatia maswali yafuatayo:

- Ni kwa kiwango gani andiko hili linaakisi mafundisho ya kanisa lako?
- Ni kwa kiwango gani linatoa msingi wa kukua kwa umoja miongoni mwa makanisa?
- Ni katika mazingira au uamsho wa namna gani kanisa lako linapewa changamoto na tamko hili ili liweze kuzifanyia kazi?
- Ni kwa kiwango gani kanisa lako linaweza kushirikiana kwa karibu na makanisa ambayo kwa namna moja au nyingine yanakubaliana kwa kiwango kikubwa na tamko hili la Kanisa?
- Ni mambo gani yahusuyo Kanisa yanaweza kuchukuliwa na kujadiliwa kwa upana zaidi, na kanisa lako linaweza kutoa ushauri gani kwenye mjadala kuhusu elimu ya imani na utaratibu wa kiibada katika kanisa?

[3] M. Thurian (mhariri.), *Churches Respond to BEM: Official Responses to the "Baptism, Eucharist and Ministry" Text*, Geneva, World Council of churches, vols. I-VI, 1986-1988; *Batism, Eucharist & Ministry 1982-1990: Report on the Process and Responses*, Geneva, WCC, 1990.

Pamoja na maswali haya ya jumla, wasomoji wataona maswali yaliyochapishwa kwa aina ya kipekee katika andiko hili, na kwenye aya kuhusu mambo ya muhimu ambayo yanaufanya mgawanyiko wa kanisa ubakie kama ulivyo. Maswali haya yanalenga kuamsha mjadala na kuhimiza makubaliano zaidi kati ya makanisa katika njia yao ya pamoja kuelekea umoja kamili.

## Sura ya I

## Misheni ya Mungu na Umoja wa Kanisa

### A. Kanisa Limekusudiwa na Mungu

1. Uelewa wa Kikristo juu ya Kanisa na misheni yake unatokana na maono ya Mungu katika ufundi wake wa uumbaji wa ajabu (uwekevu) wa viumbe vyote: ni ufalme ulioahidiwa na kudhihirishwa ndani ya Yesu Kristo. Maandiko Matakatifu yanasema kuwa mwanadamu, mume na mke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (ling. Mw. 1:26-27), hivyo wana uwezo wa asili wa ushirika na Mungu na ushirika kati yao. Lengo la Mungu la uumbaji lilivurugwa na dhambi na kiburi cha mwanadamu cha kutomtii Mungu (ling Mw. 3-4; Rum 1:18-3:20), hali iliyoharibu mahusiano kati ya Mungu na wanadamu na utaratibu mzima wa uumbaji. Lakini Mungu alivumilia na kubaki mwaminifu licha ya dhambi na makosa ya mwanadamu. Historia yenye nguvu ya mabadili inajidhihirisha katika utunzaji wa Mungu wa ushirika wake na mwanadamu na uumbaji wote, katika kufanyika kwake kuwa mwili na fumbo la sadaka katika Kristo Yesu. Kanisa kama mwili wa Kristo, linatenda kwa nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuendeleza misheni ya kuleta uzima katika kutoa unabii na matendo ya huruma na hivyo kushiriki kazi ya Mungu ya uponyaji wa dunia iliyoharibika. Ushirika ambao asili yake ni maisha halisi ya Utatu Mtakatifu, ni tuzo iliyo ndani ya maisha ya Kanisa na wakati huo huo ni tuzo ambapo Mungu analiita Kanisa kujitolea sadaka kwa ajili ya kusaidia waliojeruhiwa na dunia iliyogawanyika, kwa matumaini kuwa patakuwepo na upatanisho na uponyaji ulio kamili.

2. Akiwa hapa duniani, "Yesu alitembea kila mahali katika miji yote na vijiji, akifundisha katika masinagogi na kuihubiri injili ya ufalme [wa Mungu] na akiponya kila udhaifu na

ugonjwa. Kila alipoona kundi alilionea huruma..." (Mt. 9:35-36). Kanisa linapata mamlaka kutokana na matendo ya ahadi ya Kristo mwenyewe, ambaye si tu alihubiri juu ya ufalme wa Mungu kwa maneno na matendo, bali pia aliwaita na kuwatuma wanaume kwa wanawake wakiwa wamejazwa na Roho Mtakatifu (Yohana 20:19-23). Kitabu cha Matendo ya Mitume kinatupa maneno ya mwisho ambayo Yesu aliwaambia mitume kabla hajapaa, "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Mdo 1:8). Injili zote nne zinamalizia na maneno yenye mamlaka ya kitume; Mathayo anakazia: "Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mt. 28:18-20); angalia pia Marko 16:15; Luka 24:45-49; na Yohana 20:19-21). Amri hii ya Yesu inafichua siri ya jinsi ambayo Yesu alitaka Kanisa lake liwe ili libebe na kupeleka misheni [ya Mungu]. Kanisa lilitakiwa liwe jamii ya wanaoshuhudia, na kuutangaza ufalme ambao Yesu aliutangaza hapo kwanza, likiwaalika watu kutoka mataifa yote kwenye imani iokoayo. Lilitakiwa kuwa jumuiya ya kiibada, inayotafuta waumini wapya kwa njia ya ubatizo katika Jina la Utatu Mtakatifu. Lilitakiwa kuwa jumuiya ya ufuasi, ambapo mitume, kwa njia ya kutangaza Neno [la Mungu], kubatiza na kusherehekea Chakula cha Bwana, wawaongoze waumini wapya kuyatii yote ambayo Yesu mwenyewe ameamuru.

3. Roho Mtakatifu aliwajia mitume asubuhi ya Pentekoste kwa lengo la kuwaimarisha ili kuanza kazi ya misheni aliyokuwa amewapa (ling. Mdo 2:1-41). Mpango wa Mungu wa kuuokoa

ulimwengu (ambao wakati mwingine hutajwa kwa kilatini kuwa *Missio Dei* au "misheni ya Mungu") unafanywa kwa njia ya [Mungu] kumtuma kwetu Mwana na Roho Mtakatifu. Shughuli ya kuokoa ya Utatu Mtakatifu ni muhimu katika kufikia uelewa mpana wa Kanisa. Kama ilivyoelezwa katika andiko la *Ukiri wa Imani Moja* katika kipengele cha Imani na Utaratibu wa Kanisa: "Wakristo wanaamini na kukiri kuwa kuna muunganiko usioweza kuvunjika kati ya kazi ya Mungu ndani ya Yesu kwa njia ya Roho Mtakatifu na uwepo halisi wa Kanisa. Huu ni ushuhuda wa Maandiko Matakatifu. Asili ya Kanisa ina mizizi katika mpango wa Utatu wa Mungu kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu."[1]

4. Yesu anaieleza misheni yake kuwa ni ya kuihubiri habari njema kwa maskini, kuwafungulia wafungwa, kuwapa vipofu uwezo wa kuona tena, kuwakomboa wanaokandamizwa na kutangaza mwaka wa Mungu unaokubalika (ling Luka 4:18-19, akinukuu Isaya 61:1-2). "Misheni ya Kanisa inatokana na asili ya Kanisa kuwa mwili wa Kristo, likishiriki katika huduma ya Kristo kama Mpatanishi kati ya Mungu na uumbaji wake. Katikati ya moyo wa wito wa Kanisa ni kuuhubiri ufalme wa Mungu uliowekwa wakfu na Yesu Bwana, aliyesulibiwa na kufufuka. Makanisa yanajaribu kutimiza wito huu wa kiuinjilisti kwa njia ya maisha yake ya ndani ya ibada ya ekaristi takatifu, sadaka, sala za kuombea watu na mambo mbalimbali, kwa njia ya kupanga misheni na uinjilisti, kwa njia ya maisha ya kushikamana kila siku na walio maskini, na kwa njia ya utetezi

[1] *Confessing the One Faith: An Ecumenical Explanation of the Apostolic Faith as It Is Confessed in the Nicene-Constantinopolitan Creed (381).* Geneva-Eugene, WCC-Wipf & Stock, 2010, §216.

na hata kupambana na nguvu za dola zinazokandamiza wanadamu."[2]§

**B. Misheni ya Kanisa katika Historia**

5. Toka mwanzo Kanisa limejitolea kutangaza habari njema ya wokovu katika Kristo kwa njia ya maneno na matendo, likisherehekea vipawa vya neema, yaani sakramenti, hasa eukaristi takatifu, na kujenga jumuiya za Kikristo. Juhudi hizi wakati mwingine zimekabiliwa na upinzani mkubwa; zimekwamishwa na wapinzani au hata kusalitiwa na uovu wa wanaotumwa kupeleka habari. Licha ya ugumu mwingi wa jinsi hiyo, utangazaji huu umetaleta matunda makubwa (ling Marko 4:8, 20, 26-32).

6. Moja ya changamoto ya Kanisa imekuwa jinsi ya kutangaza Injili ya Kristo katika hali inayoweza kuamsha mwitikio mzuri katika mazingira, lugha na tamaduni mbalimbali za watu wanaosikia habari hizi. Katika mahubiri yake pale Areopago (Mdo 17:22-34), Mtume Paulo, huku akitumia imani za wenyeji na maandiko yao, anaonyesha jinsi kizazi cha Wakristo wa kwanza kilivyojaribu kushirikisha habari njema za kifo cha Yesu na Ufufuko wake, na pale ilipofaa, wakijenga katika msingi huo, walileta mabadiliko katika mapokeo ya tamaduni za wasikilizaji wao wakiongozwa na Roho Mtakatifu, na hivyo kuamsha chachu kwa Wakristo ya kuendeleza mstakabali wa maisha bora ya kijamii walimoishi. Katika karne zilizofuata, Wakristo wameishuhudia Injili hadi ng'ambo ya mipaka yao kutoka Yerusalemu hadi kwenye miisho ya dunia (ling. Mdo 1:8). Mara nyingi ushuhuda wao juu ya Yesu uliwafanya kuwa wahanga wa mateso, wakimbizi na wa mauaji, lakini pia ushuhuda wao ulisababisha imani [ya

[2] "Mission and Evangelism: An Ecumenical Affirmation,"§6, in J. Matthey (mhariri.), *You Are the Light of the World: Statements on Mission by the World Council of Churches*, Geneva, WCC, 2005, 8.

injili] kuenea na kuanzishwa kwa Kanisa kila kona ya dunia. Kuna nyakati tamaduni na urithi wa kidini wa wale waliohubiriwa Injili havikupewa heshima stahiki, kwa kuwa wale waliokuwa wakitangaza injili walishiriki kuutumikia ubeberu wa kikoloni, ambao ulisambaratisha na hata kupoteza kabisa mila na desturi za watu hao kwa sababu ya nguvu kubwa ya mataifa vamizi ya kikoloni. Bila kujali matukio hayo, neema ya Mungu, yenye nguvu kuliko uovu wa mwanadamu, iliweza kuwainua wanafunzi wa kweli na marafiki wa Yesu katika nchi nyingi na Kanisa likajengeka katikati ya utajiri wa tamaduni nyingi. Utajiri wa tofauti hizi katika jumuiya moja ya Kikristo ulieleweka vizuri na baadhi ya waandishi wa mwanzo kama inavyosimuliwa katika Maandiko Matakatifu juu ya Yesu kama bibi arusi mzuri wa Kanisa (lin. Efe 5:27; na Ufu 21:2).[3] Leo waumini kutoka makanisa yale yaliyowakarimu wamishenari wa kigeni yamekuwa msaada tena kwa makanisa yale yaliyoweka mawakala wa kuleta Injili.[4]

7. Sasa utangazaji wa ufalme wa Mungu unaendelea kote duniani katikati ya mabadiliko makubwa [ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini]. Mabadiliko mengine yanaleta changamoto kwa misheni ya Kanisa na katika kujielewa kwake. Kuishi katikati ya mchanganyiko wa dini mbalimbali kunawapa Wakristo changamoto ya kutafakari kwa kina kuhusu uhusiano wa kutangaza kuwa Yesu ni yeye pekee Mwokozi wa ulimwengu, kwa upande mmoja, na madai ya imani zingine kwa upande mwingine. Kutengeneza njia ya namna ya kuimarisha mawasiliano kunayapa makanisa changamoto ya kutafuta njia mpya za kutangaza Injili na kujenga na

---

[3] Angalia kwa mfano, Augustine, "Ennarrationes in Psalmos," 44, 24-25, in J. P. Migne, *Patrologia Latina* 36, 509-510.

[4] Mshikamano huu wa kusaidiana kwa dhati ni lazima kuutofautisha na hali ya kuchanganya dini na kufikiri kusiko sahihi kuwa jumuiya zingine za Kikristo ni maeneo ya misheni ya kuwageuza watu kutoka kwenye imani zao.

kuimarisha jumuiya za Kikristo. "Makanisa yanayoibuka," yanaleta pia namna mpya ya uwepo wa Kanisa, na yanatoa changamoto kwa makanisa mengine yatafute njia ya kutoa majibu ya mahitaji na matakwa ya Wakristo katika njia ambazo zinayafanya yawe na uaminifu wa mapokeo toka kuanzishwa kwa Kanisa. Kukua kwa utandawazi wenye utamaduni wa kupuuzia mambo ya dini na imani yanalipa changamoto Kanisa katika hali ambayo watu wengi wanahoji imani, huku wakiamini kwamba maisha ya mwanadamu yanajitosheleza yenyewe bila kumhusisha Mungu. Katika maeneo mengine Kanisa linakabiliwa na changamoto ya kupungua kwa idadi ya waumini, na inachukuliwa na wengi kuwa Kanisa halina maana tena kwao, na hata kupelekea wale ambao bado ni waumini kuongelea haja ya kuwa na uinjilisti mpya. Makanisa yote yanashirikiana katika wajibu wa kazi ya uinjilisti katika kukabili changamoto hizi na nyingine ambazo huibuka kwa kufuata mazingira fulani.

**C. Umuhimu wa Umoja**

8. Katika Agano Jipya umuhimu wa umoja wa Kikristo kwa ajili ya misheni na asili ya Kanisa ulikuwa tayari umejidhihirisha wazi. Katika Matendo ya Mitume 15 na Galatia 1-2, ni dhahiri kwamba misheni kwa mataifa (mengine) ilizaa minyukano na kutishia migawanyiko kati ya Wakristo. Kwa njia nyingine, harakati za kiekumene za sasa zinahuisha uzoefu wa Baraza la kwanza la Yesuralemu. Somo hili ni mwaliko kwa viongozi, watheologia, na waumini wa makanisa yote ili kutafuta umoja ambao Yesu Kristo aliuombea tuwe nao kabla ya kuyatoa maisha yake sadaka kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu (ling. Yohana 17:21).

9. Umoja wa makanisa unaoonekana unahitaji yatambuane na kuona ukweli wa uwepo kile Imani ya Nikea (381) inachoita, "Kanisa moja, takatifu, la kikatoliki, na la

kimitume." Kutambua huku kwa upande mwingine kutatokana na mabadiliko ya kiimani, matendo, na huduma katika jamii husika. Hali hii inatoa changamoto kubwa kwa makanisa katika safari yao ya kuelekea kwenye umoja.

10. Kwa sasa, baadhi ya Wakristo wanalitambulisha tu Kanisa la Kristo na jamii zao, wakati wengine wanaweza kuzitambua jamii zingine pia, lakini utambuzi huu tu haukamilishi vitu vinavyofanya umoja wa Kanisa. Wengine wameungana na kuweka makubaliano au maagano mbalimbali ya mahusiano, na mengi ya hayo huhusisha ushirikiano katika ibada.[5] Wengine wanaamini kwamba Kanisa la Kristo lipo katika jumuiya mbalimbali zenye imani ya kweli ya Kikristo, wakati wengine wanasisitiza kwamba Kanisa la Kristo ni lile lisiloonekana na haliwezi kutambuliwa vya kutosha wakati huu wa hija ya kidunia.

***Mambo ya msingi katika njia ya kuelekea umoja***

*Tokea Azimio la Toronto la 1950, BMD limeyapa makanisa changamoto ya "kutambua kuwa ushiriki katika kanisa la Kristo unaleta kujumuika zaidi kuliko ushiriki wa Wakristo katika madhehebu yao." Zaidi ya hayo maelewano kati ya makanisa na washiriki wake yamehimizwa na yameendelezwa na mikutano mbalimbali. Hata hivyo, tofauti katika masuala ya msingi zitabakia kuwa changamoto na yatahitaji utatuzi wa pamoja: "Tutalitambulishaje Kanisa linalojiita kwa njia ya Ukiri wa Imani, Kanisa moja, takatifu, la kikatoliki na la kimitume?"Nini mapenzi ya Mungu kwa ajili ya umoja wa Kanisa hili?"*

---

[5] Ling. Ripoti ya Kianglikana-Kilutheri "Growth in Communion," J. Gros, FSC, T.F. Best na L. F. Fuchs, SA (wahariri), *Growth in Agreement III: International Dialogue Texts and Agreed Statements*, 1998-2005, Geneva-Grand Rapids, WCC-Eerdmans, 2007, 375-425, ripoti inarejea makubaliano muhimu ya kikanda kati ya makanisa ya Kilutheri na Kianglikana.

*"Tunahitaji tufanye nini ili kutimiza mapenzi ya Mungu kwa vitendo?" Nakala ya andiko hili ni kwa ajili ya kuyasaidia makanisa yatafakari na kutoa majibu ya maswali haya.*[6]

[6] Hivyo nakala ya andiko hili inatarajia kujenga msingi wake katika tamko la Mkutano wa Porto Alegre wa Baraza la Makanisa Duniani linalosema "Tumeitwa Kuwa Kanisa Moja," na kichwa kidogo, "Mwaliko kwa Makanisa Kuamsha Dhamira ya Kutafuta Umoja na Kuwa na Mazungumzo ya Kina," ndani ya kitabu *Growth in Agreement*, III, 606-610. Angalia "Ripoti ya Mwisho ya Kamati Teule juu ya Ushiriki wa Orthodoksi katika BMD," sehemu ya III, 12-21, ndani ya andiko la *Ecumenical Review* 55.1, January 2003, 7-8.

## Sura ya II

## Kanisa la Utatu Mtakatifu

### A. Kutambua Mapenzi ya Mungu kwa Kanisa

11. Wakristo wote wanaamini kuwa Maandiko Matakatifu ndio msingi mkuu, hivyo ushuhuda wa kibiblia unatoa chanzo kisichoondosheka kwa ajili ya kufikia makubaliano makubwa yahusuyo Kanisa. Pamoja na Agano Jipya kutotoa ufahamu fasaha juu ya elimu ya Kanisa, inaweka wazi masimulizi juu ya imani ya jumuiya za Kanisa la Kwanza, ibada zao, majukumu yao katika huduma na uongozi wa Kanisa, na hata kuweka picha na mifano inayoelezea utambulisho wa Kanisa. Tafsiri zilizoendelea ndani ya Kanisa, zikitafuta kila wakati kubakia kwa uaminifu katika mafundisho ya kibiblia, zimezaa utajiri wa ziada wenye maono katika kanisa na historia yake. Roho Mtakatifu yule yule aliyeziongoza jumuiya za kwanza kuandika maandiko yenye msukumo wa kiroho anaendelea kuwaongoza wafuasi wa Yesu kizazi hadi kizazi wajitahidi kubaki waaminifu kwa ajili ya kazi ya Injili. Hiki ndicho kile kinachojulikana kuwa ni "Mapokeo ya Kanisa Yanayoishi."[1] Umuhimu mkubwa wa mapokeo umekubalika katika jumuiya zilizo nyingi. Hata hivyo jumuiya hizi

---

[1] Kama Kongamano la Dunia juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada linavyosema katika ripoti yake "Maandiko Matakatifu, Mapokeo na Mila," "Mapokeo ina maana ya Injili yenyewe, iliyoenezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine ndani na iliyofanywa na Kanisa lenyewe, Yesu mwenyewe akiwepo katika maisha ya Kanisa. Mapokeo maana yake pia ni mchakato wa kimapokeo. Neno mila linatumika kuonyesha aina tofauti za kuelezea na pia mila mbalimbali za kimadhehebu..." P. C. Roger and L. Vischer (wahariri.), *The Fourth World Conference on Faith and Order: Montreal 1963*, London, SCM Press, 1964, 50. Angalia pia *A Treasure in Earthen Vessels: An Instrument for an Ecumenical Reflection on Hermeneutics*, Geneva, WCC, 1998, §§ 14-37, pages 14-26.

zinatofautiana katika namna zinavyotathmini mamlaka hayo na jinsi yanavyohusiana na yale mamlaka ya Maandiko Matakatifu.

12. Ufahamu wa aina tofauti juu ya mafundisho ya Kanisa unapatikana katika vitabu mbalimbali vya agano Jipya na mapokeo yake ya baadaye. Agano Jipya, kwa kukubali uwingi huu wa ufahamu, inashuhudia kukubaliana kwake na umoja wa Kanisa, bila kusahau mipaka inayotokana na tofauti zilizo halali.[2] Tofauti zilizo halali si ajali katika maisha ya jumuiya ya Kikristo, bali zaidi ni kipengele chake cha umoja wa kikanisa, ubora unaoakisi ukweli kuwa ni usanifu wa Mungu kuwa wokovu katika Kristo ni lazima ufanyike "kuwa mwili" katika watu wa namna tofauti ambao wanahubiriwa wanatangaziwa Injili. Njia kamili ya kufikia fumbo la Kanisa Moja linahitaji kutumia na kushirikisha picha na ufahamu wa namna nyingi (watu wa Mungu, mwili wa Kristo, hekalu la Roho Mtakatifu, mzabibu, kundi, bibi arusi, kaya, askari, marafiki, n.k.). Sehemu hii ya kitabu inatafuta kufunua utajiri wa ushuhuda wa kibiblia pamoja na ufahamu wa kutoka mapokeo ya Kanisa.

## B. Kanisa kama *Ushirika* wa Utatu wa Mungu

### *Uwezo wa Mungu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu*

13. Kanisa linaitwa na Mungu ambaye "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." (Yohana 3:16) na aliyemtuma Roho Mtakatifu kuwaongoza waumini hawa katika kweli yote, na kuwakumbusha yale ambayo Yesu amewafundisha (ling. Yohana 14:26). Ndani ya Kanisa waumini wanaunganishwa na Yesu Kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu ambaye hushirikiana

[2] Mada hii intazungumziwa katika kipengele cha §§ 28-30 hapo chini.

kwa njia ya mahusiano yaliyo hai na Mungu Baba, anayezungumza nao na kutoa majibu ya uaminifu wa wito wao. Dhana ya kibiblia ya *jumuiya* imekuwa kitovu katika jitihada za kiekumene kuwa na ufahamu wa pamoja wa maisha na umoja wa Kanisa. Jitihada hizi zinatabiri kuwa ushirika hauna maana tu ya umoja wa makanisa ya madhehebu shiriki. Jina *jumuiya* (ushirika, ushiriki, faragha ya pamoja, kushirikishana),linatokana na maana ya kitenzi "kuwa na kitu cha pamoja kwa pamoja," "kushirikishana," "kushiriki," kuwa na sehemu ya," au "kutenda kwa pamoja," na maana hii inaonekana katika mkazo wa kushirikishana karama ulio kwenye dhana ya Chakula cha Bwana (ling. 1 Kor 10:16-17), upatanisho kati ya Paulo na Petro, Yakobo na Yohana (ling. Gal 2:7-10), mchango kwa ajili ya maskini (ling. Rom 15:26; 2 Kor 8:3-4), na uzoefu na ushuhuda wa Kanisa (ling. Mtd. 2:42-45). Kama umoja uliojengwa kwa uwezo wa ki-Mungu, Kanisa ni la Mungu na haliishi kwa kujitegemea lenyewe. Kwa hali halisi ya asili yake Kanisa ni la kimishenari, limeitwa na limetumwa kutoa ushuhuda kwa kwa njia ya maisha yake lenyewe kwa jumuiya ambayo Mungu ameikusudia kwa ajili ya wanadamu wote na kwa uumbaji wote katika ufalme wake.

14. Kanisa linalenga na kujenga msingi wake katika Injili, yaani kutangaza Neno aliyefanyika mwili, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Hii inaakisiwa na kuthibitishwa na Agano Jipya kuwa, "Kwa kuwa mmezaliwa upya mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele" (1 Pet. 1:23). Kwa njia ya kuihubiri Injili (ling.. Rum 10:14-18), na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu (ling. 1 Kor 12:3), wanadamu wanakuja kwenye imani iokoayo na kwa njia ya vipawa vya Sakramenti, wanajumuishwa ndani ya mwili wa Kristo (ling. Efe 1:23). Jumuiya zingine, wangeliita Kanisa ni mwili ulioumbwa na

Injili (*creatura evangelii*) kwa kufuata mafundisho haya.[3] Maana halisi ya maisha ya Kanisa ni kuwa katika jumuiya inayosikikiliza na kutangaza Neno la Mungu. Kanisa linavuta uhai wake kutoka kwenye Injili na kugundua mwelekeo mpya kila wakati katika safari yake.

15. Jibu la Maria, Mama wa Mungu (*Theotokos*), katika siku aliyopewa ujumbe na malaika juu ya kuwa na mimba kwa uwezo wa Mungu, "Mariamu akasema, Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema. Kisha malaika akaondoka akaenda zake" (Luka 1:38), limeonekana kuwa picha na mfano kwa Kanisa na Mkristo mmoja mmoja. Andiko kuhusu Imani na Utaratibu wa Ibada katika *Kanisa na Dunia* (1990) lilibainisha kuwa Maria ni "mfano muhimu kwa wale wote wanaotafuta vipimo kamili vya maisha katika umoja wa Kikristo" kwa jinsi anavyopokea na kuitikia ujumbe wa Neno la Mungu (Luka 1:26-38); anamshirikisha Elizabeti furaha yake ya habari njema aliyoipokea (Luka 1:46-55); anapatanisha, anateseka na kujitahidi kuelewa matukio juu ya kuzaliwa kwa Yesu na utoto au ukuaji wake (Mt 2:13-23; Luka 2:19, 41-51); anatafuta kufahamu athari kamili ya ufuasi (Mk

---

[3] Angalia "The Church as 'Creature of the Gospel'," katika Mazungumzo ya Walutheri na Wakatoliki, "Church and Justification," katika kitabu cha J. Gros, FSC, H. Meyer and W. G. Rusch, (wahariri.), *Growth in Agreement II: Reports and Agreed Statements of Ecumenical Conversations on a World Level, 1982-1998*, Geneva-Grand Rapids, WCC-Eerdmans, 2000, 495-498, inayorejea matumizi ya maelezo haya ya Martin Luther katika *WA 2, 430, 6-7: "ecclesia enim creatura est evangelii*." mazungumzo mengine baina ya makanisa yametumia neno la Kilatini *creatura verbi* kuelezea wazo lile lile: angalia kipengele "Two Conceptions of the Church" (§§ 94-113), kinaeleza Kanisa kuwa ni "*creatura verbi*" na "sakramenti ya neema" katika Mazungumzo ya Kanisa la Matengenezo na Kanisa Katoliki, "Towards a Common Understanding of the Church," katika kitabu cha *Growth in Agrement II*, 801-805. Angalia pia tamko "Called to Be the One Chruch," angalia rejea 1, hapo juu.

3:31-35; Lk 18:19-20); anasimama karibu naye chini ya msalaba na kuusindikiza mwili wake kaburini (Mt 27:55-61; Yohana 19:25-27) na akiwa na wafuasi wengine anasubiri kupokea Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste (Mtd. 1:12-14; 2:1-4).[4]

16. Yesu alimuomba Baba atume Roho Mtakatifu kwa wanafunzi wake ili awaongoze katika kweli yote (Yohana 15:26, 16:13), na ni huyu Roho Mtakatifu ndiye humpa kila muumini imani na karama nyingine na pia kulipa Kanisa karama zinazohitajika, ubora, na utaratibu. Roho Mtakatifu huulisha na kuuchangamsha mwili wa Kristo kwa njia ya sauti ya uzima itokanayo na Injili, kwa njia ya vipawa vya Sakramenti, na hasa Ekaristi Takatifu, na kwa njia ya huduma mbalimbali za kijamii.

### ***Unabii, Utume na Ufuasi wa Watu wa Mungu***

17. Kwa njia ya wito ulioelekezwa kwa Ibrahimu, Mungu tayari alikuwa anachagua watu watakatifu. Manabii mara kwa mara waliurudia uchaguzi na wito huu kwa njia ya maneno yenye nguvu kama ifuatavyo: "Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema Bwana; Nitatia sheria yangu ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu." (Yer. 31:33; Ezek 37:27; imeakisiwa pia 2 Kor 6:16; Ebr 8:10). Agano la Mungu na Israeli liliweka nafasi yenye uamuzi wa kipekee katika kuchipuka kwa utimilifu wa mpango wa wokovu. Wakristo wanaamini kuwa katika huduma, kifo na

---

[4] Angali ripoti ya Imani na Utaratibu wa Kanisa ndani ya *Church and World: The Unity of the Church and the Renewal of Humani Community*, Geneva, WCC, 1990, 64. Angalia pia ripoti ya Kamisheni ya Kimataifa Waangalikana na Wakatoliki, "Mary: Grace and Hope in Christ," *Growth in Agreement III*, 82-112; na ripoti ya Groupe des Dombes, *Mary in the Plan of God and in the Communion of Saints* (1997-1998), Mahwah, N.J., Paulist Press, 2002.

kufufuka kwa Yesu na kwa njia ya kumtuma Roho Mtakatifu, Mungu ameweka agano jipya kwa ajili ya kusudi la kuwaunganisha wanadamu wote na yeye na kati yao wenyewe. Kuna ukweli usiopingika wa upya wa agano lililoanzishwa na Kristo na hata hivyo Kanisa linabaki kuwa matokeo ya usanifu wa Mungu, likihusiana kimsingi na watu wa agano la kwanza, ambao Mungu atabaki mwaminifu kwao (ling. Rum 11:11-36).

18. Katika Agano la Kale, wana wa Israeli wanasafiri kuelekea kwenye utimilifu wa ahadi ambayo inabaini kuwa katika Ibrahimu mataifa yote ya nchi yatabarikiwa. Wote wanaomgeukia Kristo wanaona jinsi ahadi hii ilivyotimizwa, pale msalabani, Kristo alipovunja ukuta kati ya Wayahudi na Mataifa (ling. Efe 2:14). Kanisa "ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingia katika nuru yake ya ajabu; ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema" (1 Petro 2:9-10). Wakati tukitambua upekee wa ukuhani wa Yesu Kristo, ambaye sadaka yake imeanzisha agano jipya (ling. Ebr 9:15), waumini wameitwa kwa njia ya maisha yao kuueleza ukweli kwamba wameitwa kuwa "ukuhani wa kifalme," wakijitolea kama Paulo asemavyo, "Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana." (Rum 12:1). Kila Mkristo anapokea vipawa vya Roho Mtakatifu kwa ajili ya kulijenga na kuliinua Kanisa na kwa ajili ya kuwa sehemu ya misheni ya Kristo. Vipawa hivi hutolewa kwa ajili ya faida ya wote (ling. 1 Kor 12:7; Efe 4:11-13) na vinatupa majukumu na wajibu na uwajibikaji unaohimiza kuheshimu kila mtu na kila jumuiya na kuwa na uwajibikaji kwa Kanisa lote katika kila hatua ya maisha yake. Wakiwa wanatiwa nguvu na Roho Mtakatifu,

Wakristo wameitwa kuuishi ufuasi wao kwa njia ya namna mbalimbali wakiwa katika huduma.

19. Watu wote wameitwa kuwa manabii, wakibeba ushuhuda wa Neno la Mungu; watu wa kikuhani, wakitoa sadaka ya maisha waishiyo ya ufuasi; na watu wa ufalme, wakitumika kama vyombo katika kuujenga ufalme wa Mungu. Watu wote wa Kanisa wanashiriki wito huu. Katika kuita na kuwatuma wale Thenashara, Yesu aliweka misingi ya uongozi wa jumuiya za wafuasi wake katika huduma yake iliyoendelea ya kutangaza ufalme wake. Wakiwa waaminifu kwa mfano wa [Yesu], toka mwanzo, baadhi ya waumini walichaguliwa kwa uongozi wa Roho Mtakatifu na wakapewa mamlaka na wajibu maalumu. Watumishi waliowekwa wakfu "wanakutana na kuujenga mwili wa Kristo kwa njia ya kutangaza na kufundisha Neno la Mungu, kusherehekea Sakramenti Takatifu, na kwa kuongoza maisha ya jumuiya katika ibada, misheni na huduma za Kanisa."[5] Washiriki wote wa mwili, waliobarikiwa na wasiobarikiwa, ni washirika wanaohusiana kama watu wa Mungu ambao wote ni makuhani. Watumishi waliobarikiwa wanaikumbusha jamii juu ya utegemezi wa jamii kwa Yesu Kristo, ambaye ndiye chimbuko la umoja na misheni yake, hata kama wanaelewa kuwa huduma yao yote humtegemea yeye. Wakati huo huo wanaweza kutimiza wito wao kwa ajili na ndani ya Kanisa tu; wanahitaji kutambuliwa na Kanisa, kuungwa mkono na kutiwa moyo.

20. Kuna uvumi mpana wa mapatano dhidi ya makanisa yenye mapokeo tofauti kuhusu umuhimu wa nafasi ya huduma. Hili limeelezwa kwa ufasaha katika andiko juu ya Imani na Utaratibu wa Kanisa katika kitabu cha *Ubatizo,*

---

[5] *Baptism, Eucharist and Ministry,* Geneva, WCC, 1982, kipengele kuhusu Huduma, §13

*Ekaristi na Huduma* (1982), ambacho kinatamka kuwa "Kanisa halijawahi kuwa bila watu walioshikilia mamlaka au wajibu maalumu," likibainisha kuwa "Yesu aliwachagua na kuwatuma wanafunzi kuwa mashahidi wa ufalme [wake]."[6] Misheni ambayo Yesu aliwakabidhi wale kumi na moja katika Injili ya Mathayo 28 inajumuisha "huduma ya Neno, Sakramenti Takatifu, na uangalizi waliopewa na Kristo kwa ajili ya Kanisa ili kubebwa na baadhi ya washiriki kwa ajili ya faida ya wote. Kazi ya utatu huu wa huduma unaliimarisha Kanisa kwa ajili ya misheni yake katika dunia."[7] Matamko ya makubaliano yanaweka wazi kuwa ukuhani wa kifalme wa watu wote wa Mungu (ling. 1 Peter 2:9) na ubarikio kwa ajili ya huduma maalumu yote ni mambo muhimu katika kanisa, na si mambo yanayotakiwa kuonekana kuchochea ubaguzi. Wakati huo huo makanisa yanatofautiana katika kuweka utaratibu wa nani awe na uwezo wa kufanya maamuzi ya mwisho kwa ajili ya jumuiya; baadhi ya makanisa ni kwa wale waliobarikiwa tu, na kwa

---

[6] Mwendelezo, sehemu kuhusu Huduma, § 9

[7] Mazungumzo kati ya Kanisa la Reformed na Kikatoliki, "Towards a Common Understanding of the Church," § 132, katika *Growth and Agreement II*, 810. Angalia pia ripoti ya Walutheri na Wakatoliki "Ministry in the Church," §17, katika kitabu cha H. Meyer and L. Vischer (wahariri.), *Growth in Agreement: Reports and Agreed Statements of Ecumenical Conversations on a World Level*, Ramsey-Geneva, Paulist-WCC, 1984, 252-253: "Agano Jipya linaonyesha jinsi ambavyo huduma maalumu ilitokana na huduma zingine ambazo zieleweka kuwa zinatokana na mfuatano wa huduma za mitume waliotumwa na Yesu. Huduma hii ya kipekee ilionekana wazi kuwa ni ya muhimu kwa ajili ya uongozi katika hizo jumuiya. Hivyo mtu anaweza kusema kuwa kwa kufuata maandiko ya Agano Jipya 'huduma maalumu' iliyoanzishwa na Yesu Kristo kwa njia ya kuwaita na kuwatuma wanafunzi 'ilikuwa muhimu kwa wakati huo - na ni muhimu kwa wakati wote na matukio yote.'" Wamethodisti na Wakatoliki kwenye "Toward a Statement on the Church," wanakubali kwamba "kanisa limehitaji wakati wote huduma inayopewa kibali na Mungu mwenyewe," ling. *Growth in Agreement II*, 588, §29.

makanisa mengine wakristo wa kawaida wanakuwa na wajibu katika maamuzi kama hayo.

### *Mwili wa Kristo na Hekalu la Roho Mtakatifu*

21. Kristo ndiye kiungo na kichwa mwili wake yaani Kanisa, akiliongoza, kulitakasa na kuliponya (ling. Efe 5:26). Wakati huo huo, yeye mwenyewe ameungana nalo kwa kulikumbatia, akilipa uhai wake wote kwa njia ya Roho Mtakatifu (Rum 12:5; ling. 1 Kor 12:12). Imani katika Kristo ni msingi wa ushiriki wa mwili [wa Kristo] (Rum 10:9). Kutokana na ufahamu wa mapokeo yaliyo mengi, pia ni kwa njia ya matambiko au sakramenti ili wanadamu wawe washirika wa Kristo na kwa njia ya Chakula cha Bwana ushiriki wao kati mwili wake (1 Kor 10:16) ufanywe upya kila mara. Roho Mtakatifu hutoa vipawa vingi kwa washiriki na huleta umoja katika kuujenga mwili [wake] (ling. Rum 12:4-8; 1 Kor 12:4-30). Anaamsha upya mioyo yao, anawaimarisha na kuwaita kutenda mema,[8] hivyo kuwawezesha kumtumikia Mungu katika kuuendeleza ufalme wa Mungu duniani. Hivyo picha ya "mwili wa Kristo," hata kama kiukweli na kimsingi linarejea Kanisa kwa Kristo, pia linamaanisha kwa kina uhusiano na Roho Mtakatifu, kama inavyoshuhudiwa katika Agano Jipya lote. Mfano wa wazi ni ule wa kushuka kwa ndimi za moto juu ya wanafunzi waliokuwa wamekusanyika katika chumba cha juu siku ya asubuhi ya Pentekoste (ling. Mtd 2:1-4). Kwa nguvu ya Roho Mtakatifu waumini wanakua ndani ya "hekalu takatifu la Bwana" (Efe 2:21-22), ndani ya "nyumba ya kiroho" (1 Petro 2:50. Wakiwa wamejazwa Roho Mtakatifu, wameitwa kuyaongoza maisha yakionyesha utajili wa wito wao katika ibada, ushuhuda na huduma, wakiwa na hamu ya kuendelea

---

[8] Ling. Tamko la Pamoja kati ya Walutheri na Wakatoliki *Joint Declaration on the Doctrine of Justification*, Grand Rapids, Eerdmans, 2000,§15

kuuimarisha umoja wa Roho Mtakatifu kwa dhamana ya amani (ling. Efe 4:1-3). Roho Mtakatifu analiumua na kuliimarisha Kanisa kushika nafasi yake katika kutangaza na kuleta mabadiliko ambayo yanaliliwa na uumbaji wote (ling. Rum 8:22-23).

### *Kanisa Moja, Takatifu, la Kikatoliki na la Kimitume*

22. Tangu wakati wa baraza la pili la kiekumene, lililokaa Konstantinopoli mwana 381, Wakristo wengi wameweka kwenye liturgia zao ukiri unaeleza kuwa Kanisa ni moja, takatifu, la kikatoliki na la kimitume. Sifa hizi ambazo hazitengani lakini zinaelezana na kutegemeana kwa karibu, ni vipawa vya Mungu kwa ajili ya Kanisa ambalo waumini wake, licha ya utukutu wao wa kibinadamu wanaitwa kila wakati kuukiri utukufu huu na kuendelea kuuwezesha ufanye kazi.

- Kanisa ni moja kwa sababu Mungu ni Mmoja (ling. Yohana 17:11; 1 Tim 2:5). Kwa sababu hiyo imani ya kimitume ni moja; maisha mapya katika Kristo ya pamoja; na tumaini la Kanisa ni moja.[9] Yesu aliomba kuwa wanafunzi wake wote wawe na umoja ili ulimwengu wote upate kusadiki (ling. Yohana 17:20-21), na akatuma Roho Mtakatifu ili kuwaweka wawe na umoja (ling. 1 Kor 12:12-13). Migawanyiko ya sasa ndani na kati ya makanisa ni kinyume kabisa na hali hii ya umoja; "hali hii inatakiwa itatuliwe kwa njia ya vipawa vya kiroho vya imani, matumaini, na upendo ili utengano na ubaguzi visiwe na nafasi tena."[10] Hata pamoja na migawanyiko hii, makanisa yote yanajielewa kuwa yamejengwa katika msingi wa Injili

[9] Ling. "Called to Be the One Church," §5, katika *Growth in Agreement III*, 607.
[10] Mwendelezo.

(ling. Gal 1:5-9), na yameunganishwa kwa njia ya alama nyingi za maisha yake (ling. Efe 4:4-7).

- Kanisa ni takatifu kwa sababu Mungu ni mtakatifu (ling. Isa 6:3; Law 11:44-45). Yesu "alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake; ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa" (Efe 5:25b-27). Umhimu wa utakatifu wa Kanisa umeshudiwa katika vizazi na watakatifu, na kwa njia ya maneno na vitendo vitakatifu Kanisa limetangaza na kutenda kwa jina la Mungu, lililo Takatifu. Hata hivyo dhambi inayoenda kinyume na huu utakatifu na kwenda kinyume na asili ya kweli na wito wa Kanisa, wakati wote imevuruga maisha ya waumini. Kwa sababu hii sehemu ya utakatifu wa Kanisa ni huduma yake ya kuendelea kuwaita watu kutubu, kuwaamsha na kuwabadilisha.
- Kanisa ni la Kikatoliki kwa sababu ya uwingi wa wema wa Mungu "ambaye hutaka watu wote waokolewe, na kupata kujua yaliyo kweli" (1Tim 2:4). Kwa njia ya nguvu iletayo uzima toka kwa Mungu, Misheni ya Mungu inapita katika vikwazo vyote na kuihubiri Injili kwa watu wote. Palipo na fumbo la uwepo wa Kristo, hapo kuna Kanisa la kiulimwengu wote [kikatoliki] (ling. Ignatius wa Antiokia, Barua kwa Smurna, 6), kama ilivyo katika kusherehe za Ekaristi Takatifu. Umuhimu wa umoja huu wa Kanisa unadhoofishwa na tofauti za kitamaduni na tofauti zingine ambazo zinaruhusu kukua kwa migawanyiko. Wakristo wameitwa kutoa vikwazo vyote ili kuuvaa ukweli huu ulio kamili na uzima ulioletwa juu ya Kanisa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.
- Kanisa ni la Ulimwengu wote (kikatoliki) kwa sababu Baba alimtuma Mwana kulianzisha. Mwana, kwa kuitikia hilo, aliwachagua na kuwatuma mitume na manabii, akawapa vipawa vya Roho Mtakatifu wakati wa Pentekoste,

watumike kwa misingi ya vipawa hivyo na kuiangalia misheni [ya Mungu] (ling. Efe 2:20; Ufu 21:14; na Barua ya Klementi wa Rumi, *Barua kwa Wakorinto* 24). Wakristo wanaitwa kuwa waaminifu kila wakati kwa misingi hii ya kitume; kukosa uaminifu katika mambo ya ibada, ushuhuda au huduma inakuwa ni kinyume kabisa na utume wa Kanisa. Utume wa mfuatano katika huduma, kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, unakusudia kuhudumu utume wa Kanisa.[11]

23. Kwa kuangaziwa na sura zilizopita (13-22), ni wazi kwamba Kanisa si tu ni jumla ya waumini wenyewe. Kimsingi Kanisa ni ushirika wa Utatu wa Mungu na wakati huo huo ni ushirika ambao washiriki wake wanashirikiana katika maisha na misheni ya Mungu (ling. Petro 1:4), ambayo ni Utatu Mtakatifu, na ndio chimbuko na mwelekeo wa ushirika mzima. Hivyo Kanisa ni ukweli uliosheheni Uungu na ubinadamu.

24. Pamoja na Kanisa kuwa na uthibitisho kuwa Uungu na ubinadamu vinakutana ndani yake, hata hivyo makanisa yana hisia na hata misimamo tofauti juu ya jinsi matendo ya Roho Mtakatifu yanavyohusiana na mifumo ya kikanisa na kiibada. Wengine wanaona mifumo fulani ya kiibada kuwa imependwa na kusimikwa na Kristo mwenyewe kwa ajili ya wakati wote, kwa hiyo, kwa kuwa waaminifu kwa Injili, Wakristo kimsingi hawana mamlaka ya kubadili mifumo hiyo iliyowekwa wakfu na Mungu mwenyewe. Wengine wanathibitisha kwamba utaratibu wa Kanisa kwa kufuata wito wa Mungu una sura zaidi ya moja wakati wengine

[11] Tamko la Baraza la Makanisa Duniani lisemalo "Called to Be the One Church," , linatoa maelezo yanayofanana na Ukiri wa Imani kuwa Kanisa "ni moja, takatifu, la kiulimwengu na kimitume." Ling. *Growth in Agreement III*, 607.

wanathibitisha kuwa hakuna utaratibu wa kitaasisi unaoweza kipekee ukabeba tabia ya kutimiza mapenzi ya Mungu. Wengine wanashikilia kuwa kujenga uaminifu katika injili kunaweza kusababisha kuvunjika kwa mwendelezo wa kitaasisi uliopo, wakati wengine wanasisitiza kuwa imani inayojengwa kwa msingi wa injili inaweza ikasaidia kutatua matatizo ya kimfumo bila kuleta utengano.

### *Jinsi muendelezo wa mapokeo na mabadiliko yanavyohusiana na mapenzi ya Mungu*

*Kwa njia ya kuvumiliana, na katika hali ya kuheshimiana na kujaliana, makanisa mengi yamekuwa na uelewa wa ndani wa hisia na imani zinazotofautiana kuhusu mwendelezo na mabadiliko katika Kanisa, hivyo inakuwa ni wazi kuwa katika kusudio lile lile - kutii mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kuliagiza Kanisa - inawezekana kwa wengine kuamsha dhamira ya mwendelezo na kwa wengine dhamira ya mabadiliko. Tunayaalika makanisa yote kutambua na kuheshimu dhamira ya kila moja katika kutafuta mapenzi ya Mungu kwa ajili ya kutunza utaratibu wa Kanisa. Pia tunayaalika kutafakari kwa pamoja kuhusu vigezo vinavyotumika katika makanisa mbalimbali kwa ajili ya kupima mambo yahusuyo mwendelezo wa mapokeo na mabadiliko. Ni kwa kiwango gani vigezo hivyo vinaruhusu maendeleo katika nuru ya wito wa Kristo wa kuleta upatanisho wa haraka (ling. Mtt. 5:23-24)? Je sasa si wakati wa kuwa na njia mpya [ya kufikia upatanisho]?*

## C. Kanisa kama Ishara na Mhudumu wa Mpango wa Mungu kwa ajili ya Dunia

25. Mpango wa Mungu ni kuwakusanya wanadamu na uumbaji wote katika ushirika chini ya Ukuu wa Kristo (Ling. Waef. 1:10). Kanisa kama tafsiri ya ushirika wa Utatu Mtakatifu, inatimiza lengo hili na limeitwa kuonyesha huruma

ya Mungu kwa wanadamu, likiwasaidia kutimiza kusudi la kuumbwa kwao na kusudi ambalo kwalo hatimaye wanapata furaha: ya kusifu na kumtukuza Mungu pamoja na wenyeji wa mbinguni. Misheni hii ya Kanisa inakamilishwa na washiriki wake kwa njia ya ushuhuda wa maisha yao na ikiwezekana kwa njia ya kutangaza habari njema za Yesu Kristo. Misheni ya Kanisa ni kutekeleza kusudi hili. Kwa kuwa Mungu anapenda watu wote waokolewe na kuijua kweli (ling. 1 Tim 2:4), Wakristo wanatambua kuwa Mungu huwafikia wale wote ambao si washiriki hasa wa Kanisa kwa njia ambazo si rahisi kuonekana kwa macho ya kibinadamu. Pamoja na kutambua na kuheshimu viashiria vya kweli na wema unaoweza kutokana na dini zingine na kwa watu wasio na dini, Misheni ya Kanisa inabaki kuwa yenye kuwaalika watu hao, kwa njia ya shuhuda na ushahidi, ili watu wote waume kwa wanawake waje na wamjue na kumpenda Yesu Kristo.

26. Baadhi ya vifungu vya Agano Jipya vinatumia neno *fumbo* kuelezea mpango wa Mungu wa wokovu katika Kristo (ling. Waef 1:9; 3:4-6) na uhusiano wa karibu kati ya Yesu na Kanisa (ling. Efe. 5:32; Kol 1:24-28). Hii inamaanisha kuwa Kanisa linafurahia maisha yake ya kiroho, ambayo yanavuka viwango vya ubora wake ambao hauwezi kueleweka kirahisi kwa kuangalia mambo yake yanayoonekana tu. Vipimo vya Kanisa vya kidunia na kiroho haviwezi kutenganishwa. Miundo ya kimfumo ya jumuiya za Kikristo inahitaji kuangaliwa na kupimwa kwa mazuri au mabaya yake kwa njia ya tuzo ya nuru ya Mungu ya wokovu ulio katika Kristo, unaoshangiliwa kwa njia ya liturgia. Kanisa likibeba fumbo la wokovu na sura angavu ya binadamu katika maisha yake yenyewe, linashiriki katika misheni ya Kristo ya kupatanisha vitu vyote na Mungu na kuwapatanisha wanadamu wenyewe kwa wenyewe kwa njia ya Kristo (ling. 2 Kor 5:18-21; Rum 8:18-25).

27. Wakati kukiwa na makubaliano mapana kuwa Mungu alilianzisha Kanisa kama njia ya upendeleo wa kuleta mpango wake wa wokovu kwa uumbaji wote, jumuiya zingine zinaelezea vizuri hali hii kwa njia kuzungumzia "Sakramenti ya Kanisa," na wengine mara nyingi hawatumii lugha hii au wanaikataa kabisa. Wale wanaotumia maelezo ya "Sakramenti ya Kanisa" wanafanya hivyo kwa sababu wanalielewa Kanisa kama alama yenye kufaa na chombo cha ushirika wa wanadamu wao kwa wao kwa njia ya ushiriki wao katika Utatu wa Mungu.[12] Wale wasiopenda kutumia maelezo haya wanaamini kuwa matumizi yake yanapotosha tofauti kati ya Kanisa katika upana wake na sakramenti mbalimbali na linaweza likapelekea mtu kutoona hali ya dhambi ambayo bado ipo miongozi wa washiriki wake. Wote wanakubali kuwa Mungu ndiye mwasisi wa wokovu; na tofauti huonekana tu kwenye njia ambazo jumuiya mbalimbali zinaelewa asili na wajibu wa Kanisa na ibada zake za wokovu.

---

[12] Kwa mfano, Maaskofu wa Kanisa Katoliki la Kirumi katika Baraza la Pili la Vatikani walitoa tamko kuwa "Kanisa, katika Kristo, lipo katika asili ya Sakramenti - alama au *chombo* - ikimaanisha, ushirika na Mungu na umoja na watu wote" (ling. the Dogmatic Constitution on the Church, *Lumen Gentium*, n. 1), ambapo neno *chombo* linakusudia kuleta "ufanisi" kwa Kanisa katika hali chanya. Wakristo wengine wanaokubaliana kabisa juu ya asili ya kisakramenti ya Kanisa wanaona si sawa kutumia neno *chombo* kumaanisha jumuiya ya Kikristo. Mapokeo hasa yaliyoenea ya wazo kuwa Kanisa ni alama yanashuhudiwa na Baraza la Makanisa Ulimwenguni katika ripoti yake "The Holy Spirit and the Catholicity of the Church" kutoka katika Mkutano wake Mkuu wa Nne, uliofanyika Uppsala 1968, unaoeleza: "Kanisa linajitangaza lenyewe kwa nguvu kama alama ya kuja kwa umoja wa mwanadamu." Ling. N. Goodall (mhariri.), *The Uppsala Report*, Geneva, WCC, 1968, 18. Kwa ajili ya Katiba ya Kiimani, *Lumen Gentium* angalia, http://www.vatican.va.

### *Usemi kuhusu "Kanisa kama Sakramenti"*

*Wale wanaotumia usemi huu wa "Kanisa kama Sakramenti" hawakatai upekee wa "matendo ya Sakramenti" yatokanayo na sakramenti mbalimbali, wala hawakatai uhafifu wa huduma za kibinadamu. Wanaokataa usemi huu, kwa upande mwingine, hawakatai kwamba Kanisa ni alama yenye ufanisi wa uwepo wa Mungu na matendo yake. Kwa hiyo, hii haiwezi kufikiriwa kuwa swali linalo halalisha tofauti za kimtazamo zinazopatana na zinazokubaliwa na wote?*

## D. Kanisa kama Ishara na Mhudumu wa Mpango wa Mungu kwa ajili ya Dunia

28. Uhalali wa tofauti hizi katika maisha ya ushirika ni tuzo kutoka kwa Bwana. Roho Mtakatifu anatoa karama mbalimbali zinazosaidiana kwa waaminio kwa ajili ya malengo mazuri ya pamoja (ling. 1 Kor 12:4-7). Wafuasi wanaitwa kuwa na umoja kamili (ling. Matendo 2:44-47; 4:32-37), huku wakiheshimu na kuimarishwa na tofauti zao (1 Kor 12:14-26). Sababu za kiutamaduni na kihistoria zinachangia utajiri wa tofauti hizi ndani ya Kanisa. Injili inatakiwa kuhubiriwa kwa lugha, alama na picha zinazohusika katika nyakati na mazingira yake ili iweze kuwa na uhai halisi katika muda na sehemu husika. Uhalali wa tofauti hizi utaathirika endapo Wakristo watafikiri kuwa maelezo ya Injili yanayotokana na tamaduni zao ndio pekee yaliyo sahihi, na yanayotakiwa kulazimishwa kufuatwa na Wakristo wa tamaduni zingine.

29. Wakati huo huo umoja ni lazima udumishwe. Kwa kushiriki pamoja imani katika Kristo, inayosemwa kwa njia ya kutangaza Neno, kushiriki sakramenti mbalimbali, na imani inayoonekana katika huduma na ushuhuda, katika kila kanisa kwenye eneo lake ina ushirika na makanisa jirani mahali popote na wakati wowote. Huduma ya kichungaji kwa ajili ya

umoja na kudumisha tofauti zilizopo, ni nyenzo mojawapo iliyotolewa kwa Kanisa katika kuwasaidia wale wenye karama na mitizamo mbalimbali kubaki pamoja wakiwajibika kwa kila mmoja.

30. Masuala yahusuyo umoja na tofauti zilizopo kimsingi zimeleta wasiwasi toka Kanisa lilipojipambanua kuwa moja, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, kuwa mataifa wanakaribishwa katika ushirika (ling. Matendo 15:1-29; 10:1-11:18). Barua iliyowafikia Wakristo wa Antiokia kutoka kwenye mkutano wa Yerusalemu ilibeba kile kinachoweza kuitwa kanuni za msingi zinazoongoza umoja na tofauti hizo: "Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi, tusiwatwike mzigo ila hayo yaliyo lazima " (Matendo 15:28). Baadaye Mabaraza ya Kiekumene yalitoa mifano zaidi juu ya haya "mambo muhimu," kama vile wakati ule wa Baraza la Kwanza la Kiekumene la Nikea, 325, maaskofu walifundisha kinagaubaga kuwa ushirika katika imani unahitaji uthibitisho wa Uungu wa Kristo. Katika nyakati za karibuni, makanisa yameungana pamoja katika kutamka kwa ujasiri mafundisho ya Kanisa yanayoeleza matokeo ya mafundisho ya msingi kama hayo, kama vile, katika kulaani vitendo vya kibaguzi katika jamuia nyingi za Kikristo.[13] Kuna ukomo katika kuhalalisha tofauti; hasa tofauti zinapovuka mipaka inayokubalika zinaweza kuleta uharibifu wa

---

[13] "World Council of Churches' Consultation with Member-Churches in South africa - Cottesloe, Johannesburg, 7-14 December, 1960," katika *The Ecumenical Review*, XIII(2), January 1961, 244-250; "Statement on Confessional Integrity," katika *In Christ a New Community: The Proceedings of the Sixth Assembly of the Lutheran World Federation: Dar-es-Salaam, Tanzania, June 13-25, 1977*, Geneva, Lutheran World Federation, 1977. 179-180, 210-212; "Resolution on Racism and South Africa," katika *Ottawa 82: Proceedings of the 21st General Council of the World Alliance of Reformed Churches (Presbyterian and Congregational" Held at Ottawa, Canada, August 17-27, 1982*, Geneva, Offices of the Alliance, 1983, 176-180; Ungamo la Belhar, http://www.urcsa.org.za/documents/The%20Belhar%20Confession.pdf.

tuzo ya umoja. Ndani ya Kanisa, uzushi na migawanyiko, pamoja na migogoro ya kisiasa na lugha za kuchochea uadui, vimetishia kutoweka kwa tuzo ya Mungu ya ushirika. Wakristo hawaitwi tu kuweka juhudi bila kukoma ili kuondoa toafauti na uzushi, lakini pia wanaitwa kutunza na kuthamini tofauti zao halali za kiliturgia, mila na sheria na kuendeleza tofauti halali za maisha ya kiroho, njia za kitheologia na ujengaji wa hoja kwa njia ambayo inachangia kuleta umoja na ushirikishwaji wa watu wote wa Kanisa zima.[14]

---

[14] Ling. Tamko la Baraza la Makanisa Duniani "The Unity of the Church as *Koinonia:* Gift and Calling": "Tofauti ambazo zina mizizi yake katika mapokeo ya kitheologia, tamaduni mbalimbali, makutano ya kikabila au kihistoria ni sehemu ya asili ya ushirika; hata hivyo kuna ukomo katika kutofautiana. Tofauti si halali, pale, kwa mfano, zinapofanya kusitokee ukiri wa pamoja wa Yesu Kristo kama Mungu na Mwokozi ambaye ni yule yule jana, leo na hata milele (Ebr 13:8) ... Katika ushirika tofauti huletwa pamoja katika uwiano kama karama za Roho Mtakatifu, zikichangia hali ya utajiri na ukamilifu wa kanisa la Mungu," katika kitabu cha M. Kinnamon (mhariri.), *Signs of the Spirit: Official Report Seventh Assembly*, Geneva-Grand Rapids, WCC-Eerdmans, 1991, 173. Tofauti halali zinashughulikiwa kila mara katika mazungumzo ya kimataifa kati ya makanisa na makanisa. Mazungumzo ya Waangalikana na Waorthodoksi, kwa mfano, yanatambua tofauti kubwa katika maisha ya makanisa ya kimaeneo: "Kama ushuhuda wao kuhusu imani moja haufifii, tofauti hizo hazionekani kama upungufu au sababu ya mgawanyiko, bali kama alama ya utimilifu wa Roho mmoja ambaye anagawa karama zake kwa kila mmoja kulingana na mapenzi yake," *The church of the Triune God: The Cyprus Statement Agreed by the International Commission for Anglican-Orthodox Dialogue 2006*, London, Anglican Communion Office, 2006, 91. Angalia pia: Mazungumzo katika ya Walutheri na Wakatoliki, *Facing Unity*, 1984, §§5-7, 27-30, na hasa 31-34, katika *Growth in Agreement II* 445-446, 449-450; Kamisheni ya Waangalikana na Wakatoliki, *The Gift of Authority*, §§26-31, katika *Growth in Agreement III*, 68-69; Mazungumzo ya Wamethodisti na Wakatoliki, *Speaking the Truth in Love,* §50, katika *Growth in Agreement III*, 154.

*Mazungumzo ya kiekumene katika kutafuta umoja ambao Yesu aliuombea yamekuwa katika sehemu nyingi, na ni juhudi za wawakilishi kutoka makanisa mbalimbali ya Kikristo kupambanua, kwa msaada wa Roho Mtakatifu, mambo ya msingi kwa ajili ya umoja, kwa kufuata mapenzi ya Mungu, na mambo yanayoeleweka vema kama tofauti halali. Ingawa makanisa yote yana taratibu zake kwa ajili ya kutofautisha tofauti zilizo halali na zisizo halali, ni wazi kwamba mambo mawili yanapungua (a) vigezo au njia za pamoja za kupambanua, na (b) mifumo inayotambulika kwa wote kwa kuwa inatakiwa kutumia vigezo na njia hizi kwa ufanisi. Makanisa yote yanatafuta kufuata mapenzi ya Bwana lakini bado yanaendelea kutokubaliana katika baadhi ya vipengele vya imani na utaratibu wa ibada, na zaidi sana kutokukubaliana huko ama kunaleta mgawanyiko wa Kanisa au badala yake huwa ni sehemu ya tofauti halali. Tunayaalika makanisa kutafakari: Ni hatua gani chanya zinaweza kuchukuliwa kufanya upambanuzi wa pamoja [juu ya Kanisa] uwezekane?*

## E. Ushirika wa Makanisa ya Kikanda

31. Mafundisho ya kanisa juu ya ushirika yanatoa muundo unaosaidia kufikiri juu ya uhusiano kati ya kanisa la eneo fulani na Kanisa la ulimwengu mzima. Wakristo wengi wanaweza kukubaliana kuwa kanisa la eneo fulani ni "jumuiya ya waumini waliobatizwa ambamo Neno la Mungu linahubiriwa, imani ya mitume hukiriwa, sakramenti husherehekewa, na kazi za wokovu za Kristo kwa ajili ya dunia nzima hushuhudiwa, na huduma za kichungaji/kiaskofu hufanywa na maaskofu au watumishi wengine katika kuihudumia jumuiya."[15] Utamaduni, lugha, na historia ya

[15] Ling. ripoti ya Kikozi Kazi cha Pamoja cha Baraza la Makanisa Ulimwenguni na Kanisa Katoliki la Kirumi, "The Church: Local and

pamoja vyote vinaingia katika kutengeneza mazingira ya kanisa la eneo husika. Wakati huo huo, jumuiya ya Kikristo katika kila eneo inashiriki na jumuiya zingine zote za mahali hapo mambo yote ambayo ni muhimu katika maisha ya ushirika. Kila kanisa mahali lilipo lina kile kinachoweza kuwa Kanisa katika utimilifu wake. Ni Kanisa kabisa, lakini si Kanisa zima. Kwa hiyo, kanisa la eneo fulani lisitazamwe kama kitu kilichojitenga, bali lililo katika msukumo wa mahusiano na makanisa mengine ya ukanda huo. Toka mwanzo ushirika uliimarishwa kati ya makanisa ya maeneo kwa njia ya matoleo, kubadilishana habari kwa njia ya barua, ziara, ukarimu wa kiekaristi takatifu na matamko ya mshikamano wa dhati (ling. 1 Kor. 16: 2 Kor 8:1-9; Gal. 2:1-10). Kutoka wakati mmoja hadi mwingine, enzi ya karne zaa kwanza, makanisa katika kanda moja yalikusanyika kushauriana pamoja. Mambo yote haya yalikuwa ni njia ya kutunza kutegemeana na kuimarisha ushirika. Ushirika huu wa makanisa ya maeneo si kitu cha ziada au mbadala. Kanisa la kiulimwengu ni ushirika wa makanisa yote popote yalipo yakiunganishwa na imani na ibada duniani kote.[16] Si tu ni jumla au muungano wa kuwekwa pamoja pamoja na tofauti zilizopo, bali makanisa yote kwa pamoja ni Kanisa lile lile lililopo na linalotenda katika dunia hii. Kanisa la watu wote, kama linavyoelezwa katika fundisho la ubatizo la Cirili ya Yerusalemu, linarejea si tu upana wa

---

Universal," §15, katika *Growth in Agreement II,* 866. Kanisa la "kieneo" lisichanganywe na "dhehebu" katika maelezo haya.

[16] Ling. matamko ya kuhimiza umoja ya mikutano ya Baraza la Makanisa Duniani ya New Delhi, Uppsala, na Nairobi katika W. A. Visser't Hooft (mhariri.), *The New Delhi Report: The Third Assembly of the World Council of Churches 1961*, London, SCM, 1962, 116-134; N. Goodall (mhariri.), *The Uppsala Report 1968: Official Report of the Fourth Assembly of the World Council of Churches,* Geneva, WCC, 1968, 11-19; na D. M. Paton (mhariri.), *Breaking Barriers Nairobi 1975: The Official Report of the Fifth Assembly of the World Council of Churches*, London-Grand Rapids, SPCK-Eerdmans, 1976, 59-69.

kijiografia bali pia uwingi wa makanisa mbalimbali ya eneo hilo na katika ushiriki wake katika ukamilifu wa imani na maisha ambavyo vinayaunganisha hayo makanisa kuwa ushirika mmoja.[17]

32. Katika uelewa huu wa ushirikiano wa jumuiya za makanisa ya kimaeneo katika Kanisa la kikatoliki, tofauti hujitokeza, si tu kuhusu kuenea kijiografia kwa jumuiya inayokusudiwa katika msemo wa "kanisa la eneo," bali pia kuhusiana na suala la wajibu wa huduma za maaskofu. Makanisa mengine yanashawishiwa kwamba askofu, kama ofisi ya mwendelezo wa historia ya mitume, ni muhimu katika mfumo na uyakinifu kuhusu kanisa la eneo fulani. Hivyo, katika utashi huu, kanisa la mahali fulani ni dayosisi inayojumuisha sharika mbalimbali. Kwa wengine baada ya kuwa na uelewa wake wenyewe, msemo "kanisa la eneo" si maarufu sana na hautafsiriwi kwa kurejea huduma ya askofu. Kwa baadhi ya makanisa kama hayo, kanisa la eneo fulani ni kama usharika tu wa waumini waliokutanika mahali pamoja ili kusikia Neno  na kushiriki Sakramenti. Wote wanaoona umuhimu wa askofu na wasioona hivyo msemo "kanisa la eneo" limekuwa likitumika nyakati nyingine kumaanisha eneo la makanisa, yanayokutanika pamoja katika mfumo wa kisinodi chini ya uraisi. Kwa kumalizia, bado hakuna makubaliano kuhusu jinsi muundo wa kikanisa wa eneo fulani, unavyosaidia makanisa yahusiane kieneo na kidunia, ingawa hatua muhimu katika kutafuta mwafaka kuhusu mahusiano hayo zinaweza kuonekana katika mazungumzo ya kimataifa na katika ya makanisa ya kikanda.[18]

---

[17] Cyril of Jerusalem, *Catechesis 18*, katika J. P. Migne, *Patrologia Graeca* 33, 1044.

[18] Mfamo mzuri wa mazungumzo katika ngazi ya kimataifa ni Ripoti ya Kikosi Kazi cha Pamoja cha Baraza la Makanisa Duniani na Kanisa Katoliki la

### ***Uhusiano wa Kanisa la Eneo na la Kiulimwengu***

*Makanisa mengi yanaweza kushirikiana kuelewa mafundisho ya msingi na ushirika wa makanisa ya eneo fulani ndani ya Kanisa zima la kiulimwengu. Wanashirikiana kuelewa kuwa uwepo wa Kristo, kwa mapenzi ya Baba na nguvu ya Roho Mtakatifu, kweli unaonyeshwa katika kanisa la kienyeji (ni "Kanisa kamili"), na kwamba uwepo huu hasa wa Kristo unachochea kanisa la eneo hilo kuwa katika ushirika na Kanisa la ulimwengu wote (si "Kanisa zima"). Pale kunapokuwa na makubaliano haya ya msingi, msemo "kanisa la eneo" linaweza hata hivyo kutumika kwa njia tofauti. Katika hitaji letu la pamoja la umoja wa karibu, tunayaalika makanisa kutafuta kwa usahihi zaidi maelewano na makubaliano ya pamoja katika eneo hili: Ni uhusiano gani ulio sahihi katika hatua mbalimbali za maisha ya Kanisa lililoungana kikamilifu na ni huduma gani za kiuongozi zinatakiwa zidumishwe ili kulisaidia Kanisa liendeleze mahusiano yaliyoanzishwa?*

---

Kirumi, katika andiko lenye kichwa, "The Church: Local and Universal," http://www.oikoumene.org/en/resources/documents/wcc-commissions/.

Ling. pia *Growth in Agreement II*, 862-875. Kutoka mazungumzo ya kikanda ya Walutheri-Wakatoliki, angalia "Ecclesial Communion - Communion of Churches," na "Church and Justification," katika *Growth in Agreement*, 505-512; na hasa tamko la Waorthodoksi-Wakatoliki juu ya "Ecclesiological and Canonical Consequences of the Sacramental Nature of the Church: Ecclesial Communion, Conciliarity and Authority," (2007), kwenye tovuti ya http://www.pcf.va/romancuria/pontifical_councils/chrstuni/ch_orthodox_docs/re_pc_chrstuni_doc20071013_documento-ravenna_en.html.

## Sura ya III

## Kanisa: Kukua katika Ushirika

### A. Tayari lakini Bado

33. Kanisa ni hakika ya mambo yajayo, tayari ufalme unatarajiwa, lakini bado utimilifu wake. Roho Mtakatifu ni wakala wa msingi katika kuujenga ufalme na katika kuliongoza Kanisa ili katika mchakato huu Kanisa liwe mhudumu wa kazi ya Mungu. Kama tunavyoona mambo ya sasa kwa njia ya mwanga tu kwa njia ya kazi za Roho Mtakatifu, anayeongoza mchakato mzima wa historia ya wokovu kufikia utimilifu wake katika Kristo kwa utukufu wa Baba, ndipo tunapopata jambo kuhusu fumbo la Kanisa.

34. Kwa upande mmoja, ushirika wa waaminio unapokuwa na mahusiano binafsi na Mungu, Kanisa tayari ni ushirika ujao unaotakiwa na Mungu. Alama zinazoonekana na zinazoguswa zinaeleza kuwa maisha haya mapya ya ushirika yanayotimilika ni: kupokea na kushiriki imani ya mitume, kubatiza, kumega na kushiriki ekaristi ya mkate, kuomba pamoja na kwa ajili ya wengine na kwa ajili ya mahitaji ya dunia, kuhudumiana kwa upendo, kushiriki katika furaha na huzuni ya kila mmoja, kutoa misaada ya hali na mali, kutangaza na kushuhudia habari njema katika misheni, na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya kuleta haki na amani. Kwa upande mwingine, Kanisa lililopo, kama kweli ya kihistoria, limeumbwa na wanadamu ambao wanaishi kwa kufuata masharti ya dunia hii. Mojawapo la sharti ni mabadiliko[1] chanya katika hali ya kukua na kuendelea  au hasi katika

---

[1] Sharti hili la mabadiliko halina maana ya kupuuza maana ya wakati wote ya Yesu Kristo na Injili yake: "Yesu ni yeye yule jana na leo na hata milele" (Ebr 13:8).

kudumaa na kuvurugika. Masharti mengine ni ya sababu za kitamaduni au kihistoria ambayo yanaweza kuleta matokeo chanya au hasi katika imani, maisha, na ushuhuda wa Kanisa.

35. Kama jumuiya iliyo kwenye hija wakati wote, Kanisa linashindana na kweli ya dhambi. Mazungumzo ya kiekumene yameonyesha kwamba kuna misimamo ya kina inayoshikiliwa nyuma ya mambo ambayo wakati mwingine yameonekana kuleta tofauti kuhusu mahusiano kati ya utakatifu wa Kanisa na dhambi ya mwanadamu. Kuna tofauti za msingi jinsi Wakristo wanavyoelezea kwa ufasaha kuhusu misimamo hii. Mapokeo ya wengine yanathibitisha kuwa Kanisa halina dhambi, kwa kuwa ni mwili wa Kristo asiye na dhambi, na hivyo haliwezi kutenda dhambi. Wengine wanaamini kuwa ni sahihi kukiri kuwa Kanisa linatenda dhambi, kwa kuwa dhambi inaweza kuwa ya kimfumo na kwa ajili hiyo kuathiri taasisi ya Kanisa lenyewe na hata kama dhambi ni iko kinyume na ukweli wa utambulisho wa Kanisa, bado katika hali halisi ipo. Njia mbalimbali ambazo jumuiya mbalimbali zinaeielewa dhambi yenyewe, iwe kwa msingi wa kutokutimilika kimaadili au kuvunja mahusiano, au dhambi ya kimfumo, bado tafsiri hizi zinaweza kuwa na matokeo tofauti katika swali hili.

36. Kanisa ni mwili wa Kristo; kulingana na ahadi yake, malango ya kuzimu hayawezi kulishinda (ling. 16:18). Ushindi wa Kristo juu ya dhambi ni kamili na usiobadilika, na kwa njia ya ahadi na neema yake, Wakristo wana uhakika kwamba Kanisa mara zote litashiriki matunda ya ushindi huo. Wakristo pia wanashirikiana kutambua kuwa, katika enzi ya sasa, waumini wako katika hatari ya kukumbwa na nguvu ya dhambi, mtu mmoja mmoja au kwa pamoja. Makanisa yote yanakiri mara kwa mara ukweli huu uliopo wa dhambi miongoni wa waumini na adhari zake. Makanisa yanatambua mahitaji endelevu ya Wakristo ya kujikagua, kutubu, kumrudia

(Mungu), kupatana, na kuamka kwa upya. Utakatifu na dhambi vinahusiana na maisha ya Kanisa katika njia tofauti na zisizo na usawa. Utakatifu unauelezea utambulisho wa Kanisa kulingana na mapenzi ya Mungu, wakati dhambi inasimama kinyume na utambulisho huu (ling. Rum 6:1-11).

### B. Kukua Katika Mambo Muhimu ya Ushirika: Imani, Sakramenti, na Huduma

37. Safari ya kuelekea kwenye ukweli wa tuzo ya Mungu ya ushirika kunahitaji jumuiya za Kikristo kukubaliana kuhusu mambo ya msingi ya maisha ya Kanisa. "Mambo yahusuyo kanisa yanayohitajika kwa ajili ya ushirika kamili ndani ya kanisa lililoungana kwa kuonekana - lengo la harakati za kiekumene - ni ushirika katika ukamilifu wa imani ya kimitume; katika mifumo ya mahusiano ya mitaguso na maamuzi; na katika ushuhuda wa pamoja na huduma kwa dunia."[2] Sifa hizi zinafanya muundo wa lazima kwa ajili ya

---

[2] Kutoka "The Church: Local and Universal," 1990, §25, in *Growth in Agreement II*, 868. Sura 10-11 na 28-32 za chapisho hili zinaonyesha kwa nukuu na maelezo ya rejea ukweli kwamba uwakilishaji wake wa ushirika umetokana na mazungumzo mapana ya kiekumene yaliyohusisha Waangalikana, Walutheri, Wamethodisti, Waorthodoksi, Kanisa la Matengenezo na Wakatoliki na pia limehusisha matamko mbalimbali juu ya umoja yaliyopitishwa katika mojawapo ya mikutano ya BMD (ling maelezo ya chini 16, sur. 2). Tamko la Baraza la Makanisa la Dunia, "Unity of the Church as *Koinonia*: Gift and Calling," alama ya huduma kuonekana kwa kuongeza neno kupatanishwa kwenye neno la kutambuliwa [M. Kinnamon (mhariri.) *Signs of the Spirit: Official Report Seventh Assembly*, Geneva, WCC., 1991, 173]. Mipangilio inayofanana juu ya mambo ya msingi juu ya ushirika unaonekana katika hati za Kilutheri-Kanisa Katoliki la Kirumi "Facing Unity," katika *Growth in agreement II*, 456-477, inayowasilisha kanisa kama jumuiya ya imani, sakramenti na huduma; na Kimethodisti-Kikatoliki katika chapisho la "The Apostolic Tradition," katika *Growth in Agreement II*, 610-613, inayoelezea mwili ulio hai wa kanisa kwa njia ya imani, ibada na huduma. Matamko yaliyozoeleka kuhusu umoja kutoka mikutano ya BMD ya New Delhi (1960), Nairobi (1975), Canberra (1990) na Porto alegre (2006) pia yanawasilisha

kuimarisha umoja katika hali ya tofauti [halali] zilizopo. Zaidi sana, kukua kwa makanisa kuelekea umoja wa kuwa Kanisa moja kunahusiana kabisa na wito wake wa kuhamasisha umoja wa wanadamu na uumbaji wote, tangu Kristo, ambaye ndiyo kichwa cha Kanisa, ambaye ni mmoja, na katika yeye vitu vyote vinapatanishwa. Mazungumzo kama yale yaliyosaidia machapisho na mapokeo ya *Ubatizo, Ekaristi, na Huduma*, tayari yameonyesha maendeleo muhimu katika muafaka kuhusu mambo haya muhimu ya ushirika, ingawa kiwango kidogo kimefikiwa katika huduma na si kama ilivyo katika mambo mawili [ya Sakramenti]. Si lengo la chapisho hili la sasa kurudia mafanikio haya yaliyopita, lakini kwa kiwango fulani linayaweka kwa kifupi na kuonyesha baadhi ya hatua zinazoendelea kuchukuliwa zaidi kwa kwa maamuzi yaliyopita.

### ***Imani***

38. Kuhusiana na mambo haya ya kwanza kuna makubaliano yaliyosambazwa kuwa Kanisa limeitwa kutangaza imani kwa kila kizazi "waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda mst. 3) na kudumu katika mafundisho ambayo yalienezwa hapo kale na mitume. Imani inakumbukwa kwa njia ya Neno la Mungu, inahamasishwa kwa njia ya neema ya Roho Mtakatifu, inadhibitishwa katika Maandiko Matakatifu na

---

vionjo muhimu vya umoja, kama ilivyo katika rejea hizi za mwishoni ambazo zinaweza kutumika kuonyesha: "Makanisa yetu yamethibitisha kuwa umoja ambao tunauombea, matumaini na kazi ni "ushirika unaotolewa na kuelezwa katika ukiri wa pamoja wa imani ya mitume; maisha ya pamoja ya sakramenti yanayoanzishwa na ubatizo mmoja na kusherehekewa pamoja katika ushirika wa ekaristi takatifu; maisha ya pamoja ambapo washiriki na watumishi wanajitambua na kupatana kwa pamoja; na misheni ya pamoja ya kushuhudia injili ya neema ya Mungu kwa watu wote na huduma kwa dunia yote." Ushirika huu unatakiwa uelezwe sehemu zote, na kwa njia ya mahusiano ya mitaguso ya makanisa katika maeneo mbalimbali," katika "Called to Be the One Church," §2, *Growth in Agreement in III*, 606-607.

inaenezwa kwa njia ya mapokeo hai ya Kanisa. Imani inashuhudiwa katika ibada, maisha ya kila siku, katika huduma na katika misheni [ya Mungu]. Ingawa imani hii inatakiwa itafsiriwe kukabiliana na mabadiliko ya mazingira ya nyakati na mahali, bado tafsiri yake ni lazima ibakie kuwa mwendelezo wa ushuhuda wa asili na unaodumisha tafsiri yake inayoaminika kwa vizazi vyote. Imani ni lazima kuiishi ili kuitikia changamoto za kila wakati na mahali kivitendo. Imani izungumze kufuatana na hali ya mtu na jamii, ikijumuisha pia utetezi dhidi ya hali ya uonevu, uvunjaji wa haki za binadamu na uharibifu wa mazingira.

39. Mazungumzo ya kiekumene yameonyesha kuwa katika mafundisho mengi ya msingi ya Kikristo, kuna jambo kubwa ambalo tayari linawaunganisha waumini.[3] Mwaka 1991, utafiti juu ya *Kukiri Imani Moja* si tu ulifaulu katika kuonyesha makubaliano ya makubwa yaliyofikiwa miongoni mwa Wakristo kuhusu maana ya Ukiri wa Imani ya Nikea katika liturgia za makanisa mengi. Pia andiko hili lilifanikiwa kuelezea jinsi ukiri wa imani ulivyojengewa msingi wake katika Maandiko Matakatifu, na unashuhudiwa katika alama za kiekumene na inatakiwa kukiri kwa upya kila zinapojitokeza changamoto katika wakati huu wa dunia ya sasa. Lengo si tu lilikuwa kuyasaidia makanisa yatambue hali ya uhai wake yenyewe na mengine katika imani, bali pia kutoa mwanya wa chombo cha kiekumene kinachofaa kwa ajili ya kuitangaza imani hiyo wakati wa sasa. Mwaka 1998, *Hazina ya Vyombo vya Ardhini*, ilichunguza tafsiri zinazoendelea za Maandiko

[3] Angalia kwa mfano, sura za "Fundamentals of Our Common Faith: Jesus Christ and the Holy Trinity" na "Salvation, Justification, Sanctification" kwenye andiko la Walter Kasper's, *Harvesting the Fruits: Basic Aspects of Christian Faith in Dialogue*, London-New York, Continuum, 2007, 10-47, inayorudia juu ya muafaka kuhusu mada kati ya Waanglikana, Walutheri, Wamethodisti, Katika la Matengenezo na Kanisa Katoliki la Kirumi.

Matakatifu na Mapokeo ya Kanisa katika kurithisha imani , ikirejea kuwa "Roho Mtakatifu anahamasisha na kuyaongoza makanisa kila moja kufikiria na kutafsiri kwa upya mapokeo yake katika mazungumzo kati yake, wakati wote yakilenga katika kuujenga utamaduni mmoja katika umoja wa Kanisa la Mungu."[4] Wakati makanisa yanakubaliana kwa ujumla wake juu ya umuhimu wa mapokeo kati ya vizazi na katika tafsiri za maandiko zinazoambatana nayo, mazungumzo ya sasa yamejaribu kuleta uelewa zaidi jinsi jumuiya za Kikristo zinavyoshiriki katika tafsiri hiyo. Mazungumzo mengi ya kikanda yametambua kuwa tafsiri ya mafundisho ya sasa yanayomaanisha Kanisa kuwa ni Neno la Mungu, yanajumuisha uzoefu wa kiimani wa watu wote, maono ya watheologia, na utambuzi wa wachungaji waliobarikiwa.[5]

---

[4] Andiko la *A Treasure in Earthen Vessels*, Geneva, WCC, 1998, §32. Kabla ya hapo andiko la *Baptism, Eucharist, Ministry*, sehemu ya Huduma, §34 lilijulisha kuwa: "Mapokeo ya kitume katika Kanisa maana yake ni mwendelezo wa hali ya tabia ya kudumu ya Kanisa la Mitume: kukiri imani ya mitume, kutangaza na tafsiri mpya ya Injili, kusherehekea sakramenti za ubatizo na ekaristi takatifu, kueneza wajibu wa kichungaji, ushirika katika maombi, upendo, furaha na mateso, kuwahudumia wagonjwa na wahitaji, umoja katika ya makanisa ya kila mahali na kushirikishana karama ambazo Bwana ametoa kwa kila mmoja"; katika, *Baptism, Eucharist, Ministry*, Geneva, WCC, 1982.

[5] Angalia kwa mfano, tamko la Kilutheri-Kiorthodoksi "Scripture and Tradition," katika *Growth in Agreement II*, 224-225; tamko la Kimethodisti-Kikatoliki "The Word of Life," §§62-72, likieleza "Agents of Discernment," katika *Growth in Agreement I*, 632-634; tamko la Kianglikana-Kikatoliki "Gift of Authority," katika *Growth in Agreement III*, 60-81; tamko la Kanisa la Ufuasi-Kikatoliki "Receiving and Handing on the Faith: The Mission and Responsibility of the Church," katika *Agreement III*, 121-137; tamko la Kimethodisti-Kikatoliki "Speaking the Truth in Love: Teaching Authority among Catholics and Methodists," katika *Growth in Agreement III*, 138-176; na "Ripoti" ya makanisa ya Kimatengenezo-Kiorienti Kiorthodoksi (2001), §§22-28, likifafanua "Tradition and Holy Scripture" na "The Role of the Theologian in the Christian Community," katika *Growth in Agreement III*, 43-44.

Changamoto ya leo ni kwa makanisa kukubaliana jinsi mambo haya yanavyofanya kazi kwa pamoja.

### *Sakramenti*

40. Kuhusu sakramenti makanisa yameonyesha kiwango fulani cha kukubali namna jinsi andiko kuhusu *Ubatizo, Ekaristi Takatifu na Huduma (1982)* linavyoeleza maana na namna ya kusherehekea ubatizo na ekaristi takatifu.[6] Andiko hili pia linatoa mapendekezo ya maeneo ya yanayotafutiwa muafaka zaidi kwa mambo yale yanayoonekana kuwa muhimu lakini hayajapatiwa ufumbuzi: kama vile, nani anaweza kubatizwa, uwepo wa Kristo katika ekaristi takatifu, na uhusiano wa ekaristi takatifu na Kristo kujitoa sadaka pale msalabani. Wakati huo huo, andiko hili la *Ubatizo, Ekaristi Takatifu na Huduma*, likitoa maoni juu ya kubariki Wakristo kwa njia ya kupaka mafuta au kipaimara, halikutatua utata wa ibada zingine zinazosherehekewa katika jumuiya nyingi na zinazofikiriwa na wengine kuwa ni sakramenti, na wala halikulenga kuyachukulia maanani maoni ya jumuiya hizo zinazothibitisha kuwa miito yao haihusishi ibada za ubatizo na ekaristi takatifu, huku wakidai kuwa wanashiriki katika sakramenti ya maisha ya Kanisa.

41. Kukua kwa maridhiano kati ya makanisa katika kuuelewa ubatizo kunaainishwa kwa kifupi kama ifuatavyo.[7]

---

[6] Ling. *Baptism, Eucharist and Ministry, 1982-1990: Report on the Process and Responses*, Geneva, WCC, 1990, 39,55-56.

[7] Aya hii inarudia mambo yaliyolifafanuliwa katika sura ndogo "II. The Meaning of Baptism," katika *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya Ubatizo §§2-7. Uthibitisho unaofanana kutokana na mikutano minne ya ya mazungumzo ya kimataifa iliyofanyika kikanda unapatikana katika "Common Understanding of Baptism" na W. Kasper, *Harvesting the Fruits*, 164-168, na kama ilivyo katika andiko la Imani na Utaratibu wa Ibada lililopewa jina la *One Baptism: Towards Mutual Recognition*, Geneva, WCC, 2011.

Kwa njia ya ubatizo wa maji katika Jina la Mungu wa Utatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, Wakristo wanaunganishwa na Kristo na wenyewe kwa wenyewe ndani ya Kanisa wakati wote na mahali popote. Ubatizo ni kuingizwa na kusherehekea maisha mapya katika Kristo na hivyo kushiriki katika ubatizo, maisha, kifo na kufufuka kwake (ling. Matt. 3:13-17; Rum 6:3-5). Ni "kwa kuzaliwa mara ya pili na kufanywa upya kwa njia ya Roho Mtakatifu" (Tito 3:5b) waumini wanaunganishwa katika mwili wa Kristo na kuwezeshwa kushiriki katika ufalme wa Mungu na katika maisha ya ulimwengu ujao (ling. Efe 2:6). Ubatizo unahusisha kutubu dhambi, kugeuka moyoni, kusamehe, kusafishwa na kutakaswa; muumini anawekwa wakfu kama mshiriki wa "ukuhani wa kifalme, taifa takatifu [la Mungu]" (1 Pet 2:9). Kwa hiyo ubatizo ni kiungo cha msingi cha umoja. Makanisa mengine huona karama ya Roho Mtakatifu kama kitu kinachotolewa kipekee kwa njia ya upako wa mafuta maalumu au kipaimara, na kufikiriwa na makanisa hayo kama moja ya sakramenti za kumuingiza mtu katika kundi. Makubaliano ya jumla kuhusu ubatizo yamepelekea wale wanaoshiriki katika harakati za kiekumene kuyaalika makanisa kwa ajili ya utambuzi wa pamoja wa ubatizo.[8]

42. Kuna uhusiano wenye msukumo na wenye msingi kati ya ubatizo na ekaristi takatifu. Ushirika ambao Mkristo mpya aliyebatizwa anaingizwa unaletwa kwenye maelezo makamilifu na kulishwa vizuri katika ekaristi takatifu, inayothibitisha kwa upya imani ya ubatizo na kuleta neema kwa ajili ya uhai wa kiimani utokanao na wito wa Mkristo. Maendeleo ya makubaliano kuhusu ekaristi takatifu yalioingizwa katika mazungumzo ya kiekumene yanaweza

[8] Mfano wa ufahamu wa pamoja juu ya ubatizo ulifikiwa na wanachama kumi na moja kati ya kumi na sita wa jumuiya za Baraza la Makanisa ya Ujerumani 29 Aprili, 2007, kama inavyoonyeshwa katika http//www.ekd.de/english/mutual_recognition_of_baptism.html.

kuwekwa kwa kifupi kama ifuatavyo.[9] Chakula cha Bwana ni sherehe ambapo, Wakristo waliokusanyika mezani pake, wanapata mwili na damu ya Kristo. Ni tangazo la Injili, kumsifu Baba kwa ajili ya kukamilishwa kwa uumbaji, ukombozi na utakaso (*doxologia*): kumbukumbu ya kifo na kufufuka kwa Kristo Yesu na kile kilichotimizwa mara moja kwa ajili ya wote pale msalabani (*anamnesis*): na sala ya Roho Mtakatifu katika kubadili vitu vya mkate na mvinyo na kuwabadili washiriki wenyewe (*epclesis*). Maombi hufanywa kwa ajili ya mahitaji ya Kanisa na dunia, ushirika wa waaminio unaimarishwa kwa kina kama tarajio na onjo la kabla ya kuja kwa uzima ujao, na kuwasukuma kutoka nje na kushirikisha wengine misheni ya Kristo ya kuusimika ufalme huu hata sasa. Mtume Paul anasisitiza uhusiano uliopo kati ya Chakula cha Bwana na maisha halisi ya Kanisa (ling. 1 Kor. 10:16-17; 11:17-33).

43. Kama ilivyo kwa ukiri wa imani na ubatizo kuwa ni vitu visivyotenganishwa kutoka maisha ya huduma na ushuhuda, hata ekaristi takatifu inahitaji upatanisho na ushirikiano wa wale wote ambao ni kaka na dada katika familia moja ya Mungu. "Wakristo wanaitwa kwa njia ya ekaristi takatifu kuwa na umoja na wale waliotengwa na jumuiya zao na kuwa alama za upendo wa Kristo aliyeishi na kujitolea maisha yake sadaka kwa ajili ya wote na sasa anajitoa mwenyewe kwa njia ya ekaristi takatifu... Ekaristi takatifu inaleta ukweli mpya unaothihirishwa katika nyakati za sasa na kuwabadilisha Wakristo kuwa mfano wa Yesu Kristo na hivyo

[9] Ufupisho huu unatokana na "II. The meaning of the Eucharist" katika *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya Ekaristi Takatifu, §§ 2-26. Utofauti wa viwango mbalimbali vya muafaka kati ya Waanglikana, Walutheri, Wamethodisti, Wamatengenezo na Wakatoliki, angalia "The Eucharist," katika Kasper, *Harvesting the Fruits*, 168-190.

kuwafanya mashahili wenye ufanisi."[10] Utengenezaji upya wa liturgia miongoni mwa makanisa unaweza kuonekana kuwa sehemu ya kupokea muafaka ulifikiwa katika mazungumzo ya kiekumene kuhusu sakramenti hizi.

44. Mapokeo mbalimbali ya Kikristo yamepindisha ubatizo, ekaristi takatifu na ibada zingine viitwe, "sakramenti" au "taratibu tu za kiibada." Neno *sakramenti* (linalotumika kutafsiri neno la Kiyunani *mysterion*) linaonyesha kuwa kazi ya Mungu ya kuokoa inathibitishwa katika tendo la ibada, wakati neno *utaratibu wa ibada* linakazia kuwa tendo la ibada linafanywa katika kutii neno na mfano wa Kristo.[11] Misimamo hii miwili imekuwa ikionekana kama ikipingana. Hata hivyo, kama andiko la Imani na Utaratibu wa Ibada katika *Ubatizo Mmoja* linavyoonyesha, "mapekeo yaliyo mengi, yawe yanatumia neno 'sakramenti' au 'utaratibu wa ibada', yanathibitisha kuwa matukio haya mawili ni *muhimu* (kwamba Mungu anatumia matukio haya kuleta ukweli mpya), na *yanaueleza* (ukweli ambao tayari upo). Mapokeo mengine yanahimiza msimamo wa sakramenti kutumika kama vyombo tu... Wengine wanasistiza msimamo wa kimaelezo tu."[12] Je tofauti hizi zinaweza kuwa zaidi ya moja ya mikazo kuliko kutokukubaliana katika mafundisho? Ibada hizi zinaeleza jinsi mambo ya Kanisa yanavyofuata taratibu za kimifumo au zisizo za kimifumo. Ibada hizi zinaonekana na kuleta mambo yanayofaa zikiwa zimeanzishwa na Kristo na wakati huo huo zikiwezeshwa zaidi na tendo la Roho Mtakatifu, ambaye kwa njia ya ibada hizi, anawajengea uwezo wale wanaopokea sakramenti na kuwapa

[10] Kutoka *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya "Huduma," §§24 na 26

[11] Neno la Kilatini *sakramentum* linaashiria kiapo cha mtu anayeamua kujiunga na shughuli za kijeshi na lilitumika na watheologia wakubwa wa kwanza kuandika katika lugha ya Kilatini, Tertullian (160-220), kumaanisha ubatizo.

[12] *One Baptism: Towards Mutual Recognition*, §30.

karama mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa na misheni yake ndani na kwa ajili ya dunia yote.

### *Sakramenti na Taratibu za Ibada*

*Kwa kufuata maridhiano yaliyofikiwa ya Ubatizo na Ekaristi Takatifu na tafsiri zaidi kwa kufuata mizizi ya kihistoria na uwiano mzuri wa misemo ya "sakramenti" na "taratibu za ibada," makanisa yanapewa changamoto ya kutafiti zaidi kama yanaweza kufikia makubaliano ya kina kuhusu misimamo ile ya maisha ya Kanisa ambayo inahusisha ibada hizi. Muafaka kama huu unaweza ukawafikisha kutafakari juu ya maswali kadhaa ya nyongeza. Makanisa mengi yanaadhimisha ibada au sakramenti nyingine, kama vile kubariki waliobatizwa kwa kupaka mafuta/kimaipara, ndoa na ubarikio wa wachungaji ndani ya liturgia zao na wengine pia wana ibada kwa ajili ya kusamehe dhambi na kubariki [kuponya] wagonjwa: je haiwezekani idadi na hali ya sakramenti au taratibu za ibada hizi zikajadiliwa katika mazungumzo ya kiekumene? Pia tunayaalika makanisa kufikiria kama kwa sasa yanaweza kufikia muafaka wa karibu zaidi kuhusu wale wanaotakiwa kubatizwa na wale wanaoweza kuongoza wakati wa kuadhimisha liturgia ya Kanisa? Zaidi sana, kunaweza kukawa na njia ambapo uelewa kamili wa pamoja unaweza kuanzishwa kati ya makanisa yanayoadhimisha ibada hizi na jumuiya zile za Kikristo zilizoshawishika kuwa maisha ya ushirikiano katika Kristo hayahitaji maadhimisho ya sakramenti au ibada zingine?*

### *Huduma ndani ya Kanisa*

*Utumishi wa Kubarikiwa*

45. Makanisa yote yanathibitisha mafundisho haya ya kibiblia kuwa, kinyume na makuhani wengi wa Agano la Kale (ling. Ebr 7:23), Yesu, ambaye ndiye kuhani wetu mkuu (ling. Ebr. 8:10), alijitolea sadaka kwa ajili ya wokovu "mara moja kwa ajili yetu" (ling. Ebr 7:27; 9:12; 9:26; 10:10, 12-14). Makanisa yanatofautiana kuhusu tafsiri yanazozitoa kutokana na masomo haya. Andiko la *Ubatizo, Ekaristi Takatifu na Huduma* linaonyesha kuwa wachungaji waliobarikiwa "wanaweza kuitwa makuhani kwa usahihi kwa sababu wanatimiza wajibu maalumu wa huduma ya kikuhani ili kuimarisha na kuujenga ukuhani wa kifalme na kinabii wa watu wote waaminio kwa njia ya neno na sakramenti, maombi, na kwa njia ya uongozi wa kichungaji wa jumuiya zao."[13] Sambamba na mtazamo huo, baadhi ya makanisa yanashikilia kuwa uchungaji wa kubarikiwa unawakilisha mahusiano maalumu na ukuhani wa kipekee wa Kristo ambao ni tofauti, hata kama unahusiana na ukuhani wa kifalme wa watu wote kama ulivyoandikwa katika 1 Pet. 2:9. Makanisa haya yanaamini kuwa baadhi ya watu wamebarikiwa kwa ajili ya kufanya kazi maalumu ya kikuhani kwa njia ya sakramenti ya ubarikio.[14] Wengine hawawatambui kama watumishi yaani "makuhani" wa kubarikiwa, kuwa wala hawaelewi kama ubarikio ni neno la kisakramenti. Wakristo hawakubaliani pia kuhusu kutenga utumishi wa kubarikiwa kwa ajili ya neno na sakramenti kwa ajili ya wanaume tu.

### *Utumishi wa Kubarikiwa*

---

[13] *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya Huduma, §17.

[14] Angalia andiko la Kianglikana-Kikatoliki "Ministry and Ordination" na "Elucidation," katika *Growth in Agreement I*, 78-87; na mazungumzo ya Kiorthodoksi-Kikatoliki, "The Sacrament of Order in the Sacramental Structure of the Church," katika *Growth in Agreement II*, 671-679.

*Mazungumzo ya kiekumene yamejirudia kuonyesha kuwa mambo yanayohusiana na utumishi wa kubarikiwa yanahusisha vikwazo vinavyoleta changamoto kuelekea kwenye njia ya umoja. Kama tofauti kama zile zinazohusiana na ukuhani wa kubarikiwa unazuia umoja kamili, ni nini kipewe kipaumbele cha haraka kwa makanisa kugundua jinsi ya kukabiliana na hali hiyo.*

46. Hakuna kipengele hata kimoja kuhusu huduma katika Agano Jipya, ingawa makanisa yote yanategemea Maandiko Matakatifu katika kutafuta kufuata mapenzi ya Mungu, kinachohusu jinsi gani ubarikio wa wachungaji unatakiwa kueleweka, kuwekewa utaratibu na kufanyika. Wakati fulani, Roho [Mtakatifu] ameliongoza Kanisa kuweka huduma ya kichungaji kwa kufuata mahitaji ya mazingira lilipo (ling. Matendo 6:1-6). Mifumo mbalimbali ya huduma ya kichungaji imebarikiwa na vipawa vya Roho Mtakatifu. Waandishi wa kwanza, kama Ignatio wa Antiokia, walisisitiza mihimili mitatu, yaani uaskofu, uzee wa kanisa, na udiakonia.[15] Kipengele hiki cha huduma tatu zinazohusiana kinaonyesha kuwa na mizizi katika Agano Jipya; na hatimaye kipengele hiki kimsingi kinakubalika kwa ujumla wake na kinafikiriwa kuwa halali kwa makanisa mengi ya leo. Makanisa mengine, kuanzia wakati Matengenezo ya Kanisa, yamepitisha vipengele tofauti vya huduma ya kichungaji.[16] Kati ya njia nyingi za kuimarisha utume wa Kanisa wa mfuatano, kama vile kipimo cha maandiko, mafundisho na utaratibu wa liturgia, suala la uchungaji wa kubarikiwa lina mchango mkubwa. Mnyororo

---

[15] Ling. Ignatius of Antioch's *Letter to the Magnesians* 6 and 13; *Letter to the Trallians* 7; *Letter to the Philadephians* 4; *Letter to the Smyrnaeans* 8.

[16] Masimulizi mbili zenye kusisimua kuhusu maendeleo haya ya Matengenezo ni andiko la Kanisa la Matengenezo na Katoliki "Towards a Common Understanding of the Church," §§12-63, likiitwa "Toward a Reconciliation of Memories," katika *Growth in Agreement II*, 781-795; na andiko la Kilutheri-Kikatoliki, *Apostolicity of the Church*, Minneapolis 2006, §§65-164, uk. 40-71.

katika utumishi wa kichungaji unakusudiwa kuendeleza utume wa Kanisa.

47. Karibu jumuiya zote za Kikristo kwa sasa zina mifumo rasmi ya huduma. Miundo hii wakati mwingi imetofautishwa na inaakisi, kwa kiwango fulani, vipengele vitatu yaani *uaskofu-uzee wa kanisa na udiakonia*. Makanisa bado yamegawanyika, ingawa, haijulikani ni kwa kiwango gani linapokuja suala la "uaskofu wa kihistoria" (maana yake maaskofu wanaobarikiwa katika uaskofu wa mnyororo kuanzia kizazi cha kwanza cha Kanisa), au uaskofu wa mnyororo wa wachungaji waliobarikiwa kama kawaida tu, kuwa ni jambo liliokusudiwa na Kristo kwa ajili ya jumuiya yake. Makanisa mengine yanaamini kuwa huduma hizi tatu, uaskofu, uzee wa kanisa, na udiakonia ni alama za uaminifu katika kuendeleza Injili na ni muhimu kwa ajili ya mwendelezo wa utume wa Kanisa kwa ujumla.[17] Kinyume chake, makanisa mengine hayaangalii imani katika Injili kama jambo linaloyafunga kuangalia kwa karibu huduma ya mnyororo, na wengine wana mashaka juu ya uaskofu wa kihistoria kwa sababu wanaona hatari yake ya kutumia vibaya mamlaka na hivyo kuhatarisha

[17] Katika hoja hii andiko la Kilutheri-Kikatoliki "Church and Justification" (1993), §185, linatamka: "Hakuna kutokukubaliana kati ya mafundisho ya kuhesabiwa haki na wazo la huduma ya kichungaji ya kubarikiwa iliyoanzishwa na Mungu na ambayo ni muhimu kwa kanisa" (*Growth in Agreement II*, 529). Hata hivyo, aya zingine baadaye kwenye andiko hilo zinaongezea: "Tofauti kati ya mawazo ya Kilutheri na ya Kikatoliki juu ya tathmini ya uaskofu kitheologia na kikanisa si ya kutisha sana kwamba katazo la Kilutheri au hata chuki dhidi ya huduma ya kikuhani iko kinyume kabisa na madai ya Kikatoliki juu ya mafunzo muhimu ya kanisa. Suala hasa la kulifanyia kazi ni kule kushusha hadhi ya huduma hii ya kichungaji, ambayo imekuwa ikielezwa kwa upande wa Wakatoliki kwa kutumia visifa kama vile 'lazima' au 'yenye ulazima', wakati kwa upande wa Walutheri imeelezwa kama 'muhimu', 'yenye maana' na hivyo 'inayotamaniwa'" §197; (*Growth in Agreement II*, 532).

ustawi wa jumuiya. Andiko la *Ubatizo, Ekaristi Takatifu, na Huduma ya Kichungaji*, kwa sehemu yake, linathibitisha kwamba vipengele hivi vitatu vya huduma "vinaweza kusaidia leo kutoa tamko la umoja tunaoutafuta na kama njia ya kuufikia umoja huo."[18]

***Vipengele Vitatu vya Huduma ya Kichungaji***

*Kutokana na viashiria vya kukua kwa makubaliano kuhusu nafasi ya uchungaji wa kubarikiwa katika Kanisa, tunaongozwa kuuliza kama makanisa yanaweza kufikia muafaka wa jinsi ipi vipengele vitatu hivi vya huduma ya kichungaji viwe sehemu ya mapenzi ya Mungu kwa ajili ya Kanisa katika kuutimiza umoja wake ambao Mungu anaupenda.*

*Mamlaka ya Karama ya Huduma ya Kichungaji*

48. Mamlaka yote ndani ya Kanisa yanatoka kwa Bwana ambaye ndiye kichwa cha Kanisa, yaani Yesu Kristo, ambaye mamlaka yake, yanayotafsiriwa na neno *exousia* katika Agano Jipya (= nguvu; mamlaka ya kuachiwa; mamlaka ya kimaadili; ushawishi; na kwa maana halisi "kutokana na utu wa mtu"), na ameyatumia mamlaka haya katika mafundisho yake (ling Mt 5:2; Lk 5:3), katika kutenda miujiza yake (ling. Mk 1:30-34; Mt 14:35-36), kutoa mapepo (ling. Mk 1:27; Lk 4:35-36), katika tendo lake la kusamehe dhambi (ling Mk 2:10; Lk 5:4) na katika kuwaongoza wanafunzi wake katika njia ya kufikia wokovu (ling. Mt 16:24). Kazi nzima ya huduma ya Yesu ilitawaliwa na mamlaka ambayo yalijikita katika kuhudumia wanadamu (Mk 1:27; Lk 4:36). Baada ya kupokea "mamlaka yote kutoka mbinguni na duniani" (Mt 28:18), Yesu aliwashirikisha mitume wake mamlaka haya (ling. Yohana 20:22). Wale waliowapokea katika huduma hii ya kiaskofu

[18] *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya Huduma, §22.

walitumia mamlaka haya katika kutangaza Injili, katika kuhudumia sakramenti, na hasa ya ekaristi takatifu, na katika kuwatunza waumini kichungaji.[19]

49. Tofauti ya asili ya mamlaka katika Kanisa inaweza kueleweka na kufanyiwa kazi kwa usahihi kama tu itatokana na tafsiri ya mamlaka ya chanzo chake, yaani Yesu ambaye alisulibiwa, ambaye "alijishusha" na kukubali hata mauti, naam mauti ya msalaba" (Filipi 2:7-8). Mamlaka haya ni lazima yaeleweke ndani ya ahadi ya Yesu Kristo ya maisha yajayo ili kuliongoza Kanisa katika utimilifu ulio katika utawala mbinguni. Hivyo, mamlaka ya Kanisa ni tofauti na mamlaka ya dunia. Wanafunzi walipofikiria kutumia mamlaka haya juu ya wengine, Yesu aliwasahihisha, akisema kuwa alikuja si kutumikiwa bali kutumika, na kuutoa uhai wake kwa ajili ya wengine (ling. Mk 10:41-45; Lk 22:25). Mamlaka ndani ya Kanisa ni lazima yaelewe kuwa ni huduma ya kujishusha, kulisha na kuujenga ushirika wa Kanisa katika imani, maisha na ushuhuda; na mfano wake uko katika tendo la Yesu la kuwaosha miguu wanafunzi wake (ling. Yohana 13:1-17). Ni huduma (ya *diakonia*) ya upendo, bila ukandamizaji wala kutumia nguvu.

50. Hivyo, mamlaka katika Kanisa katika miundo na madaraja yake mbalimbali ni lazima yatofautishwe na mamlaka ya kawaida. Mamlaka haya yanatoka kwa Mungu Baba kwa njia ya Mwana katika nguvu ya Roho Mtakatifu; kwa hiyo yanaakisi utakatifu wa Mungu. Vyanzo vya mamlaka vinavyotambuliwa na makanisa kwa viwango tofauti kama vile Maandiko

---

[19] Maelezo haya ya msingi juu ya mamlaka ya Yesu na jinsi anavyolishirikisha Kanisa yanaandika kwa upya maelezo yaliyotolewa na tamko la Kiorthodoksi-Kikatoliki (2007) kuhusu "Ecclesiological and Canonical Consequences of the Sacramental Nature of the Church: Ecclesial Communion, Conciliarity and Authority," §12, angalia juu, sura II, na. 18.

Matakatifu, Mapokeo, Ibada, Mabaraza na Sinodi, na pia yanaakisi utakatifu wa Utatu wa Mungu. Mamlaka kama hayo yanatambuliwa popote ambapo kweli inayoongoza kwenye utakatifu inahubiriwa na utakatifu wa Mungu unatangazwa "kutoka vinywa vya wana na watoto" (Ps. 8:2; ling Mt 21:16). Utakatifu maana yake hali ya ukweli wa hali ya juu katika mahusiano na Mungu, watu wengine na viumbe vyote. Katika historia wakati wote Kanisa limetambua baadhi ya mamlaka katika maisha ya watakatifu, katika maisha ya ushuhuda ya utawa na katika njia mbalimbali ambazo makundi mbalimbali ya waumini yameishi na kuieleza kweli ya injili. Kwa mfuatao huo, aina fulani ya mamlaka inaweza kutambuliwa katika mazungumzo ya kiekumene na katika matamko yaliyofikiwa makubaliano, wakati wa kutafakari kutafuta njia ya pamoja kwa ajili ya ugunduzi wa ukweli huu katika upendo (Ef. 4:15), kuwaasa waumini kutafuta mapenzi ya Bwana kwa ajili ya ushirika wa kanisa, na kualika *toba* na utakatifu katika maisha.

51. Mamlaka ambayo Yesu Kristo, ambaye ndiye kichwa cha Kanisa, anawashirikisha wale walio katika huduma ya uongozi si ya kibinafsi wala inayokabidhiwa na jumuiya. Mamlaka hii ni karama ya Roho Mtakatifu inayolenga kwa ajili ya huduma (*diakonia*) ya Kanisa katika upendo. Zoezi lake linahusisha ushiriki wa jumuiya nzima, ambayo hisia zake za kiimani (*sensus fidei*) zinachangia katika uelewa mzima wa Neno la Mungu na ambayo mapokeo ya uongozi na mafundisho toka kwa watumishi waliobarikiwa inakiri juu ya ukweli kuhusu uongozi huo. Mahusiano ya upendo na mazungumzo kati ya makanisa yanaunganisha wale wanaotekeleza mamlaka na wale walio chini ya mamlaka hiyo. Kama njia ya kuiongoza jumuiya ya Kikristo katika imani, ibada na huduma katika nguvu ya Bwana aliyesulibiwa na kufufuka, utekelezaji wa mamlaka unaweza ukaalika utii, lakini mwito kama huo una maana ya kukaribisha uhusiano wa hiari na maelewano kwa kuwa lengo

lake ni kusaidia waumini kukua katika ukamilifu wao katika Kristo (ling. Efe 4:11-16).[20] "Ufahamu" juu ya maana ya kweli ya Injili kwamba inashirikisha watu wote wa Mungu, mawazo ya wale waliojitolea kwa njia ya pekee katika mafunzo ya Biblia na Theologia, na uongozi wa wale ambao wamewekwa wakfu kipekee kwa ajili ya huduma ya kiaskofu, wote wanahusiana katika utambuzi wa mapenzi ya Mungu kwa ajili ya jumuiya. Uamuzi katika Kanisa unatafuta na kushawishi mwafaka kati ya wote na unategemea uongozi wa Roho Mtakatifu, ukitambuliwa kwa njia ya usikivu ulio makini wa Neno la Mungu na kila mtu. Kwa njia ya mchakato huu wa makini katika kupokea, kadri muda unavyopita, Roho Mtakatifu anarekebisha utata unaoweza kujitokeza katika maamuzi. Harakati za kiekumene zimewezesha mafundisho yenye mamlaka kwa baadhi ya viongozi wa Kikristo kuwa na ufanisi nje ya mipaka ya jumuiya zao za nyumbani, hata wakati huu wa hali ya migawanyiko. Kwa mfano uongozi wa Askofu Mkuu Desmond Tutu kutangaza vita dhidi ya "ubaguzi wa rangi uli[o]kuwa na nguvu kubwa kiasi cha kulilemea Kanisa lililokuwa limegawanyika,"[21] juhudu za kiongozi wa Kiekumene Baba wa Kiroho Bartholomeo katika kuunganisha viongozi wa Kikristo katika suala la mazingira, juhudi za Papa Yohane Paulo II na Benedikti wa XVI kuwaalika Wakristo na viongozi kutoka imani zingine ili kuungana pamoja kwa maombi katika kutetea amani, na ushawishi wa Kaka Roger Schutz aliyewaamsha waumini wengi wa Kikristo wasiohesabika, hasa vijana, kuungana pamoja katika ibada ya kutukuza Utatu wa Mungu.

---

[20] Ling. "Ecclesiological and Canonical Consequences of the Sacramental Nature of the Church: Ecclesial Communion, Conciliarity and Authority," §13-14; angalia pia sura II, na. 18.

[21] Desmond Tutu, "Towards *Koinonia* in Faith, Life and Witness," katika kitabu cha T. Best and G. Gassmann (wahariri.), *On the Way to Fuller Koinonia*, Geneva, WCC, 1994, 96-97.

***Mamlaka ndani ya Kanisa na Utekelezaji Wake***

*Hatua muhimu zimerejewa kuelekea makubaliano kuhusu mamlaka na utekelezaji wake katika mazungumzo mengi ya makanisa katika maeneo yao.*[22] *Tofauti zimeendelea ndani ya makanisa, hata hivyo, zimeangaliwa kwa ujumla wake kwa uzito unaoonyeshwa kulingana na vyanzo tofauti vya mamlaka, kwa kuona ni kwa kiwango gani na kwa kiasi gani Kanisa lina njia ya kufikia maelezo ya msingi juu ya imani yake, na kwa njia ya kuangalia wajibu wa wachungaji waliobarikiwa katika kutoa tafsiri yenye mamlaka yenye ufunuo. Bado hata hivyo makanisa yote yanashiriki kuhusu mashaka juu ya umuhimu wa Injili kuhubiriwa, kutafsiriwa na kuwafanya watu waiishi Injili hiyo kwa unyenyekevu katika ulimwengu huu wa sasa wakisukumwa na mamlaka ya Injili hiyo. Je haiwezekani kwa jinsi muafaka wa kiekumene unavyotafutwa kuhusiana na jinsi mamlaka ya Injili inavyotambuliwa na kutekelezwa navyo vikachangia katika kuleta uwajibikaji wenye ubunifu kwenye kuleta msukumu wa kazi ya misheni ya makanisa?*

*Huduma ya Uaskofu*

52. Kanisa kama mwili wa Kristo na kama watu wa Mungu wanaotarajia maisha yajayo, limejengwa na Roho Mtakatifu kwa njia ya karama au huduma mbalimbali. Tofauti hizi zinaalika uratibishaji wa huduma ili karama hizi ziweze kuimarisha Kanisa zima, umoja na misheni yake.[23] Uaminifu katika kutekeleza huduma ya kiaskofu iliyo chini ya Injili na

---

[22] Angalia, kwa mfano, ripoti za Kianglikana-Kikatoliki "Authority in the Church," 1976 katika *Growth in Agreement I*, 106-18; "The Gift of Authority," 1998, katika *Growth in Agreement III*, 60-81; hii pia inaakisiwa katika §§83-84 kwenye andiko la Kimethodisti-Kikatoliki "Speaking the Truth in Love: Teaching Authority among Catholics and Methodists," katika *Growth in Agreement III*, 163-164.

[23] Ling. *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya Huduma, §23.

watu walioteuliwa na kutengwa kwa ajili ya huduma kama hiyo ni hitaji lenye umuhimu wa msingi kwa ajili ya maisha ya Kanisa na misheni yake. Uendelezaji wa kipekee wa mifumo ya uaskofu imetofautiana katika nyakati tofauti na mahali; lakini jumuiya zote, ziwe zinafuata utaratibu wa uaskofu au la, zimeendelea kuona umuhimu wa huduma ya uaskofu. Katika kila hitaji, uaskofu upo kwa ajili ya huduma ya kuimarisha mwendelezo wa imani ya kimitume na maisha ya umoja. Pamoja na nyongeza ya kuhubiri Neno la Mungu na kushirikisha sakramenti, lengo kubwa la huduma ya kichungaji ni kuhakikisha kwa uaminifu kabisa kuwa kweli iliyodhihirishwa inalindwa na kurithishwa, kuziunganisha sharika katika jumuiya, kuleta ushirikiano wa pamoja, na kuongoza [jumuiya] katika kuishuhudia Injili. Uongozi huo unahusisha uangalizi wa mpangilio wa huduma mbalimbali za Kikristo zinazokusudia kuboresha maisha ya watu na kuwapunguzia watu mateso, na pia unahusisha mambo ya huduma (diakonia) ya Kanisa duniani, jambo ambalo tutalirudia baadaye kwenye sura inayofuata. Kazi zote hizi, zinazojumuishwa na neno uaskofu au uangalizi, zinatekelezwa na watu wanaohusiana na waumini wao wa jumuiya zao na kwa wale wanaotekeleza huduma hizo katika jumuiya zao za maeneo yao. Hii ndio maana ya kuthibitisha kuwa huduma ya uangalizi, kama zilivyo huduma zingine katika Kanisa, inahitaji kutekelezwa kwa njia ya mtu, watu na au jumuiya nzima.[24] Njia

---

[24] Tayari katika mkutano wa kwanza wa dunia juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada mnamo mwaka 1927 pale Lausanne, ulionyesha kuyapanga makanisa katika utaratibu wa "uaskofu," "uzee wa kanisa" na "kisharika" na misingi chini ya mifumo hii mitatu "inaaminiwa na wengi kuwa muhimu katika utaratibu wa Kanisa." Kwenye chapisho la H. N. Bate (mhariri.), *Faith and Order Proceedings of the World Conference: Lausanne, August 3-21, 1927*, London, Student Christian Movement, 1927, 379. Baada ya miaka hamsini na tano, andiko la *Baptism, Eucharist and Ministry*, katika sehemu ya Huduma, ufafanuzi wake §26, unanukuu andiko hili la Lausanne kuhalalisha

hizi za utekelezaji zimeelezwa kinagaubaga katika andiko la *Ubatizo, Ekaristi Takatifu, na Huduma* kama ifuatavyo: "[Huduma hii] ni lazima imhusishe mtu kwa sababu uwepo wa Kristo kati ya watu wake unaweza ukaonyeshwa kwa ufasaha na mtu aliyebarikiwa kutangaza Injili na kuiita jumuiya ili kumtumikia Bwana katika maisha ya umoja na ushuhuda. Ni lazima iwe ya watu, kwa kuwa kuna haja ya chuo cha wale waliobarikiwa kuwa wachungaji kushirikiana katika jukumu la pamoja la kutatua matatizo ya jumuiya. Na mwisho, uhusiano wa karibu sana kati ya wachungaji na jumuiya unatakiwa upate kibali kutoka katika kipenyo cha jumuiya ambako utekelezaji wa kichungaji una mizizi yake katika maisha ya jumuiya na unahitaji ushiriki wenye ufanisi wa jumuiya katika kuvumbua mapenzi ya Mungu na uongozi wa Roho Mtakatifu."[25]

53. Mojawapo ya zoezi hili la uangalizi linatafsiri kuwa tabia ya ubora wa Kanisa inayoweza ikaitwa "shughuli za kisinodi" au "shughuli za baraza." Neno *synod* linatokana na maneno ya Kiyunani *syn* (pamoja) na *odos* (njia) yakimaanisha "kutembea pamoja." Maneno yote haya, "shughuli za kisinodi" na "shughuli za baraza," yanaonyesha kuwa "kila mshiriki wa Mwili wa Kristo, kwa njia ya ubatizo, ana nafasi na wajibu muhimu" katika jumuiya ya kanisa.[26] Chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, Kanisa zima linatembea pamoja (*synodal/conciliar*), katika ngazi zote za maisha ya kanisa: nyumbani, kikanda na duniani kote. Ubora wa kutembea pamoja unaakisi siri ya maisha ya Utatu wa Mungu, na

---

uthibitisho wake kuwa uchungaji unatakiwa utekelezwe kwa njia ya mtu, watu na jamuiya.

[25] *Baptism, Eucharist and Ministry*, sehemu ya "Ministry," §26.

[26] Angalia Mazungumzo ya Kiorthodoksi-Kikatoliki katika ngazi ya kimataifa, "Ecclesial Communion, Conciliarity and Authority," §5, yanayoonyesha kuwa "shughuli za kisinodi" zinaweza kuchukuliwa kuwa sawa na "shughuli za baraza."

mifumo ya Kanisa inaueleza ubora huu ili kuutimiza katika maisha ya jumuiya katika ushirika. Katika jumuiya ya nyumbani kwa njia ya ekaristi takatifu, ubora huu unaonekana katika umoja wa ndani sana unaojali upendo na kweli kati ya washiriki na wale wachungaji wanaowaongoza. Inapotokea hali tete sinodi zimekutana ili kutafakari kwa pamoja imani ya mitume ili kujibu athari za mafundisho na maadili potofu au uzushi, zikiamini katika uongozi wa Roho Mtakatifu, aliyeahidiwa kutumwa na Yesu baada ya yeye kurudi kwa Baba (ling. Yohana 16:7.12-14). Mikutano ya Sinodi ya Kiekumene imeshuhudia ushiriki wa viongozi kutoka Kanisa zima; maamuzi yao yalipokelewa kama ishara ya kutambua umuhimu wa huduma waliyoitoa katika kuendeleza na kuimarisha ushirika kwa Kanisa zima.[27] Makanisa kwa sasa yana mitizamo na vitendo tofauti juu ya ushiriki wa wakristo wasio wachungaji/maaskofu katika sinodi.

***Mamlaka ya Mabaraza ya Kiekumene***

*Wakati makanisa mengi yanakubaliana na tafsiri za mafundisho ya mabaraza ya kwanza kama maelezo ya mafundisho ya Agano Jipya, wengine wanashikilia kwamba maamuzi yoyote yaliyotokea*

[27] Baraza au sinodi ya "kiekumene" inaweza kuwa mojawapo inayowakilisha Wakristo wote duniani. Mojawapo ya baraza kama hili linalojulikana katika dunia nzima ni lile lililokutana Nikea mnamo mwaka wa 325 kuthibitisha uungu wa Kristo katika kujibu mafundisho mapya ya Arius, yaliyokataa usawa wa Mwana na Baba. Makanisa yanatofautiana juu ya idadi ya mabaraza yaliyowahi kukutana. Kuhusu mabaraza ya kiekumene na mamlaka yake, angali kwa mfano, andiko la Kilutheri-Kiorthodoksi "Authority in and of the Church: The Ecumenical Councils" (1993), katika *Growth in Agreement III*, 12-14; sehemu ya kipengele cha "Councils and the Declaration of the Faith" cha Kanisa la Kiufuasi-Wakatoliki, "Receiving and Handing on the Faith: The Mission and Responsibility of the Church," katika *Growth in Agreement II*, 125-127; ling. pia *Councils and the Ecumenical Movement*, Geneva, WCC, 1968.

*baadaye nje ya Biblia ni lazima yawe tayari kwa ajili ya marekebisho, wakati wengine wanafikiri kwamba mafundisho mengine ni kama kanuni na hivyo ni maelezo yasiyobadilika ya imani. Je mazungumzo ya kiekumene yamejaribu kufanya tathmini ya pamoja juu ubora wa kanuni za mafundisho haya ya mabaraza ya kwanza ya kiekumene?*

54. Mara Kanisa linapokutana kwa ajili ya kushauri na kufanya maamuzi muhimu, kuna haja ya kuwepo mtu kwa ajili ya kuitisha na kuongoza mikusanyiko hii kwa ajili ya kutunza utaratibu na kusadia mchakato wa kukuza, kutafsiri na kuweka bayana muafaka unaofikiwa. Wale wanaoongoza mikutano hii ni lazima wawe katika huduma ya watu ambao wanawaongoza kwa ajili ya kulijenga Kanisa la Mungu, kwa upendo na imani. Ni jukumu la wale wanaoongoza kuheshimu utu wa makanisa ya maeneo, kuwasemea wale wasio na sauti na kutunza umoja licha ya tofauti zilizopo.

55. Neno *ukuu*, kuhusu utamaduni wake na matumizi yalitambuliwa tayari na mabaraza ya kiekumene ya kwanza kwenye ibada za kale, ambapo maaskofu wa Alexandria, Rumi na Antiokia, na baadaye Yerusalemu na Konstantinopoli, walitekeleza huduma ya mtu mmoja mmoja ya kuangalia kazi ya eneo katika upana wake ambapo huduma hizo zilikuwa nyingi kuliko kazi ya kanisa katika majimbo yake. Uangalizi kama huo wa kiaskofu haukuonekana kupingana na majukumu ya sinodi au baraza yanayoelezea zaidi huduma za pamoja kwa ajili ya umoja. Katika historia, mifumo ya kiaskofu imekuwepo katika ngazi mbalimbali. Kutokana na sheria ya 34 ya Sheria za Mitume, ambayo inajieleza jinsi Kanisa lilivyojielewa lenyewe katika karne zake za kwanza na bado inashikiliwa na wengi kwa ajili ya heshima hiyo, ingawa si wote, Wakristo wa leo, wa kwanza kati ya maaskofu katika kila taifa anaweza kufanya jambo kwa kukubaliana na maaskofu wengine

na wa mwisho hatafanya uamuzi wowote muhimu bila kukubaliana na wa kwanza.[28] Hata katika karne za kwanza, huduma nyingi za kiaskofu zilikumbwa wakati mwingine na mashindano miongoni mwa viongozi wa Kanisa. Uwezo wa kiaskofu wa kuamua na mamlaka ya kufundisha, yaliyowafikia watu wote wa Mungu, taratibu yaliwekwa chini ya mamlaka ya Askofu wa Rumi kwa misingi ya uhusiano wa kanisa la eneo fulani na mitume kama Petro na Paulo. Licha ya kutambuliwa na makanisa mengine katika karne za kwanza, umuhimu katika wajibu wake (askofu) na jinsi ofisi hii ilivyofanya kazi ilileta utata mkubwa. Katika miaka ya karibuni, harakati za kiekumene zimesaidia kuleta mazingira mazuri ya upatanisho ambapo uongozi katika huduma kuelekea umoja wa Kanisa zima vimejadiliwa.

56. Kutokana na hatua zilizofikiwa kwa sehemu tayari katika mazungumzo ya kikanda na kimataifa, Mkutano wa Tano wa Dunia Kuhusu Imani na Utaratibu wa Ibada uliuliza swali "kuhusu huduma ya watu wote ya umoja wa Kikristo."[29] Katika waraka wake *Ut Unum Sint*, Papa Yohane Paulo wa II ananukuu andiko hili anapowaalika viongozi wa Kanisa na watheologia wao "kuingia katika mazungumzo ya uvumilivu na kindugu" na yeye kuhusu huduma hii.[30] Katika mjadala

---

[28] Angalia tovuti ya http://www.newadvent.org/fathers/3820htm.

[29] §31.2 ya "Report of Section II: Confessing the One Faith to God's Glory," katika T. F. Best na G. Gassman (wahariri.), *On the Way to Fuller Koinoia*, Geneva, WCC, 1994, 243.

[30] John Paul II, *Ut Unum Sint*, London, Catholic Truth Society, 1995, §96. Ripoti iliyoitwa "Petrine Ministry" inaweka majumuisho ya hoja na uchambuzi wa mazungumzo mbalimbali ya kiekumene ambayo mpaka kufikia 2001, yalikuwa yamechukua suala la uongozi wa uaskofu, na pia majibu yaliyotolewa kwenye mwaliko wa mazunguzo na Yohane Paulo II kuhusu uongozi huu. Iliweka mambo makubwa katika vichwa vinne: misingi ya kibiblia, *Dei iure divino* [kama uongozi kama huo unaweza kutokana na mapenzi ya Mungu], mamlaka ya watu wote (utekelezaji wa mamlaka au

unaofuata, licha ya kuendelea kwa tofauti katika maeneo mengi, baadhi ya wajumbe wa makanisa mengine wameonyesha kuwa wazi kuhusu jinsi huduma inavyoweza kuchochea umoja wa makanisa ya maeneo duniani kote na kukuza na sio kuhatarisha kuwa na vipengele tofauti vya ushuhuda katika makanisa yao. Kutokana na unyeti wa kiekumene wa jambo hili, ni vizuri kutofautisha kati ya maana ya huduma ya kiaskofu na njia zozote za kipekee ambazo zinaonyesha jinsi huduma hii kwa sasa imekuwa ikitekelezwa. Wote watakubaliana kuwa kazi yoyote ya huduma ya mtu ya kiaskofu inahitaji kufanywa katika jumuiya na kwa njia ya ushirikiano na wengine.

57. Bado kuna kazi kubwa inayotakiwa kufanyika ili kufikia mwafaka katika jambo hili. Kwa wakati huu bado Wakristo hawakubaliani kwamba huduma ya kiaskofu ya watu wote ni muhimu au hata kutamaniwa, ingawa mazungumzo mengi katika kanda yametambua thamani ya uongozi katika huduma hii ili kuunganisha jumuiya nzima ya Kikristo au hata kuona kwamba huduma hiyo inaweza kuhusishwa na mapenzi ya Kristo kwa ajili ya Kanisa lake.[31] Kukosekana kwa muafaka si tu ni kati ya makanisa fulani, bali hali hii ipo pia ndani ya baadhi ya makanisa yenyewe. Kumekuwa na mazungumzo muhimu ya kiekumene yakileta ushahidi kutoka Agano Jipya kuhusu uongozi wa kuhudumia umoja mpana wa Kanisa, kama vile uongozi wa Mtakatifu Petro na Mtakatifu Paulo. Hata

---

nguvu ndani ya Kanisa), na papa kutokosea. Ripoti hii ya mwanzo inaweza kupatikana katika *Information Service*, N. 109 (2002/I-II), 29-42, na inaonyesha kwamba tathmini ya "uongozi wa ki-Petro" unatofautiana kabisa kulingana na baadhi ya mapokeo ambapo jumuiya hiyo ya Kikristo inahusika.

[31] Angalia ripoti ya Kianglikana-Kikatoliki "The Gift of Authority," katika *Growth in Agreement III*, 60-81, na Kiorthodoksi-Kikatoliki, "The Ecclesiological and Canonical Consequences of the Sacramental Nature of the Church."

hivyo, tofauti zinabaki juu ya umuhimu wa huduma zao na maana inayoweza kuambatana nazo kuhusu uwezekano wa kusudi la Mungu kwa ajili ya aina fulani ya uongozi katika huduma kwa ajili ya umoja na misheni ya Kanisa lake kwa ujumla.

### *Uongozi unaoshirikisha watu wote kwa ajili ya umoja*

*Kama, kwa kufuata mapenzi ya Kristo, migawanyiko ya sasa itaondolewa, ni kwa jinsi gani uongozi wa Kanisa utaendeleza na kuhamasisha umoja wa Kanisa katika ngazi ya dunia nzima ili ueleweke na kutekelezwa?*

## Sura ya IV

## Kanisa: Duniani na kwa ajili ya Dunia

### A. Mpango wa Mungu kwa ajili ya Uumbaji: Ufalme

58. Sababu ya misheni ya Yesu imeelezwa kinagaubaga katika maneno haya, "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwana wake wa pekee" (Yohana 3:16). Hivyo tabia ya Mungu ya kwanza na inayotangulia kuhusiana na ulimwengu ni upendo, kwa ajili ya mtoto, mwanamke na mwanaume ambaye ametokea kuwa sehemu ya historia ya mwanadamu, na hasa upendo kwa uumbaji mzima. Ufalme wa Mungu uliodhihirishwa kwa njia ya mahubiri ya Yesu kwa njia ya mifano na kuwekwa wakfu kwa njia ya matendo yake makuu, hasa kwa njia ya fumbo la pasaka kwa njia ya kifo na kufufuka kwake, ndio hitimisho la mwisho la ulimwengu wote. Kanisa lililokusudiwa na Mungu si kwa ajili yake lenyewe, bali kwa ajili ya kutumikia mpango wa Mungu wa kuibadilisha dunia. Hivyo, huduma za diakonia zinamilikiwa na uwepo hasa wa Kanisa lenyewe. Andiko la kitafiti juu ya *Kanisa na Dunia* linaelezea huduma hizo kama ifuatavyo: "Kanisa kama mwili wa Kristo linashiriki katika fumbo la uungu wa Mungu. Kama fumbo, Kanisa linamdhihirisha Kristo duniani kwa njia ya kutangaza injili, kusherehekea sakramenti (ambazo hata zenyewe ni fumbo la imani), na kwa kuonyesha upya wa maisha uliotolewa na Bwana, kwa hivyo kuutarajia ufalme wa Mungu ambao upo ndani yake hata sasa."[1]

59. Kusudi kubwa la Kanisa duniani ni kuwatangazia watu wote kwa maneno na matendo habari njema ya wokovu katika Kristo Yesu (ling Mk 16:15). Kazi ya uinjilisti ndio

---

[1] *Church and World: The Unity of the Church and the Renewal of Human Community*, Geneva, WCC, 1990, Sura ya III, §21, ukurasa wa 27.

jukumu linalotangulia majukumu yote ya Kanisa katika kutii amri ya utume wa Yesu (ling. Mat 28:18-20). Kanisa limeitwa na Kristo kwa njia ya Roho Mtakatifu kushuhudia upatanisho wa Baba, uponyaji na mabadiliko ya uumbaji. Hivyo jambo la kikatiba la kazi ya uinjilisti ni kukuza haki na amani.

60. Leo hii Wakristo wanauelewa upana wa dini zingine dhini yao na maudhui yake yenye ukweli fulani na maadili yake.[2] Hii inawawezesha Wakristo kurejea nyuma na kuvitaja vifungu vya injili ambavyo Yesu mwenyewe alikuwa na mtizamo chanya kuhusu wageni na watu wengine kuhusiana na kundi walilomsikiliza (ling Mat 8:11-12; Luka 7:9; 13:28-30). Wakristo wanatambua uhuru wa kuabudu kama moja ya mihimili ya msingi ya utu wa binadamu na jambo lililowekwa kwa upendo na Kristo mwenyewe, wanahitaji kuheshimu utu huo na kuwa na mazungumzo na wengine, si tu kushirikisha wengine utajiri ulio katika imani ya Kikristo, bali pia kuheshimu aina yoyote ya ukweli na uzuri uliopo katika dini zingine. Wakati uliopita, yaani wakati uliokuwa wa kutangaza Injili kwa watu ambao hawakuwa wameisikia kwanza, dini zao hazikupewa heshima iliyostahili. Uinjilisti ni lazima uheshimu watu wa imani zingine. Kushirikisha habari njema ya ukweli

---

[2] Kuhusu maswali yanayohusiana na mada hii, angalia "Religious Plurality and Christian Self-Understanding" (2006), matokeo ya mchakato wa utafiti kuhusiana na kujibu mapendekezo yaliyotolewa mwaka 2002 na kamati kuu ya BMD kwa watendaji watatu wa timu juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada, Mahusiano ya Dini Mbalimbali, na Misheni na Uinjilisti inayopatikana http://www.oikoumene.org/en/resources/documents/assembly/porto-alergre-2006/3-preparatory-and-background-documents/religious-plurality-and-christian-self-understanding.html. Tamko hili linafuatia mazungumzo ya uhusiano kati ya misheni na dini nyingine duniani katika kongamano la Utume kuhusu Misheni ya Ulimwengu na Uinjilisti lililofanyika San Antonio mwaka 1989. Kutokana na umuhimu wake kwa mada mbalimbali zilizopo katika sura hii, kutajwa kwa baadhi ya mahusiano ya kidini kutajitokeza katika sehemu zote tatu za sura hii.

uliofunuliwa katika Agano Jipya na kuwaalika wengine kwenye utimilifu wa maisha katika Kristo ni kielelezo cha upendo wenye kuheshimu.[3] Katika muktadha wa sasa ambapo uelewa kuhusu dini nyingine umeongezeka, uwezekano wa wokovu kwa wale wasioamini hasa katika Kristo na uhusiano kwa njia ya mazungumzo ya kidini na kumtangaza Yesu kuwa ni Bwana vimeendelea kuwa mada za kutafakari na kujadiliana miongoni mwa Wakristo.

### *Jibu la Kiekumene kuhusu Uwingi wa Dini*

*Kuna kutokukubaliana kwingi ndani na kati ya makanisa kuhusu mambo haya. Agano Jipya linatufundisha kuwa Mungu anapenda watu wote wapate wokovu (ling Tim 2:4) na wakati huo huo anatufundisha kuwa Yesu ndiye pekee Mwokozi wa ulimwengu (ling 1 Tim 2:5 na Mdo 4:12). Hitimisho gani linaweza kupatikana kuhusu mafundisho ya kibiblia juu ya uwezekano wa wokovu kwa wale wasiomwamini Kristo? Wengine bado wanashikilia kwamba, kwa njia zijulikanazo na Mungu, kwa njia ya nguvu ya Roho Mtakatifu inawezekana kuwa wale wasioshiriki kabisa imani katika Kristo, wanaweza kupata wokovu. Wengine wanaona jinsi msimamo huo usivyokidhi vipengele vya kibiblia vinavyoona ulazima wa imani*

---

[3] "Charta Oecumenica" (2001) ya Kongamano la Makanisa ya Ulaya (CEC) na Makongamano ya Baraza la Kiekiskopali ya Ulaya (CCEE), §2, linaelezea: "tunaahidi kutambua kuwa kila mtu anaweza kwa uhuru alio nao kuchagua dini na dhehebu kama utashi wake unavyomtuma, hivyo hii ina maana hakuna kumlazimisha mtu kugeukia dini nyingine kwa njia ya shinikizo la kimaadili au kivutio cha mali, lakini pia kutozuia mtu kugeukia dini nyingine kwa hiari na uhuru wake mwenyewe. Angalia pia "Christian Witness in a Multi-Religious World: Recommendations for Conduct" na mapendekezo ya Baraza la Kipapa juu ya Mazungumzo na Dini Zingine, Baraza la Makanisa Duniani na Baraza la Umoja wa Kiinjilisti, yaliyoidhinishwa tare 28 Januari 2011, na yanapatikana katika tovuti hii http://www.vatican.va/roman_curia/pontifical_councils/interelg/documents/rc_pcinterelg_doc_20111110_testimonianza-cristiana_en.html.

*na ubatizo kwa ajili ya wokovu. Tofauti hizi katika swali hili zinaweza kuwa na matokeo [hasi au chanya] juu ya namna mtu anavyoelewa au kuweka katika vitendo misheni ya Kanisa. Katika mazingira ya leo yenye kuongezeka kwa uelewa wa uwepo wa dini mbalimbali duniani kote, ni makanisa mangapi yamefikia mwafaka kuhusu mambo haya na je yanashirikiana kwa ufanisi katika kuishuhudia Injili katika neno na tendo?*

**B. Changamoto ya Kimaadili ya Injili**

61. Wakristo wameitwa kutubu dhambi zao, kusamehe wengine na kujitolea kwa ajili ya huduma: ufuasi unadai kujitolea kuishi maisha ya uadilifu. Hata hivyo Mt. Paulo anafundisha kwa msisitizo kuwa wanadamu wanahesabiwa haki si kwa matendo ya sheria bali kwa neema kwa njia ya imani (Rum 3:21-26; Gal 2:19-21). Kwa hiyo jumuiya ya Kikristo inaishi katika upeo wa msamaha wa neema ya Mungu, inayotaka na kubadili maadili ya waumini. Ni muhimu katika kufufua tena umoja wa jumuiya hizi mbili ambazo kutengana kwake kulisababisha mwanzo wa matengenezo ya Kiprotestanti zifikie mwafaka juu ya mawazo muhimu ya mafundisho ya kuhesabiwa haki kwa imani, jambo kubwa ambalo ndilo lililosababisha kutokuafikiana wakati wa mpasuko.[4] Ni kwa msingi wa imani na neema kwamba kujihusisha kimaadili na tendo la pamoja vinawezekana na mambo hayo kuthibitishwa kuwa ni sehemu ya asili ya kuwepo maisha na uwepo wa Kanisa.

62. Maadili ya Wakristo kama wafuasi yana mizizi yake kutoka kwa Mungu, Muumbaji na Mfunuaji, na yanabadilika wakati jumuiya inapotafuta kuyaelewa mapenzi ya Mungu katika matukio tofauti. Kanisa halijitengi na mapambano ya

---

[4] Angalia andiko la Kilutheri-Kikatoliki *Joint Declaration on the Doctrine of Justification*, Grand Rapids, Eerdmans, 2000.

kimaadili ya mwanadamu. Kwa kushirikiana na waumini wa dini zingine na watu wenye mapenzi mema, Wakristo lazima wahamasishe si tu maadili ya mtu binafsi ambayo ni muhumu kwa ajili ya kuukamilisha utu wa mtu bali pia wahamisishe maadili ya kijamii ya haki, amani na ulinzi wa mazingira, kwa kuwa ujumbe wa Injili unamfikia mtu na mambo yake yahusuyo jumuiya inayomuwezesha kuishi. Hivyo *ushirika* hauhusishi tu ukiri wa imani moja na ibada moja, bali inahusu pia ushirikiano wa kimaadili, unaotokana na mvuto na maono ya Injili. Bila kujali hali ya mpasuko uliopo sasa, makanisa bado yameshirikiana na yanaelewa kuwa chochote yanachofanya kina madhara pia katika maisha ya wengine, na kwa sababu hiyo, hali ya kuwajibika kwa wengine imeongezeka ikizingatia mawazo na maamuzi ya kimaadili ya makanisa husika. Makanisa yanapojihusisha na maswali haya na ukiri wa pamoja, yanaonyesha ushirikiano zaidi kati yao uliojengwa katika Kristo.

63. Wakati misuguano juu ya mambo ya kimaadili yameleta wasiwasi ndani ya Kanisa mara zote, katika dunia ya leo maendeleo ya kifalsafa, kijamii na kitamaduni yamepelekea kufikiria upya juu ya kanuni nyingi za kimaadili, zinazosabisha migongano juu ya misingi ya kimaadili na maswali yake yanayohatarisha umoja wa makanisa. Wakati huo huo, maswali ya kimaadili yanahusiana na anthropologia ya Kikristo, na kipaumbele chake kinatokana na Injili kama kipimo cha kuangalia maendeleo katika kufikiri juu ya maadili hayo. Wakristo mmoja mmoja na makanisa wakati mwingine hugawanyika kutetea maoni pingamizi kuhusu hasa misingi ya maadili ya mtu au kikundi kwa kufuata muafaka wa Injili ya Yesu Kristo. Zaidi sana, wengine huamini kwamba maswali ya kimaadili si ya kuasilisha "mgawanyiko ndani ya kanisa," na wengine hufikiri kuwa maswali haya ni ya kweli na yanaligawanya kanisa.

***Maswali ya kimaadili na umoja wa Kanisa***

*Mazungumzo ya kiekumene katika ngazi ya kimataifa na kikanda yameanza kuweka wazi baadhi ya vigezo juu ya umuhimu wa mafundisho ya kimaadili na utendaji wake kwa ajili ya umoja wa Kikristo.*[5] *Kama mazungumzo ya sasa na ya baadaye ya kiekumene yatatakiwa kuimarisha misheni na umoja wa Kanisa, ni muhimu mazungumzo haya yakashughulikia kwa uwazi changamoto ya kukutana kunakowakilishwa na mambo ya sasa ya kimaadili. Tunayaalika makanisa kutafiti juu ya mambo haya katika roho ya kusikilizana na kusaidiana. Ni kwa jinsi gani makanisa, yakiongozwa na Roho Mtakatifu, yatatafakari kwa pamoja nini maana ya leo katika kuelewa na kuishi kwa uaminifu katika mafundisho na tabia ya Yesu? Ni kwa jinsi gani makanisa, yanapojishughulisha kwa pamoja katika jukumu hili la kutafakari, yanaweza kutoa mifano sahihi ya mihadhara na mashauri ya hekima kwa jamii ambazo yanazitumikia?*

## C. Kanisa katika Jamii

64. Dunia ambayo "Mungu aliipenda" inagutushwa na matatizo na majanga na inalia kwa ajili ya kutaka Wakristo wajishughulishe na matendo ya huruma. Chanzo cha uchu wao wa mabadiliko chanya ya dunia kinatokana na ushirika wao na Mungu katika Kristo Yesu. Wanaamini kuwa Mungu, ambaye ndiye mwenye upendo kamili, huruma na haki, anaweza kutenda kwa kutumia wao, kwa njia ya Roho Mtakatifu. Wanaishi kama wafuasi wa Kristo aliyemjali kipofu, mlemavu

[5] Kwa mfano, tamko la Kianglikana-Kikatoliki "Life in Christ: Morals, Communion and the Church," katika *Growth in Agreement II*, 344-370; na andiko la Kikosi Kazi cha Baraza la Makanisa Duniani na Kanisa Katoliki, "The Ecumenical Dialogue on Moral Issues: Potential Sources of Common Witness or of Divisions" (1995), katika *The Ecumenical Review* 48 (2), April 1996, 143-154. Kwa kazi za karibuni "Moral Discernment in the Churches" angalia andiko la Faith and Order 215, WCC, Geneva, 2013.

wa miguu na mwenye ukoma, aliyekaribisha maskini na waliotengwa na jamii, na aliyepingana na mamlaka yaliyoonyesha kutoheshimu utu wa mtu au mapenzi ya Mungu. Kanisa linahitaji kuwasaidia wanyonge katika jamii ili wasikike; kuna wakati linatakiwa liwe sauti ya wasio na sauti. Kwa sababu ya imani yenye usahihi, jamii za Kikristo haziwezi zikasimama zikiangalia tu yanapotokea majanga ya asili yanayoweza kuwaathiri wanadamu wenzao au tishio la afya kama vile UKIMWI. Imani pia inawasukuma kufanya kazi kwa ajili ya utawala wa haki katika jamii, ambamo mema ya nchi yanaweza kugawanywa kwa usawa, mateso ya maskini yakapunguzwa na ufukara wote siku moja ukaondolewa kabisa. Kuwa na toafauti za kiuchumi zilizokithiri ni hali inayotishia maisha ya familia ya wanadamu, kama vile hali inayotofautisha kati ya dunia ya Kaskazini na ya Kusini ni jambo la kushughulikiwa na makanisa yote katika nyakati zetu za sasa. Kama wafuasi wa "Mfalme wa Amani," Wakristo wanatetea amani, hasa kwa kutafuta kukabiliana na vyanzo vya vita (na hasa vile vya msingi kama uonevu wa kiuchumi, ubaguzi wa rangi, chuki za kikabila na kidini, utaifa uliokithiri, ukandamizaji na matumizi ya nguvu katika kutatua migogoro). Yesu anasema alikuja ili watu wawe na uzima kisha wawe nao tele (ling. Yohana 10:10); wafuasi wake wanatambua wajibu wao wa kulinda maisha ya mwanadamu na utu wake. Haya ni madai kwa makanisa na kwa kila muumini. Kila muktadha unatoa vidokezo vyake kwa ajili ya kupambanua njia sahihi ya Kikristo ya kutoa majibu katika maeneo mbalimbali. Hata sasa, jumuiya nyingi za Kikristo zilizogawanyika zinaendelea na kupambanua kwa pamoja na kuwa na kazi za pamoja ili kuleta unafuu kwa watu wanaoteseka na kusaidia kujenga jamii inayojali utu wa mwanadamu.[6] Wakristo wanatafuta kuendeleza maadili

[6] Angalia, kwa mfano, andiko la Kanisa la Matengenezo-Kanisa Katoliki "The Church as Community of Common Witness to the Kingdom of God,"

yanayohusiana na ufalme wa Mungu kwa njia ya kufanya kazi kwa pamoja na wafuasi wa dini zingine na hata wale wasio na imani za kidini.

65. Sababu nyingi za kihistoria, kitamaduni, na makundi ya watu zinaweka masharti ya mahusiano kati ya Kanisa na nchi, na kati ya Kanisa na jamii. Mifano mingi ya mahusiano haya kwa kufuata mahitaji ya mazingira yanaweza kuwa vielelezo halali vya kazi ya Kanisa katika dunia nzima. Katika hali ya jumla ni sawa kwa waumini kushiriki katika mambo yahusuyo haki za kuwa raia. Hata hivyo, Wakristo wamegongana na mamlaka za nchi katika njia ambayo imebariki au kupalilia zaidi matendo ya dhambi na uonevu. Wito wa wazi wa Yesu kwa wanafunzi wake kuwa "chumvi ya dunia" na kuwa "nuru ya ulimwengu" (ling. Math 5:13-16) imewaonyesha Wakristo njia ya kujihusisha na mamlaka za kisiasa na kiuchumi ili kuendeleza maadili ya ufalme wa Mungu, na kupinga sera na mipango inayoenda kinyume na maadili hayo. Hii inahusisha uchambuzi yakinifu na uwekaji wazi wa mifumo onevu, na kupigania mabadiliko, lakini pia kusaidia uendelezaji wa mipango ya mamlaka za kiraia zinazokuza haki, amani, utunzaji wa mazingira na uwezeshaji wa maskini na wanaokandamizwa. Kwa njia hii Wakristo watakuwa na uwezo wa kusimamia mapokeo ya manabii waliohubiri hukumu dhidi ya uonevu wa aina yoyote ile. Hali hii inaweza ikawaweka katika mazingira magumu [manabii hao] ya kuwa wahanga wa mateso na maumivu. Utumishi wa Yesu ulimfanya atoe uhai wake msalabani na yeye mwenyewe

---

ambapo sura ya pili inasimulia ushirikiano kati ya makanisa kuhusiana na haki za watu wa asili wa Kanada, kupinga ubaguzi Afrika Kusini na kuleta amani Ailendi ya Kaskazini na sura yake ya tatu inaelezea mifumo ya kupambanua inayotumika katika kila jumuiya, katika PCPCU, *Information Service* N. 125 (2007/III), 121-138, na *Reformed World* 57 (2/3), Juni-Septemba 2007, 105-207.

aliwatabiria wafuasi wake kuwa wayategemee mateso na maumivu ya jinsi hiyo. Kanisa litahusisha, kwa mtu mmoja na/au jumuiya, njia ya msalaba, hata ikibidi kuifia imani (ling. 10:16-33).

66. Kanisa lina makundi yanayotofautiana kijamii na kiuchumi; matajiri na maskini kwa pamoja wanahitaji wokovu unaotolewa na Mungu peke yake. Baada ya mfano wa Yesu, Kanisa linaitwa na limepewa nguvu ya pekee ili kushiriki sehemu ya wanaoteseka na kuwatunza wahitaji na wale wanaobaguliwa. Kanisa linatangaza maneno ya matumaini na faraja yatokanayo na Injili, linajihusisha katika kazi za matendo mema na huruma (ling. Luka 4:18-19) na limetumwa kuponya na kupatanisha mahusiano ya wanadamu yaliyovunjika na kumtumikia Mungu katika kupatanisha wale waliotengana kwa sababu ya chuki na mafarakano (ling. 2 Kor 5:18-21). Pamoja na watu wote wenye mapenzi mema, Kanisa linatafuta kuutunza uumbaji, unaolia ili kushiriki katika kutafuta uhuru wa viumbe vya Mungu (Rum 8:20-22), kwa kupinga matumizi mabaya ya uumbaji na uharibifu wa nchi na kushiriki katika mpango wa Mungu wa uponyaji wa mahusiano yaliyovunjika kati ya uumbaji na kazi za mwanadamu.

**Hitimisho**

67. Umoja wa mwili wa Kristo unategemea karama ya *ushirika* ambayo Mungu anaitoa kwa wanadamu kwa neema. Kuna kuongezeka kwa muafaka kuwa ushirika, kama ushirika na Utatu Mtakatifu wa Mungu, unajidhihirisha katika njia tatu zinazohusiana: umoja katika imani, umoja kwa njia ya ushiriki wa sakramenti, na umoja katika huduma (katika hali zote, ukijumuisha huduma na misheni). Liturgia, hasa ihusuyo kusherehekea ekaristi takatifu, inatumika kama nguvu ya kuonyesha mwelekeo mpya kuhusu mwonekano wa ushirika huu katika nyakati za sasa. Liturgia inafanya watu wa Mungu wapate uzoefu wa kujumuika na Mungu na kuwa na ushirika na Wakristo wengine wakati wote na mahali popote. Wanakusanyika na viongozi wao, wanatangaza Habari Njema, wanakiri imani yao, wanaomba, wanafundisha na kujifunza, wanatoa sifa na shukrani, wanapokea Mwili na Damu ya Bwana [Yesu], na kutumwa kwa ajili ya kazi ya misheni.[1] Mtakatifu Yohana Krisostomu aliongelea juu ya madhabahu mbili: moja iliyo ndani ya Kanisa na nyingine miongoni mwa wale maskini wanaoteseka na wale wenye huzuni.[2] Likiwa limetiwa nguvu na kulishwa na kazi za liturgia, Kanisa ni lazima liendelee na kazi yake ya misheni ya Kristo iletayo uzima wa kinabii na kwa njia ya matendo ya huruma kwa ulimwengu wote na kwa kupambana dhidi ya kila aina ya uonevu na ukandamizaji, kukosa imani, na migogoro inayosababishwa na wanadamu.

---

[1] Sentensi zilizopita kwa sehemu kubwa zinarudia na kuunda upya matamko kutoka kongamano la 9 la mazungumzo ya kikanda, yaliyofanyika Breklum, Ujerumani, mwezi wa Machi 2008. Tamko linalotokana na kongamano hili, angalia *The Ecumenical Review* 61 (3), Oktoba 2009, 343-347; angalia pia http://www.oikoumene.org/fileadmin/files/wccmain/documents/p2/breklum-statement.pdf.

[2] Mt. Yohana Krisostomu, Homily 50, 3-4 kuhusu Mathayo, katika J. P. Migne, *Patrologia Graeca*, 58, 508-509.

68. Baraka mojawapo ya harakati za kiekumene ni ugunduzi juu ya nyanja nyingi zinazohusu ufuasi ambazo makanisa hushiriki, hata kama hayaishi katika ushirika ulio kamili. Kuvunjika na kugawanyika kwetu kunapingana na mapenzi ya Kristo kwa ajili ya umoja wa wanafunzi wake na unakwamisha misheni ya Kanisa. Ndio maana kuuhuisha umoja kati ya Wakristo, chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu, ni jambo linalotakiwa kufanyika kwa haraka. Kukua kwa ushirika kunajionyesha ndani ya ushirika mpana wa waaminio nak kurudi hadi wakati uliopita na kwenda hadi wakati ujao ukihusisha pia ushirika na watakatifu wote. Lengo la mwisho la Kanisa ni kuja kushikamanishwa na ushirika wa Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ili kuwa sehemu ya uumbaji mpya, kusifu na kumfurahia Mungu hata milele (ling. Ufu 21:1-4; 22:1-5).

69. "Maana Mungu hakumtuma mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye". (Yohana 3:17). Agano Jipya linamalizia na maono ya mbingu mpya na nchi mpya, iliyobadilishwa kwa neema ya Mungu (ling. Ufu 21:1-22:5). Dunia hii mpya inaahidiwa kwetu wakati wa mwisho lakini tayari ipo katika wakati huu wa sasa katika hali ya kutazamia hata sasa wakati Kanisa likidumu katika imani na matumaini katika kuhiji kwake wakati wote, likialika kwa upendo kushiriki ibada "Njoo, Bwana Yesu" (Ufu. 22:20). Kristo hulipenda Kanisa kama bwana arusi ampendavyo bibi arusi (ling Efe 5:25) na hadi wakati wa karamu ya mwana kondoo katika ufalme wa mbinguni (ling. Ufu 19:7), anashiriki na Kanisa katika misheni yake ya kuleta nuru na uponyaji kwa wanadamu hadi atakaporudi tena katika utukufu.

***Maelezo ya Kihistoria***

**Mchakato Ulioleta Andiko la Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja**

Baraza la Makanisa Duniani linajitambulisha kama "ushirika wa makanisa yanayomkiri Bwana Yesu Kristo kuwa Mungu na Mwokozi kwa kufuata maandiko na hivyo yanatafuta kutimiza kwa pamoja wito wa pamoja kwa ajili ya utukufu wa Mungu mmoja, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu."[1] Wito huu wa pamoja unayasukuma makanisa kutafuta kwa pamoja kuja pamoja na kufikia makubaliano makubwa katika mambo yahusuyo kanisa lakini wakati huo huo yakiwa bado ni sababu ya mgawanyiko wake yenyewe: Kanisa ni nini? Nini wajibu wa Kanisa katika kuitikia mpango wa Mungu wa kiulimwengu wa kuweka muhitasari wa uumbaji wake wote katika Yesu Kristo?

Katika karne zilizopita, imeonyesha namna makanisa ya Kikristo yalivyojibu maswali haya na jinsi yalivyoishi na kuendesha theologia katika hali isiyo ya kawaida ya mgawanyiko katika kanisa. Kwa hiyo haishangazi kuona mkazo mkubwa wa elimu kuhusu kanisa – swali la kitheologia kuhusu Kanisa - linasindikiza historia ya harakati za sasa za kiekumene.

Hivyo Kongamano la 1927 kuhusu imani na Utaratibu wa Ibada ulijengwa na mada saba za kitheologia. Mada mojawapo ilikuwa maalumu kwa ajili ya mjadala kuhusu asili ya Kanisa;[2]

---

[1] "Constitution and Rules of the World Council of Churches," katika L. N. Rivera-Pagan (mhariri.), *God in Your Grace: Official Report of the Ninth Assembly of the World Council of Churches,* Geneva, WCC, 2007, 448.

[2] H. N. Bate (mhariri.), *Faith and Order: Proceedings of the World Conference - Lausanne, August 3-21, 1927*, New York, George H. Doran Co., 1927, hasa uk. 463-466. *Reports of the World Conference on Faith and Order - Lausanne Switzerland August 3 to 21, 1927*, Boston, Faith and Order Secretariat, 1928, uk. 19-24.

mada ya pili ilishughulikia uhusiano kati ya Kanisa moja tunalolikiri na makanisa yaliyogawanywa tunayoyashuhudia katika historia. Kwa kufuata msingi wa majibu ya makanisa kuhusu matokeo ya mkutano,[3] walioandaa kongamano la pili la mwaka 1938 kuhusu Imani na Utaratibu wa Ibada walitoa mapendekezo kuwa mada kubwa kwa ajili ya mkutano unaofuata iwe "Kanisa kwa ajili ya Kusudi la Mungu."[4] Pamoja na kongamano la pili kutozingatia kipekee mada hii, sehemu mbili kati ya vifungu vyake vilijadili kiini cha mambo yahusuyo kanisa: "Kanisa la Kristo na Neno la Mungu" na "Ushirika wa Watakatifu."[5] Kongamano la mwaka 1937 lilihitimisha na msimamo kuwa maswali kuhusu asili ya Kanisa yalikuwa chanzo kikubwa katika mambo yaliyosababisha mgawanyiko wa [Kanisa].[6]

Mnamo mwaka 1948 kutambuliwa kwa umoja katika Kristo kuliamsha ushirika licha ya jumuiya zilizogawanyika, na kukaonyesha njia ya kuanzisha Baraza la Makanisa Duniani. Ripoti ya mkutano wa kwanza wa BMD ilitamka bayana kuwa licha ya kuwa na umoja katika Kristo, makanisa kimsingi bado yalikuwa yamegawanyika katika namna mbili za uelewa wa Kanisa unaoingiliana, ukiundwa na uelewa unaokaza "kutenda" zaidi au "kutendewa" zaidi kwenye wajibu wa Kanisa katika

---

[3] Kwa ajili ya uchaguzi wa majibu, angalia L. Dodgson (mhariri.), *Conviction: A Selection from the Responses of the Churches to the Report of the World Conference on Faith and Order, Held at Lausanne in 1927*, London, Student Christian Movement Press, 1934.

[4] L. Hodgson (mhariri.), *The Second World Conference on Faith and Order Held at Edinburgh, August 3-18, 1937*, London, Student Christian Movement Press, 1938, 5.

[5] Kitabu hicho hicho, 228-235, 236-38.

[6] Ling. O. Tomkins, *The Church in the Purpose of God: An Introduction to the Work of the Commission on Faith and Order of the World Council of Churches*, Geneva, Faith and Order, 1950, 34.

kushiriki wokovu wa Mungu duniani.[7] Ilikuwa katika hali ya mazingira haya mapya na magumu - makubaliano katika kuiishi elimu ya Kristo kuliyasaidia makanisa kutambua masalia mengine juu ya Kanisa moja wakati likibakia katika mgawanyo huu wa kikanisa na kimafundisho ya kanisa - bado Kamisheni ya Baraza la Makanisa Duniani lilifanya Kongamano lake la Tatu kunako mwaka 1952 juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada.

Kwa mara nyingine tena pasipo kushangaza, ripoti ya kwanza ya kitheologia kati ya tatu zilizoandaliwa kwa ajili ya Kongamano la Tatu la Dunia[8] lilitokana na zoezi yakinifu la kulingalisha mafundisho ya kanisa ya kiekumene. Matunda ya zoezi hili yalihaririwa katika kitabu *Asili ya Kanisa*,[9] na kitabu hiki baadaye kiliakisiwa katika sura ya ripoti ya mwisho ya Kongamano lililopewa jina la "Kristo na Kanisa Lake."[10] Hii ilikuwa ndio mada hasa ya utafiti wa ripoti[11] iliyowasilishwa miaka kumi na moja iliyofuata, katika Sehemu ya I ya Kongamano la Nne la mwaka 1963 juu ya Imani na Utaratibu

---

[7] Ling. "The Universal Church in God's Design," katika W. A. Visser't Hooft (mhariri.), *The First Assembly of the World Council of Churches Held at Amsterdam August 22nd to September 4th, 1948*, London, SCM Press Ltd, 1949, 51-57.

[8] *The Church: A Report of a Theological Commission of the Faith and Order Commission of the World Council of Churches in Preparation for the Third World Conference on Faith and Order to Be Held at Lund, Sweden in 1952*, London, Faith and Order, 1951.

[9] R. N. Flew (mhariri.). *The Nature of the Church: Papers Presented to the Theological Commission Appointed by the Continuation Committee of the World Conference on Faith and Order*, London, SCM Press, 1952.

[10] *Report of the Third World Conference on Faith and Order, Lund, Sweden: August 15-28, 1952*, London, Faith and Order, 1952, 7-11.

[11] *Christ and the Church: Report of the Theological Commission for the Fourth World Conference on Faith and Order*, Geneva, WCC, 1963.

wa Ibada, ripoti iliyoitwa "Kanisa kwa ajili ya Kusudi la Mungu."[12]

Mkazo unaofafana juu ya mafundisho ya kiekumene ya kanisa umeonyeshwa katika matamko makubwa kuhusu umoja wa Kanisa uliopokelewa katika mikutano ya BMD: tamko la New Delhi juu ya umoja "wa wote popote"[13] la mwaka 1961; Tamko la Nairobi la mwaka 1975 juu ya Kanisa moja kama ushirika wa upatanisho[14]; tamko la Canberra juu ya umoja wa Kanisa kama ushirika[15]; na tamko la Porto Alegre la mwaka 2006 kuhusu "Kuitwa Kuwa Kanisa Moja."[16] Matamko yote haya yamekuwa ni mkusanyiko wa hatua kuelekea mapatano na muafaka mkubwa juu ya mafundisho ya kanisa.

Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Ibada, ikisukumwa na maono ya kiekumene ya yenye kauli mbiu “wote kila mahali” yaliyoletwa na Roho Mtakatifu katika umoja unaoonekana katika imani ya mitume, maisha ya sakramenti, huduma na mission, imeleta kiwango kikubwa cha kazi zake zilizofuatia mkutano wa mwaka 1961 wa New Delhi pamoja, kwenye andiko la *Ubatizo, Ekaristi na Huduma*.[17]

---

[12] P. C. Rodger and L. Vischer (wahariri), *The Fourth World Conference on Faith and Order: Montreal, 1963*, New York, Association Press, 1964, 41-49.
[13] W. A. Visser’t Hooft (mhariri), *The New Delhi Report: The Third Assembly of the World Council of Churches, 1961*, London, SCM Press, 1962, 116.
[14] D. M. Paton (mhariri), *Breaking Barriers: Nairobi 1975 – The Official Report of the Fifth Assemblyof the World Council of Churches, Nairobi, 23 November – 10 December, 1975*, London-Grand Rapids, SPCK-Eerdmans, 1976, 60.
[15] M. Kinnamon (mhariri), *Signs of the Spirit: Official Report Seventh Assembly – Canberra, Australia, 7-20 February 1991*, Geneva-Grand Rapids, WCC-Eerdmans, 1991, 172-174.
[16] L. N. Rivera-Pagán (mhariri), *God, in your Grace: Official Report of the Ninth Assembly of the World Council of Churches*, Geneva, WCC, 2007, 255-261.
[17] *Baptism, Eucharist and Ministry*, Geneva, WCC, 1982.

Wakati muhimu katika kutafakari juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada juu ya mafundisho ya kanisa ni pale lilipofanyika Kongamano la Dunia mwaka 1993 kule Santiago de Compostela, Uhispania. Kuna sababu nyingi zilizofanya Kongamano hili liwe na mada yake ya "Kuelekea *Ushirika* katika Imani, Maisha na Ushuhuda." Sababu ya kwanza ilikuwa ni mafafanuzi ya majibu rasmi ya makanisa kuhusu *Ubatizo, Ekaristi na Huduma*, iliyotolewa kwenye maandiko sita.[18] Uchambuzi yakinifu wa majibu 186 ya *Ubatizo, Ekaristi na Huduma* ulihitimishwa na orodha ya mada nyingi kubwa kuhusu mafundisho ya kanisa ambazo zilitakiwa kufanyiwa utafiti zaidi: wajibu wa Kanisa kuhusu kusudi la Mungu; *Ushirika*; Kanisa kama karama ya Neno la Mungu (*creatura verbi*); Kanisa kama fumbo la sakramenti ya upendo wa Mungu kwa ulimwengu; Kanisa kama hija ya watu wa Mungu; Kanisa kama alama ya unabii na utumishi wa ufalme wa Mungu unaokuja.[19] Sababu ya pili iliyokuwa imelijenga kongamano la 1993 ilikuwa ni matokeo ya mchakato wa utafiti kuhusu Imani na Utaratibu wa Ibada "Kuelekea Maelezo ya Pamoja Juu ya Imani ya Mitume kwa Wakati Huu,"[20] ulioonyesha mapatano ya kutia moyo kuhusu yaliyomo yote kwenye mafundisho ya Imani, ikihusisha pia mafundisho yake juu ya Kanisa. Sababu ya tatu ilikuwa ni mchakato wa utafiti juu ya "Umoja wa Kanisa na Uamsho wa Jumuiya ya Watu,"[21] iliyokazia juu ya asili ya Kanisa kama alama na chombo cha mpango wa Mungu wa wokovu kwa ulimwengu. Na sababu ya nne zilikuwa ni changamoto za mafundisho ya kanisa zilizoibuliwa na

[18] Ling. *Churches Respond to BEM* Geneva, WCC., 1986-1988, nakala 1-VI.

[19] Ling. *Baptism, Eucharist & Ministry, 1982-1990: Report on the Process and Responses*, Geneva, WCC, 1990, 147-151.

[20] Ling.

[21] *Ling. Church and World: The Unity of the Church and the Renewal of Human Community*, Faith and Order Paper 151, Geneva, WCC, 1990.

mchakato wa upatanisho uliotokana na Haki, Amani na Ukamilifu wa Uumbaji.[22] Pia kulikuwa na nguvu mpya ya kiekumene ambayo umaarufu wake ulikua kutokana na elimu juu ya umoja wa makanisa katika mazungumzo ya kimaeneo na kikanda. Harakati hizi za miaka ya 1980 ziliungana na kuzaa uamzi uliochukuliwa na Kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Ibada katika mjadala wake wa wazi mwaka 1989, na kuanzisha utafiti mpya juu ya kile kilichoitwa, "Asili na Misheni ya Kanisa - Mawazo ya Kiekumene Juu ya Mafundisho ya Kanisa."[23] Mada yenyewe ya Kongamano la Tano la Dunia - "Kuelekea *Ushirika* katika Imani, Maisha na Ushuhuda" - ulitafakari michakato ya tafiti zote hizi za miaka ya 1980. Wakati *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* inachukua nafasi yake katika njia hii ndefu ya tafakari ya Imani na Utaratibu wa Ibada juu ya Kanisa, msukumo mpya ulitolewa kwa kazi hii katika Kongamano la Tano mnamo mwaka 1993.

Baada ya miaka mingi ya utafiti na mazungumzo juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada, toleo la kwanza la utafiti juu ya Elimu Kuhusu Kanisa lilichapishwa mwaka 1998 chini ya kichwa *Asili na Kusudi la Kanisa*.[24] Dhima yake kama andiko la muda lilielezwa katika kichwa kidogo: *Hatua Kuelekea Tamko la*

---

[22] "Final Document: Entering into Covenant Solidarity for Justice, Peace and the Integrity of Creation," katika D. P. Niles (mhariri), *Between the Flood and the Rainbow: Interpreting the Conciliar Process of Mutual Commitment (Covenant) to Justice, Peace and the Integrity of Creation*, Geneva, WCC, 1992, 164-190; cf. T. F. Best & M. Robra (wahariri), *Ecclesiology and Ethics: Ecumenical Ethical Engagement, Moral Formation, and the Nature of the Church*, Geneva, WCC, 1997.

[23] Ling. G. Gassmann, "The Nature and Mission of the Church: Ecumenical Perspectives," katika T. F. Best (mhariri), *Faith and Order 1985-1989: The Commission Meeting at Budapest 1989*, Geneva, WCC, 1990, hasa kurasa za 202-204, 219.

[24] *The Nature and Purpose of the Church: A Stage on the Way to a Common Statement*, Geneva, WCC, 1998.

*Pamoja*. Ni andiko lenye sura sita: "Kanisa la Utatu wa Mungu," "Kanisa katika Historia," "Kanisa kama *Ushirika*," "Maisha ya Ushirika," "Huduma ndani na kwa ajili ya Ulimwengu," na "Kufuata wito wa Ufuasi Wetu: Kutoka Kuunganisha Uelewa Wetu hadi Kutambuana kwa Kuheshimiana." Majibu ya andiko hili yalipokelewa na makanisa mbalimbali, asasi za kiekumene, na mabaraza ya makanisa ya kikanda, taasisi za elimu na watu binafsi. Maoni mengi ya kuthamini kazi hii yaliendana pia na ukosoaji wenye kujenga. Kwa mfano, ilionekana wazi kwamba andiko la *Asili na Kusudi la Kanisa* lilihitaji kushirikisha zaidi: ni jinsi gani dhana ya Kanisa kama Ushirika ingeweza kushughulikiwa licha ya kuwepo kwa sura inayohusu Kanisa la Utatu wa Mungu? Zaidi ya hayo, kulikuwa na mambo ambayo yalionekana kukosekana: kwa mfano, hakukuwa na sehemu kuhusu mamlaka ya kufundisha na mada kuhusu misheni haikuwekewa mkazo. Pia, Kongamano la Dunia la Santiago liliitisha utafiti juu ya swali la huduma ya kiulimwengu ya umoja wa Kikristo,"[25] ambao haukuwemo kwenye andiko. Kwa kiwango kikubwa, katika barua yake ya kichungaji juu ya kuhimiza kujitoa kwa ajili ya shughuli za kiekumene, *Ut Unum Sint*, akialika mazungumzo juu ya huduma ya Askofu wa Rumi, Mtakatifu Paulo wa II anarejea andiko la Imani na Utaratibu wa Ibada iliyokuwa na maono ya Kongamano la Santiago.[26]

Baada ya kutoa muda wa kutosha kwa ajili ya kupeleka majibu kwenye tume, tume iliweka muda wa kuendelea kupitia andiko juu ya mafundisho ya kanisa, ikitoa rasimu ya kwanza ya andiko

[25] T. B. Best na G. Gassmann (wahariri), *On the Way to Fuller Koinonia: Official Report of the Fifth World Conference on Faith and Order*, Geneva, WCC, 1994, 243.

[26] *Encyclical Letter Ut Unum Sint of the Holy Father, John Paul II, on Commitment to Ecumenism*, Rome, Libreria Editrice Vaticana, 1995, §89.

lililoitwa *Asili na Misheni ya Kanisa,*[27] ambalo liliwasilishwa kwenye Mkutano wa BMD uliofanyika mwaka 2006 huko Porto Alegre, Brazili. Katika kutafuta kuunganisha mapendekezo yote kutoka kwenye majibu mbalimbali, andiko hili likaja na sura nne kama ifuatavyo: "Kanisa la Utatu wa Mungu," "Kanisa katika Historia," "Maisha ya Ushirika ndani na kwa ajili ya Ulimwengu," na "Ndani na kwa ajili ya Ulimwengu." Sura ya kwanza ilijumuisha vipengele vingi vya kibiblia juu ya asili ya Kanisa kama watu wa Mungu, mwili wa Kristo na hekalu la Roho Mtakatifu, pamoja na ufahamu wa kibiblia juu ya kanisa kama *ushirika* na juu ya misheni ya Kanisa kama mhudumu wa Ufalme na uthibitisho wa kiimani wa Kanisa ambalo ni Moja, Takatifu la Ulimwengu Wote na la Kimitume. Sura ya pili kuhusu historia ilidokeza matatizo yanayoyakumba makanisa katika mipasuko ya sasa: tofauti zinawezaje kuwianishwa na umoja na nini kinafanya tofauti hizi ziwe halali? Makanisa yanaelewaje juu ya kanisa la mahali (fulani) na maana hii inahusiana vipi na makanisa mengine? Ni mambo gani ya kihistoria na yanayoendelea yanayowagawa Wakristo? Sura ya tatu iliangazia vitu ambavyo ni muhimu kwa ajili ya ushirika kati ya makanisa, kama vile imani ya mitume, ubatizo, ekaristi takatifu, huduma, uaskofu, mabaraza na sinodi, ikihusisha sasa pamoja na mada juu ya ukuu juu ya wote na mamlaka. Sura ya mwisho ilichunguza kwa kifupi kuhusu huduma ya Kanisa kwa ulimwengu katika kusaidia wale wanaoteseka, kuwalinda wanaokandamizwa, kuushuhudia ujumbe wa kimaadili wa Injili, kufanya kazi kwa ajili ya kuleta haki sawa, amani na kuyalinda mazingira, na kwa ujumla kutafuta kuboresha jamii ya mwanadamu inayotunza misingi ya maadili ya ufalme wa Mungu.

[27] *The Nature and Mission of the Church: A Stage on the Way to a Common Statement,* Faith and Order Paper 198, WCC, Geneva, 2005.

Andiko hili juu ya mafundisho ya kanisa lililohaririwa pia lilikuwa na kichwa kidogo kisemacho, "Njia Kuelekea Tamko la Pamoja," na pia lilipelekwa kwenye makanisa ili litafutiwe itikio. Zaidi ya majibu themanini yalipokelewa, ingawa ni majibu kama thelathini hivi yalitoka hasa kwenye makanisa. Majibu mengi kutoka makanisa, taasisi za elimu na kiekumene, na kwa kiwango kikubwa kutoka vyama vya kimisionari yalieleza kujiridhisha kuwa misheni ya Kanisa ilipewa umuhimu mkubwa, na hata kuwa na jina katika kichwa cha andiko. Maoni mengine hata hivyo yalikuwa na mashaka kuwa matumizi ya maneno mawili - *asili* na *misheni* - yangefunika ukweli kwamba Kanisa kwa asili ni la kimisionari. Ili kusaidia Kikosi Kazi juu ya Mafundisho ya Kanisa katika kutathmini majibu kuhusu *Asili na Misheni ya Kanisa*, watumishi wa kamisheni ya Imani na Utaratibu wa Ibada waliandaa majumuisho na uchambuzi wa awali wa kila jibu.

Hatua tatu kubwa zilichukuliwa hasa katika kutathmini andiko la *Asili na Misheni ya Kanisa*. Kwanza, Kamisheni ya Wazi Juu ya Imani na Utaratibu wa Ibada, ikiwa na wajumbe 120 wakiwakilisha makanisa mbalimbali, ilikutana Creta mwaka 2009. Kusanyiko hili liliwaleta pamoja wale wote waliokuwa wanashiriki Kamisheni hii ya Imani na Utaratibu wa Ibada kwa mara ya kwanza na mkutano uliandaliwa ili kupata mawazo mengi kadri inavyowezekana kutoka kwa wajumbe juu ya miradi mitatu ya tafiti za Imani na Utaratibu wa Ibada, na hasa utafiti juu ya mafundisho ya Kanisa. Mijadala mingi ya wazi ilitathmini *Asili na Misheni ya Kanisa*.[28] Mwelekeo mkubwa kutoka mijadala ya wazi ya Kamisheni ilikuwa kufupisha andiko na kulifanya likubaliane na mazingira husika, liakisi maisha ya makanisa duniani kote, na liweze kupatikana na

[28] Ling. John Gibaut (mhariri), *Called to Be the One Church: Faith and Order at Crete*, Geneva, WCC, 2012, 147-193.

wasomaji wengi. Vikundi kumi na mbili vilijadili kuhusu *Asili na Misheni ya Kanisa*, na vikatoa tathmini za kina kuhusu andiko hili.[29]

Pili, mnamo mwezi Juni 2010 huko Etchmiadzin Takatifu, Armenia, Kamisheni Kuu ya Ibada na Utaratibu wa Ibada iliamua kuwa baada ya kuchunguza kwa uangalifu majibu juu ya *Asili na Misheni ya Kanisa*, na kutathmini andiko kutoka kwenye mkutano wa Kamisheni ya Wazi ya Crete, ilikuwa ni muda muafaka kuanza uchambuzi wa mwisho. Kamati ya kutengeneza rasimu iliteuliwa ikiwa na watheologia kutoka makanisa ya Kianglikana, Kikatoliki, Kilutheri, Kimethodisti, Kiorthodoksi, na wenye mapokeo ya Kimatengenezo; na walioendesha utengenezaji wa rasimu hii walitoka makanisa yenye mapokeo ya Kimethodisti na Kiorthodoksi.

Tatu, Kamisheni ilijua pengo kubwa lililoachwa na katika mchakato wa majibu: kulikuwa bado hakuna jibu lenye maana kutoka makanisa ya Mashariki na ya Orthodoksi ya Mashariki ya Mbali. Kwa hiyo, ushauri wa ndani kati ya Makanisa ya Kiorthodoksi ulifanyika Aghia Napa, Cyprus, katika mji Mtakatifu wa Konstansia, mnamo Machi 2011, ambao ulijumuisha watheologia 40 kutoka Orthodoksi ya Mashariki na watatu Kutoka Orthodoksi ya Mashariki ya Mbali. Mkutano huo ulizaa tathmini ya kina juu ya *Asili na Misheni ya Kanisa*. Ushauri mkubwa ulitolewa kuingiza kwa uwazi zaidi mambo yahusuyo ubatizo, ekaristi takatifu na huduma kwenye uwasilishaji wa kile ambacho ni muhimu kwa maisha ya Kanisa. Mkutano huu wa mashauriano na taarifa vikawa sehemu muhimu ya ajenda ya mkutano wa Kikosi Kazi juu ya Mafundisho ya Kanisa, na hivyo kuwa na mchango wa kipekee katika mchakato uliopelekea kutokea kwa andiko jipya.

[29] Ling., andiko hilo hapo juu, 207-231.

Uchambuzi mpana wa majibu uliendelea katika mkutano wa kwanza wa kamati ya kuandika rasimu uliofanyika Geneva mwishoni mwa Novemba 2010. Mchakato ulipewa msukumo mpya baada ya mkutano wa ndani wa Kiorthodoksi mwanzoni mwa mwezi Machi 2011. Mkutano wa Kikosi Kazi juu ya Mafundisho ya Kanisa uliofanyika huko Kolumbus, Ohio, Marekani, baadaye katika mwezi huo huo ulitoa rasimu mpya toleo la kwanza la andiko ambalo likaja kuwasilishwa kwenye Kamisheni Kuu ya Imani na Utaratibu wa Ibada huko Gazzada, Italia mnamo Julai mwaka 2011. Maoni mengi yalipokelewa kutoka kwa wajumbe wa Kamisheni, yalipewa kipaumbele sana lakini bado yalionyesha kuwa andiko lilihitaji kukaza zaidi na kwa uwazi njia ambazo zingewezesha mchakato kuelekea makubaliano zaidi, hasa katika jambo la huduma, na kipekee katika makubaliano ya kimaeneo, na katika kazi ya karibuni ya Imani na Utaratibu wa Ibada, kama vile andiko la kitafiti la *Ubatizo Mmoja: Kulekea Kutambuana na Kuheshimiana*.[30]

Ombi hili lilishughulikiwa kwa kuziimarisha baadhi ya hoja na kuziunga mkono kwa kuzitolea maelezo ambapo zinathibitisha mchakato uliofikiwa kuelekea makubaliano. Kwa mfuatano huo, nakala nyingine iliandaliwa na kamati ya kuandaa rasimu huko kwenye Chuo Kikuu cha Kiekumene, Bosey huko Uswisi, mnamo Desemba 2011. Kamati ya kuandaa rasimu ilisaidiwa sana na mawazo kutoka kwa watumishi wa Kamisheni ya Misheni na Uinjilisti Duniani ya BMD. Matokeo ya kitabu hicho yaliwasilishwa baadaye kwa wataalamu wa nje wa mambo ya kiekumene kwa ajili ya kuyatathmini upya; maoni yao yalichambuliwa na kuingizwa na kamati ya rasimu na yakapelekwa kwenye Kikosi Kazi cha Mafundisho ya Kanisa katika kikao kilichofanyika Freising, Ujerumani, mwishoni mwa Machi 2012. Kwa msingi wa majadiliano na majibu

[30] *One Baptism: Towards Mutual Recognition*, Geneva, WCC, 2011.

kuhusu andiko katika kikao cha Freising, Kikosi Kazi kuhusu Mafundisho ya Kanisa kilihitimisha rasimu iliyotakiwa kuwasilishwa kwenye Kamisheni Kuu ya Imani na Utaratibu wa Ibada.

Huko Penang, Malaysia, andiko la mwisho liliwasilishwa kwenye Kamisheni Kuu mnamo tarehe 21 Juni 2012, ambayo kwa kauli moja ilipitisha andiko hilo kama tamko la makubaliano likiwa na kichwa *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja*. Hivyo andiko hili sio hatua ya namna ya kuelekea zaidi kwenye tamko la pamoja; ni tamko la pamoja ambalo maandiko yaliyopita - *Asili na Kusudi la Kanisa na Asili na Misheni ya Kanisa* - yalielekeza. *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* inakamilisha hatua ya pekee ya mjadala wa Imani na Utaratibu wa Ibada kuhusu Kanisa. Kamisheni inaamini kuwa mjadala wake umefikia kiwango cha ukomavu unaoweza kutambuliwa kama andiko la makubaliano, kuwa ni andiko lenye hadhi sawa na sifa kama andiko la mwaka 1982 la *Ubatizo, Ekaristi Takatifu na Huduma*. Kwa msingi huo, andiko hili linapelekwa kwenye makanisa kama rejea ya pamoja ya kuanzia ili kupima au kutambua mapatano ya mafundisho ya kikanisa kati yao wenyewe, na hivyo kutumika katika kuendeleza hija yao kuelekea kudhihirika kwa umoja ule ambao Kristo aliuombea. Kamati Kuu ya Baraza la makanisa Duniani katika kikao chake huko Crete, Ugiriki, mwanzoni mwa Septemba 2012, ulipokea andiko la *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* na kuliweka mikononi mwa makanisa washirika kwa ajili ya utafiti na kutoa majibu yao rasmi [ya umuhimu wa andiko hili].

*"Kamisheni ya BMD Kuhusu Imani na Utaratibu wa Ibada inatuleletea sisi zawadi.... Itakuwa na wajibu mkubwa katika miaka inayokuja kwa ajili ya kutambua hatua nyingine kuelekea umoja unaoonekana." - Olav Fykse Tveit, Katibu Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani*

Tunaweza kusema nini kwa pamoja kuhusu Kanisa la Utatu wa Mungu ili kukua katika ushirika, kupambana kwa pamoja kwa ajili ya haki na amani katika dunia, na kushinda kwa pamoja dhidi ya migawanyiko ya zamani na sasa? *Kanisa: Kuelekea Maono ya Pamoja* kinapendekeza jibu lenye uzito kuhusu swali hili. Likiwa limetolewa na watheologia kutoka mapokeo mbalimbali ya Kikristo na tamaduni mbalimbali, andiko la *Kanisa*, kwanza linashughulikia Misheni ya Kanisa, umoja, na asili yake ya kuwa katika maisha ya Utatu wa Mungu. Baadaye kitabu hiki kinajadili juu ya kukua kwetu katika ushirika—katika imani ya kimitume, maisha ya ekaristi takatifu, na huduma—kama ilivyo kwamba makanisa yameitwa kuishi ndani ya na kwa ajili ya dunia.

*"Kwa miaka ishirini, wawakilishi wa makanisa ya Kiorthodoksi, Kiprotestanti, Kianglikana, Kiinjilisti, Kipentekoste, na Kikatoliki... walifikiri kwa pamoja kuanika maono juu ya asili, kusudi, na lengo la Kanisa duniani, katika tamaduni mbalimbali na ushirika wa kiekumene" - Kutoka Utangulizi*

Baraza
la Makanisa Duniani